Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 14 Februari, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-**

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu zilizokaguliwa za Hifadhi ya Taifa Ngorongoro kwa Mwaka 2005/2006 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Ngorongoro Conservation Area Authority for the Year 2005/2006*).

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenye shughuli ya maswali. Napenda kuwakumbusha tu, kwa mujibu wa Kanuni zetu mpya kupongezana ni jambo ambalo limewekewa mipaka ni Kanuni ya 151(1)(2)(3). Nitaisoma tu ili kuwakumbusha kwa sababu wakati wa maswali sitaruhusu pongezi.

"(1)Endapo litatokea jambo lolote ambalo mhusika wake au mwathirika wa jambo hilo anastahili kupewa pongezi au pole na Wabunge basi Spika atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo hilo kwa niaba ya Wabunge wote. (2)Baada ya Spika, kutoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote, kwa ajili ya kuokoa muda wa majadiliano, Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa pongezi au pole kwa muhusika au mwathirika wa jambo hilo wakati wowote wa majadiliano Bungeni. (3)Kwa upande wa Serikali, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni atatoa pongezi au pole kwa mhusika au mwathirika wa jambo lolote kwa niaba ya Serikali." Niliona niseme mapema na wale wanaosema ubabe wa Spika, huu ni ubabe wa Kanuni, hizi ndizo kanuni zetu. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, baada ya hapo sasa napenda kwa niaba ya Bunge Zima kuwapongeza wenzetu wote ambao wamepata nyadhifa mbalimbali katika Serikali. Tunaamini kabisa

kwamba Baraza hili Jipya la Mawaziri chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu Ndugu Mizengo Pinda, litatimiza wajibu na matarajio ya wananchi kwa kiwango ambacho kitaitukuza nchi yetu. Ahsanteni sana. (*Makofi)*

Na. 117

**Kukarabati Barabara za Wilaya ya Kilwa**

**MHE. MHE. DUNSTAN D. MKAPA (K.n.y. MHE. HASNAIN G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima wa korosho wa Wilaya ya Kilwa wanakumbana na tatizo la kupanda kwa bei na ruzuku ya dawa za korosho kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu, hususan katika Kata za Pande, Limaria na Najirenge:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kutengeneza barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba wakulima wa Kata ya Pande, Limaria na Njirenge wanakumbana na tatizo la kupanda kwa bei ya ruzuku ya dawa za korosho kama ilivyo kwa maeneo mengine kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu.

Kutokana na hali hiyo ya kuharibika kwa miundombinu Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina mipango mikubwa ya kuimarisha miundombinu katika barabara zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya Kilwa imeweza kuyafanya yafuatayo:- Katika ya Kata ya Pande, kwa mwaka 2006/2007 Halmashauri ilitumia jumla ya shilingi milioni 106 fedha za ruzuku ya maendeleo na shilingi milioni 28 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika Barabara ya Hotelitatu hadi Pande yenye urefu wa kilomita 32 ambapo hapo awali ilikuwa na hali mbaya sana kutokana na kuwa na udongo mweusi ambao unasababisha barabara kutopitika majira ya mvua. Kwa sasa barabara hiyo ipo katika hali ya kuridhisha.

Katika Kata ya Limaria katika mwaka 2007/2008 barabara ya Limaria, Magisani imetengewa shilingi milioni 7 kwa matengenezo ya kawaida. Zabuni ya matengenezo ya

barabara hii imetengazwa na hadi sasa mkandarasi hajapatikana. Halmashauri inafanya utaratibu wa kujumuisha matengenezo haya na kandarasi nyingine katika maeneo hayo.

Katika Kata ya Najiringi kwa mwaka 2006/2007 barabara ya Kirangiragi hadi Najirenge yenye urefu wa kilomita 54 imefanyiwa matengenezo kwa jumla ya shilingi milioni 88 zilitumika kwa matengenezo hayo. Kwa mwaka 2008/2009 barabara hii itaendelea kupangiwa bajeti kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007 barabara ya Naiwanga hadi Najirenge hadi Mbwemkulu yenye urefu wa kilomita 114 imefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi. Aidha, katika mwaka 2007/2008 jumla ya shilingi milioni 127 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ukarabati wa barabara hiyo.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara toka Hotelitatu kwenda Pande bado hairidhishi, na huyo mkandarasi ameifanya hiyo barabara isipitike kabisa sasa kwa kuweka udongo usiofaa. Je, Serikali inasema nini kumchukulia hatua huyo mkandarasi ambaye ameharibu hiyo barabara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya ya Hotelitatu hadi Pande ni kweli imetengewa fedha kwa mwaka 2007/2008 na imekwishaanza kutengenezwa.

Sasa kama imetengenezwa vibaya na huyo mkandarasi. Mimi ninaomba nilifanyie kazi, nilifuatilie pamoja na Mheshimiwa Mbunge tuone ni nini kilitokea ili tuweze kutafuta suluhisho la kudumu.

Na. 118

## Ujenzi wa Wodi ya Akinamama Wajawazito

**MHE. LEDIANA M. MNG’ONG’O** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Ludewa ni kubwa na ina Kata na Vijiji vilivyokaa mbali na Hospitali ya Wilaya kwa sababu za kijiografia; na kwa kuwa, hali hiyo imewafanya wanawake wajawazito wenye matatizo kulazimika kwenda kujiongelea kupatiwa huduma za kujifungua kwenye hospitali ya Wilaya:-

Je, Serikali itajenga lini Wodi kwa ajili ya Wanawake wanaosubiri kujifungua Ludewa ili kuwaondolewa usumbufu na kupunguza vifo vinavyotokana na ujauzito?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ludewa kwa kushirikiana na wadau wengine mbalimbali kwa mwezi Desemba, 2007 ilikamilisha ujenzi wa Wodi ya Wanawake wajawazito yenye jumla ya vitanda 46. Wodi hiyo ina sehemu kuu nne ambazo ni kwa ajili ya kujifungulia yenye vitanda maalum 6, sehemu maalum kwa ajili ya kujifungulia kwa njia ya upasuaji yenye vitanda 8, sehemu ya wajawazito wagonjwa wanaosubiri kujifungua yenye vitanda 16 na sehemu ya wanawake waliojifungua kwa njia ya kawaida yenye vitanda 16. Wodi hiyo imegharimu jumla ya shilingi milioni 69. Zikiwemo fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo na michango kutoka kwa wahisani ambao ni MMI *Steel Limited*.

Mheshimiwa Spika, Wilaya inatambua umuhimu wa wanawake wote wenye vidokezo vya hatari na matatizo katika ujauzito kuwa na karibu na hospitali wanapokaribia kujifungua ili ifikapo muda wa kujifungua wajifungulie hospitali na hivyo kuhudumiwa na wataalam wenye ujuzi na vitendea kazi maalum ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Kwa kutambua hilo Wilaya imenunua jengo karibu na eneo la Hospitali ya Wilaya na kulifanyia ukarabati mdogo kama mkakati wa muda mfupi. Jengo hilo lina vitanda 13 na linatumika kwa ajili ya wanawake wenye vidokezo hatarishi katika ujauzito na wanaokaa mbali na hospitali ili kuwaondolea usumbufu na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wananchi wa Wilaya ya Ludewa kuhamasika kupata huduma za afya hospitalini wanawake wengi wajawazito wanakwenda mapema hospitalini kusubiri kujifungua. Hali hii hii imesababisha msongamano wa wajawazito kwenye jengo hilo ambalo uwezo wake ni mdogo. Ili kutatua tatizo hilo Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa katika Bajeti ya mwaka ujao yaani 2008/2009 inakusudi kupanua huduma hiyo na kiasi cha shilingi milioni 20 zinategemewa kutengwa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa wodi maalum ya vitanda 40 kwa ajili ya wanawake wanaosubiri kujifungua, na hivyo kupunguza kero ya msongamano mkubwa uliopo sasa hivi. Tungependa sana kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuitembelea Wilaya ya Ludewa mara kwa mara na kwa misaada mbalimbali ambayo amekuwa akitoa kila mara yakiwemo mashuka, sabuni kwa wajawazito hao. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri. Kwa kuwa wodi inayozungumzwa ya akinamama wajawazito wenye vidokezo vya hatari ina msongamano mkubwa na kuwafanya hao akinamama wanalala chini bila kuwa na godoro, hawana choo, choo ni kibovu, wala bafu, wala mahali pa kupikia; na kwa kuwa amesema mpaka Bajeti isubiriwe ya mwaka kesho. Je, Serikali itakuwa tayari kutengeneza bafu pamoja na choo na mahali pa kupikia haraka sana

iwezekanavyo ili kuzuia magonjwa ya mlipuko yanayoweza kutokea? Swali la kwanza.

La pili, Mheshimiwa Spika, kwa vile hao akinamama kila mmoja anakuja na chakula chake kutoka nyumbani; na kwa vile hao akinamama ni wajawazito na wanahitaji lishe bora ili kuboresha afya zao na afya za watoto wao. Je, Serikali itakuwa tayari kutoa chakula badala ya akinamama kuja na vyakula vyao kutoka nyumbani? Aidha Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa na tayari kuongozana na mimi kwenda Ludewa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika hospitali hiyo na katika wodi hiyo ya wanawake ambao wanangoja kujifungua kwa kweli *standard* yake kwa sasa hivi ipo katika hali ya chini na sisi tunafahamu kwamba kuna baadhi ya vitu ambavyo ni vibovu havipo katika hali ya kawaida. Ndiyo maana nimesema kwamba huo ni mkakati wa muda mfupi, lakini tumeona kwamba tuwe na mkakati wa muda mrefu. Lakini hata hivyo kwa hali hiyo, kama kweli sehemu hiyo haina choo na haina vile vitu vya muhimu, mimi nasema kwamba tutafanya kila njia ili kuhakikisha kwamba hizo huduma muhimu zinapatikana katika wodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la chakula nakumbuka kabisa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii alikwishakujibu hapa Bungeni kwamba mgonjwa yeyote akilazwa hospitali ni jukumu la hospitali kutoa huduma ya chakula. Kwa hiyo, wagonjwa hao wanatakiwa kuhudumiwa na hospitali na si vinginevyo. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo la Ludewa linafanana na tatizo la Kilwa; na kwa kuwa Kilwa hospitali kuu ya Wilaya ipo mbali na Jimbo la Kaskazini, na Jimbo la Kaskazini lina vijiji kadhaa ambavyo vinatumia Kituo cha Afya cha Tingi ambacho ni kidogo na hakitoshelezi mahitaji na kuna msongamano mkubwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatueleza kwamba hiyo hospitali ataifanyia ukarabati gani ili wananchi wa maeneo ya Jimbo la Kaskazini waweze kupata huduma zilizo bora kama wengine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hospitali nyingi katika nchi yetu zipo mbali na wananchi, ndiyo maana Serikali imeweka mkakati toka mwaka 2005/2006 mpaka sasa hivi mkakati wa ukarabati wa vituo vya Afya na Zahanati, na fedha hizo zimetolewa kwa awamu katika Wilaya mbalimbali. Kwa hiyo, ni jukumu la Wilaya kuchagua zile Zahanati au Vituo vya Afya ambavyo vipo mbali na hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, mimi ningemshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Wilaya yake, na mimi nitamsaidia ili kuhakikisha kwamba hicho kituo cha Afya cha Tingi kinampata zile huduma muhimu ili kitoe huduma kwa vijiji vingi zaidi.

**MHE. VUAI A. KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa swali la msingi linafanana na hali halisi iliyokuwepo katika maeneo mengi ya Mkoa wa Pwani. Nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali itatoa msaada gani au itawapa haki

gani wanawake wa Mkoa wa Pwani wanaohangaika wakati wa kwenda kujifungua wanalazimika kubeba maji na vyakula ili waondokane na adha hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali kwamba Serikali imeweka mkakati wa ukarabati wa vituo vya afya pamoja na zahanati na pia ukarabati wa hospitali za Wilaya na hospitali za Mikoa kama nilivyosikia Bungeni kwenye Bajeti iliyopita mwaka huu angalau hospitali za Mkoa zimeanza kukarabatiwa, hospitali 11. Hatafu tunaenda kwenye hospitali za Wilaya na mkakati wa Serikali wa kuanzisha zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila Kata. Mimi nina uhakika kwamba zoezi hili likifanikiwa na mpango huu ukifanikiwa kwa kweli wanawake wengi watakuwa wamejikomboa katika hali ya kutangatanga kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Naomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane kuhakikisha kwamba Mpango huu ukishaanza uendelee tushirikiane ili uweze kutekelezwa vizuri.

Na. 119

**Mradi wa Maji Chankorongo Nyakagomba**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, maji ni muhimu katika maisha ya binadamu na wanyama na kwa kuwa, Mradi wa Maji wa Chankorongo – Nyakagomba una zaidi ya miaka 30 tangu uanzishwe na haujakamilika na ndiyo tegemezi la vijiji vya chikobe, Chigunga, Kabuguzo, Ruhuha, Inyala, Chibingo, Katoro, Nyamigota na Beserere:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuukamilisha mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Jimbo la Busanda, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa Maji wa Nyakagomba ulifanyiwa usanifu na kuanza kujengwa mwaka 1976. Mradi huo ulilenga kutoa huduma ya maji kwa vijiji sita (6) vya Chankorongo, Chikobe, Chigunga, Kabuguzo, Ruhuha na Nyakagomba katika Jimbo la Busanda. Kutokana na uhaba wa fedha mradi ulisimama kujengwa mwaka 1988 baada ya kutekeleza asilimia 85 ya mradi mzima. Katika mwaka 2002, mradi huo ulifanyiwa tathmini kwa lengo la kuainisha kazi za kukamilisha mradi. Kazi

zilizoainishwa ni pamoja na kukamilisha ufungaji wa mabomba ya usambazaji maji na ukarabati wa tanki na vituo vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali sasa la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Geita imeandaa vijiji 10 vitakavyotekeleza Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika hatua ya kwanza. Kati ya hivyo, vijiji 4 vya Nyang'holongo, Chigunga, Nyakamwaga na Nyakagwe vipo katika Jimbo la Busanda. Mchakato wa kupata Wataalamu Washauri watakaohamasisha wananchi, kufanya usanifu wa miradi na kuisimamia, ulianza mwezi Oktoba mwaka 2007, ambapo watalaamu hao wanatarajiwa kupatikana ifikapo mwezi Juni, 2008. Mpango uliopo ni kuwa watalaamu hao watafanya pia uchunguzi na usanifu wa mradi wa Chankorongo – Nyakagomba katika mwaka wa fedha 2008/2009 ambapo gharama za kukamilisha mradi zitafahamika na hatimaye mradi huu kuanza kujengwa. Baada ya mradi huo kukamilika, vijiji vya Chikobe, Chigunga, Kabuguzo na Ruhuha alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, ambavyo vinategemea mradi huo, vitapata maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, kiasi cha shilingi 475,773,250/= zilitumwa Wilayani Geita kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya Wilaya. Kijiji cha Katoro ni miongoni mwa vijiji ambavyo hivi sasa vinatekeleza miradi kwa kutumia fedha hizo, ambapo pampu itafungwa katika kisima kilichopo na huduma kupatikana. Ninamshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili vijiji vya Inyala, Chibingo na Nyamigota viwekwe katika mipango ya Wilaya na kuitengea fedha.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Mradi huu kama ilivyoelezwa katika jibu la msingi ulianza mwaka 1976 na upo na miradi mingine inafanyika katika nchi hii. Sasa kutokamilika mradi huu Serikali haioni kwamba ni aibu kwamba fedha zilizikwa chini na hazihudumii wananchi ambao wanaona zilikufa kule kule chini. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Maji aliyeingia sasa anafahamu vijiji vizuri sana hivi na aliwahi kwenda kule akafanya harambee na akafanya shughuli mbalimbali kule. Wananchi wakamlilia kuhusu maji ingawaje alikwenda kufanya kazi nyingine. Je, anawaahidi nini kwamba katika Bajeti ijayo mradi huu ataukamilishwa? Au tuseme anawapa matumaini gani wananchi wa vijiji hivyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, kwa majibu mazuri alilyotoa na ninapenda niongezee kwa kufuatana na hilo jibu nzuri kwamba Wizara ya Maji walitembelea huko na pia walifanya mazungumzo na wanavijiji wa sehemu hizo na ni kweli kwamba mradi huo kama ilivyoelezwa kwamba ulikuwa umesimama. Hata hivyo, Wizara ya Maji ilishirikiana na wanakijiji na kutoa uamuzi wa kuhakikisha kwamba mradi huo unakuwepo na hapo hapo ukaingizwa katika vijiji kumi vya Wilaya ya Geita.

Kwa hivi, mradi huo upo katika hatua nzuri kwani hakuna mabadiliko, mradi huo utapewa maji kwa sababu kinachongojewa ni mshauri ambaye ataweza kwenda kuongea na wanavijiji ili waweze kukubaliana na teknolojia na miundombinu ya kutumia kwa ajili ya kuleta maji kwenye vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, namtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huo upo na awafahamishe wanavijiji na wanaotusikia wasikie kwamba ni kweli mradi huo utatekelezwa wakati huo huo kipindi cha pili cha mwaka huu. *(Makofi)*

Na. 120

**Mradi wa Maji Geita**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na ahadi nyingi za Mji wa Geita kupatiwa maji; na kwa kuwa, mpango huo huwa moto sana wakati wa uchaguzi na baada ya hapo huwa kama maji baridi:-

Kama wafadhili hawatekelezi ahadi yao ya kuupa Mji wa Geita maji. Je, Serikali iko tayari kutoa fedha zake za ndani ili kukamilisha mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Jimbo la Geita, kama ifuatavyo:-

Mji wa Geita unapata huduma ya Maji kutokana na vyanzo mbalimbali ambavyo ni mradi wa maji ya mtiririko kutoka katika chemichemi ya Kagera na jumla ya visima virefu 27 ambavyo vimechimwa na Halmashauri ya Wilaya kupitia mipango mbalimbali. Huduma hiyo haitoshi kwani ni sawa na asilimia 13 tu ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la maji katika Mji wa Geita, juhudi mbalimbali zimefanyika ili kupata ufumbuzi wa muda mfupi na muda mrefu wa tatizo hilo.

Katika mwaka wa fedha 2006/2007, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imeboresha visima virefu vitatu vya Bombani, Kagera na Na.14 Kambarage kwa kubadilisha pampu kwa lengo la kuongeza kiwango cha upatikanaji maji.

Uboreshaji huo umeongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka mita za ujazo 2,298 hadi 2,333 kwa siku.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ikishirikiana na Shirika lisilokuwa la Kiserikali la *Plan International* imechimba kisima kirefu chenye uwezo wa kutoa kiasi cha meta za ujazo 9 kwa saa.

Kiasi hicho cha maji kitaongeza uzalishaji wa maji Mjini Geita. Hadi sasa, ujenzi wa nyumba za mashine umekamilika, ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji na uchimbaji wa mitaro kwa ajili ya kufunga mabomba unaendelea ikiwa ni pamoja na katika maeneo ya Tambuka Reli.

Mheshimiwa Spika, ili kupata ufumbuzi wa muda mrefu wa tatizo hili, mwaka 2005, wataalam kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza walipima na kufanya usanifu wa mradi wa maji kutoka eneo la Senga Mchangani hadi Geita kwa kutumia Ziwa Victoria kama chanzo cha maji. Wizara yangu iligharamia kazi hiyo kwa kiasi cha shilingi milioni 15.

Gharama ya mradi huo ilikadiriwa kufikia shilingi bilioni 18.6. Kutoka na mahitaji makubwa ya fedha na ufinyu wa fedha Serikalini, mradi huo haujatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 kiasi cha shilingi milioni 734 kimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji Geita mjini kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mamlaka ya Maji Mjini Geita imeombwa kuwasilisha mapendekezo yao yakionyeshwa mahitaji ya fedha kwa ajili ya kutekeleza kazi zinazohusu hatua ya muda mfupi kulingana na fedha zilizotengwa. Wizara yangu itatuma fedha Wilayani Geita mara nitakapopata mapendekezo ya Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kushirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali la *Plan International, UNHABITAT* pamoja na mashirika mengine ili kuwapatia wananchi wa Mji wa Geita huduma bora zaidi ya maji.

Hatua ya Serikali kutafuta msaada kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji nchini inatokana na uhaba wa fedha za Serikalini kwa sasa.

Hata hivyo, Serikali iko tayari kutoa fedha zake za ndani ili kutekeleza mradi wa maji wa Geita Mjini kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amesema kwamba wananchi wa Geita wanapata maji kwa asilimia 13 tu ambapo Sera ya Serikali inasema ni asilimia 60. Sasa basi, kwa kuwa maji wanayopata wananchi wa Geita ni ya visima na ya visima kwa Geita mengi yana zebaki. Je, Serikali inasemaje kutekeleza mpango wake wa muda mrefu wa kutoa maji Ziwa Victoria utatekelezeka lini?

Swali la pili, kwa kuwa kulikuwa na utaratibu na viongozi wa Serikali walikuwa wanakuja Geita wanasema kwamba *MCC* italeta maji kutoka Senga mpaka Geita na mpaka sasa hivi sijasikia *MCC* italeta lini Geita. Je, Serikali inasemaje kuhusu huo mradi?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mabina na wananchi wa Geita kwamba kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu tunafanya mipango ya kuwa na ufumbuzi wa kudumu Geita na kwa sasa hatua za haraka tayari zimetengwa zaidi ya shs. 700 milioni hii ikiwa ni pamoja na kutekeleza hatua za haraka katika miji ya Geita, Misungwi, Tarime, Bunda na Bukoba. Kwa muda wa kati tunaingiza Geita katika mpango wa maendeleo ya sekta ya maji *WSDP* tukiwa na lengo la kufika huko huko katika kutatua tatizo la maji Geita pamoja na miji mingine.

Mheshimiwa Spika, maswali mawili ya leo yote yamehusu Geita na napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Geita ni moja ya maeneo ambayo nitayatembelea mapema iwezekanavyo kwa sababu nilikuwa nimepanga kwenda huko kwa shughuli za mazingira sasa nitabadilisha ratiba kidogo ili iwe ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nilikuwa na swali dogo la nyongeza. Miradi ya wawekezaji inapoingia nilidhani ndio wakati mzuri kama kuna mahitaji ya maji kuwaeleza ili waingize kwenye programu zao.

Sasa Serikali ilizungumza na wawekezaji wakati wanavuta bomba kuleta *Geita Gold Mine* kwa kiwango gani? Kwa sababu pale pangekuwa pametosheleza *GGM* pamoja na Geita. Serikali ilikuwa *involved* kwa kiwango gani? (*Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kufuatana na wawekezaji wa *Geita Gold Mine* wenyewe katika mikakati yao walikuwa na mpango wa kujenga visima viwili na pia Serikali kwa wakati huo huo yenyewe ilijenga visima viwili. Lakini hata hivyo *Geita Gold Mine* ni kwamba mimi niliwahi kufika kule wakati nikiwa Naibu Waziri na kuweza kuona hali halisi na wenyewe ni watu ambao tumeongea nao kwamba tukiwapelekea mahitaji mengine pia hawatakuwa wabaya kutukatalia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kitu ambacho tulichokuwa na mategemeo nayo makubwa ilikuwa ni mradi kwa kupitia wafadhili MCC, lakini baada ya kuwapelekea MCC Mradi wetu wa Maji na wenyewe walileta wataalamu wao wakauangalia lakini kwa vigezo vyao wenyewe waliona kwamba mradi ule hawataufadhili na baada ya hapo Serikali hatukukaa nyuma kama Mheshimiwa Waziri alivyoongea tulitenga fedha zetu shilingi 734 milioni kwa ajili ya kuaanzishia mradi huo na baada ya hapo Serikali haitasita na iko tayari yenyewe itaendelea kutoa fedha zake za humu ndani kuhakikisha kwamba mpaka Geita inapata maji ya kuwatosha. Kwa sasa kinachotakiwa ni kwamba hizi shilingi 734 milioni ni sasa wenyewe Wilaya ya Geita wapange mchakato na

mahitaji yao ya kuanzia ili fedha hizo waweze kupewa waanze pole pole na Serikali itakuwa ikiongeza mwaka hadi mwaka mpaka tuhakikishe Geita itapata maji.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa Serikali ama juhudi za Serikali zinazofanywa kuwawezesha wananchi wa mji wa Geita kupata huduma ya maji kama ambavyo vile Mheshimiwa Diallo ameuliza suala la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imekuwa na mazungumzo na wamiliki wa Mgodi wa *Geita Gold Mine*, tunajaribu kuangalia ni jinsi gani wanaweza kushirikiana na Serikali kutoa ujenzi wa miundombinu hatimaye kutoa huduma ya maji katika Mji wa Geita kwa maana ya wao kuufadhili mradi. Tumeshafanya tathmini ya gharama na imeshabainika na zinahitajika kama bilioni 13 lakini bado tunaendelea na mazungumzo kuona ni jinsi gani mradi huo tutautekeleza baada ya kukamilisha mazungumzo yanayoendelea. Kwa hiyo, nilitaka kutumia nafasi hii kuwaarifu wananchi wa Geita kwamba juhudi mbalimbali kutoka katika sekta na Wizara mbalimbali za Serikali zinaendelea kuweza kuwafanikishia wananchi wa Geita kupata huduma ya maji. *(Makofi)*

Na. 121

## Mchakato wa Ujenzi wa Mgodi wa Buzwagi

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mchakato wa ujenzi wa miundombinu ya mgodi mpya wa Buzwagi – Kahama unaendelea vizuri, na kwa kuwa, kipindi kirefu nyuma kabla ya Serikali kusaini mkataba wa Kampuni ya Barrick wananchi wa vijiji vya Mwendakulima, Mwime, na Chapulwa kwenye Kata ya Mwendakulima waliomba kupitia Mbunge wao Waziri au Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini atembelee eneo hilo kuona hali halisi ya mchakato mzima wa mgodi na kuzungumza nao juu ya Maendeleo yao katika mazingira ya mgodi, ombi ambalo lilikubaliwa lakini halijatekelezwa:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha viongozi hao kutotekeleza ahadi hiyo iliyotolewa Bungeni?

(b) Je, ni sababu gani za msingi ziliwafanya Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali walipotembelea migodi iliyomilikiwa na Kampuni ya Barrick ukiwemo na mgodi wa Buzwagi mapema mwezi Oktoba 2007 kushindwa kukutana na viongozi wa Serikali ya Kata walipotembelea Buzwagi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Nishati na Madini iliahidi kuutembelea mradi wa Buzwagi wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kujionea maendeleo ya ujenzi wa mgodi huo. Baada ya Mkutano wa Nane wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Wizara yetu ilimtuma Kamishna wa madini kuzuru eneo la Mradi wa Buzwagi ikiwa ni utekelezaji wa ahadi tuliyoitoa Bungeni. Kamishna wa Madini alitembelea Mgodi wa Buzwagi mara mbili kati ya mwezi Novemba 2007 na Februari, 2008.

Mheshimiwa Spika, safari ya kwanza ilikuwa ziara ya kikazi aliyoifanya tarehe 22 Novemba, 2007. Katika ziara hiyo Kamishna wa Madini alitembelea shughuli za Mgodi zinazoendelea. Safari ya pili ilikuwa wakati wa ziara ya Kamati ya Rais iliyofanyika tarehe 12 Janarui, 2008. Kamati hiyo ilikutana na Wananchi wa Kijiji cha Mwendakulima na kufanya mkutano wa hadhara ambapo Kamishna wa Madini alitumia nafasi hiyo kufafanua mambo muhimu yaliyoulizwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kata ya Mwendakulima katika Wilaya ya Kahama kuwa baada ya Mkutano huu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Waziri au Naibu Waziri wa Nishati na Madini atatembelea mradi wa Mgodi wa Buzwagi kwa lengo la kuona shughuli za ujenzi wa Mgodi huo pamoja na miundombinu yake na pia kukutana na wananchi wa vijiji vya Mwendakulima, Mwime na Chapuliwa.

(b) Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba 2007 Makatibu Wakuu wa Wizara walikuwa na ziara ya kujifunza shughuli za migodi mbalimbali nchini na walitembelea migodi ya dhahabu ya Bulyanhuku -Wilayani Kahama, Tulawaka -Wilayani Biharamulo, North Mara – Wilayani Tarime na mgodi wa almasi wa Mwadui -Wilayani Kishapu.

Mheshimiwa Spika, ziara hiyo iliandaliwa na Wizara ya Nishati na Madini kwa lengo la kuwapa Makatibu Wakuu wa Wizara na watendaji wengine Serikalini ufahamu mpana wa shughuli za uchimbaji mkubwa na uchenjuaji wa madini ya dhahabu na almasi ili waweze kushiriki ipasavyo katika mchakato wa kudurusu sera na sheria ya madini, pamoja na sera na sheria zingine zinazogusa sekta ya madini. Kwa kuzingatia kuwa mradi wa Buzwagi bado uko katika hatua ya ujenzi wa mgodi na miundombinu yake, Makatibu Wakuu hawakupangiwa kuutembelea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mradi huu unategemewa uingie kwenye hatua ya mgodi mwishoni mwa mwaka huu 2008. Kama ilivyofanyika kwa migodi niliyoitaja hapo awali. Utaratibu huu wa kujifunza pamoja na kufanyia tathmini shughuli za migodi itafanyika kwa mgodi huu wa Buzwagi vile vile.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa mgodi huu tarajiwa unaendelea kwa kasi ikiwa pamoja na ujenzi wa uzio kuzunguka eneo lote la mgodi na hivyo kusababisha kufungwa kwa barabara na njia zote zilizokuwa zikitumika na wananchi kutoka eneo moja kwenda eneo lingine, hali ambayo imeleta manung'uniko na usumbufu mkubwa. Je, Serikali inatambua kwamba hilo

ni tatizo na kama inatambua hivyo ni kwa nini mpaka hivi sasa mgodi hauonyeshi dalili zozote za kutengeneza barabara na njia mbadala ili kuwarahisishia wananchi hao mawasiliano kama ilivyokuwa hapo awali?

Pili, kwa kuwa Mkataba wa Buzwagi bado ni kitendawili sio tu miongoni mwa wananchi wa Kata ya Mwendakulima Wilaya ya Kahama na mimi mwenyewe Mbunge wa eneo hilo na kwa kuwa katika siku za nyuma baadhi ya magazeti yalichapisha mkataba huo wa Buzwagi.

Je, Serikali inaweza kuuthibitishia umma wa Tanzania na hususan wananchi wa Buzwagi kwamba mkataba ule ni sahihi na kama sio sahihi je, Serikali inaweza kunipa mimi Mbunge wa eneo nikauona ili niwathibitishie wananchi wa eneo hilo kwamba huo ndio mkataba wa Buzwagi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya kwanza ya swali lake la nyongeza. Niseme Wizara yetu mpaka tunapoongea sasa hivi ina taarifa ya migogoro miwili kimsingi katika eneo hilo la Mwendakulima ambapo mradi wa ujenzi wa Mgodi wa Buzwagi unaendelea. Kuna tofauti ya tafsiri na makubaliano kuhusu fidia kwa wananchi ambao wako katika eneo hilo. Lakini kuhusu suala la njia kwa kweli Wizara yetu ilikuwa haijapata taarifa yoyote. Lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge yeye na sisi tukae pamoja tuone kama imejitokeza kama tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, kuhusu mikataba napenda tena kutumia nafasi hii kuliarifu Bunge hili Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba kama ambavyo Mheshimiwa Spika, umekuwa ukifafanua utaratibu wa kuona mikataba hii ya Serikali ambayo inaingiwa na wawekezaji wengine ama washiriki wadau wa maendeleo kuna utaratibu wake wa kuiona.

Kwa hivi napenda kutumia nafasi hii kumkumbusha Mheshimiwa Lembeli, Mbunge, kaka yangu, kwamba kama atapenda kuona mkataba huo naomba afuate taratibu za kawaida ambazo zinafahamika na hatimaye tuone kujiridhishe kwa kile ambacho angependa kukifahamu. Lakini vinginevyo hatuna mashaka na napenda kumhakikishia kwamba mkataba ule umefungwa kutokana na misingi ya sheria na taratibu za nchi kama zinavyoelekeza. Haikuwa zaidi ya hapo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Kabla sijamwita mwuliza swali linalofuata ningependa kufafanua kwamba vile viti nyuma ya Waheshimiwa Manaibu Mawaziri Dr. Nkya na Dr. Wanyancha si vya Mawaziri tena. Mnakumbuka Baraza la Mawaziri limepunguzwa, kwa hiyo, msiviache naona vimekuwa wazi pale ni vitu vizuri tu naomba mvitumie. (*Makofi)*

Na. 122

**Ahadi ya Kupeleka Umeme Vijiji vya Arumeru**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nishati ya Umeme ni kichocheo cha maendeleo na kukuza uchumi, kwa kuwa Serikali iliahidi kupeleka umeme katika baadhi ya vijiji vya Arumeru vikiwemo vijiji vya Sambasha, Timbolo, Nduruma, Oldonyosambu, Mlangarini na Oljoro.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake kwa wananchi wa Vijiji husika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elisa Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Sambasha, Timbolo, Nduruma, Oldonyosambu, Mlangarini na Oljoro vilikuwa vimepangwa kupatiwa umeme chini ya mradi wa *Electricity Rural Transformation (ERT).* Baada ya Mradi wa *ERT* kusitishwa vijiji vya Nduruma, Mlangarini na Oljoro Jeshini vilipatiwa umeme wakati wa utekelezaji wa mradi wa "*Electricity IV, Phase II.* Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vilivyobaki vya Sambasha, Timbolo, Oldonyosambu na Oljoro na miradi mingine. Mara tu fedha zitakapopatikana vijiji hivyo vitapatiwa umeme.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika kijiji cha Midawe Serikali imeweka nguzo na nyaya za umeme katika kijiji hicho lakini hakuna *transfoma.* Je, Serikali itaweka lini *transfoma* ili wananchi wa kijiji cha Midawe wapate huduma ya umeme?

Swali la pili, kwa kuwa mwaka 2005 Serikali ilianzisha Mfuko wa Kusambaza Umeme Vijijini na ilikuwa na shilingi 10 bilioni. Je, fedha hizi haziwezi kutumika sasa ili kuchochea kasi ya usambazaji wa umeme vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba ipo katika Sera za Serikali kusambaza umeme vijijini. Kama tulivyosema ni nia ya Serikali kusambaza umeme kupitia Mradi wa *Electricity V Phase II* na tumeshaanza kufanya hivyo kwa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa suala hili linategemea na upatikanaji wa fedha basi Serikali ichukue jukumu la kuangalia gharama husika ni ya kuwasilisha umeme na kuangalia uwezekano wa kufikisha umeme kwenye kijiji hicho cha Midawe kwa kuweka hiyo *tranfoma* kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la shilingi 10 bilioni kumi ambazo zipo kwa ajili ya Mradi wa Maendeleo wa Usambazaji wa Umeme. Nadhani tukubaliane kwamba hili ni swali linalohusiana na mipango ya ujumla ya usambazaji wa umeme katika maeneo yote ya Tanzania na hivyo naomba Mheshimiwa Mbunge anipe nafasi ya Wizara yangu

kuangalia utekelezaji na mipango ya jumla ya usambazaji umeme ili tulitumbukize suala hili katika mpango huo wa jumla wa usambazaji umeme.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la *tranforma* katika kijiji cha Midawe tunalichukua na tutalifanyia kazi kwa sababu nguzo zipo lakini pia ni katika ule mpango wa ujumla wa utekelezaji wa usambazaji umeme vijijini kwamba tunaanzia na Makao Makuu ya Wilaya na hatimaye tutakwenda kwenye maeneo ambayo yana miradi mikubwa ya uzalishaji na kwa kweli pia hatua ya tatu ni kwa wale ambao tayari wameshafikishiwa miundombinu ikiwemo kama hiyo anavyosema Mheshimiwa Mbunge suala la nguzo kufikia katika eneo na ni maeneo ambayo tunayapa kipaumbele.

Lakini napenda kulitaarifu Bunge letu Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba matumizi ya zile fedha bilioni 10 ambazo tulipata kutoka kwenye Bajeti ambayo tunaendelea sasa hivi yanaendelea vizuri na sasa tunaendelea na maandalizi katika hatua za mwisho. Ni kweli tutaanza mwezi huu Februari kutekeleza ama kufikisha huduma ya umeme katika Wilaya za Kilolo, Kilindi, Mkinga, Uyui, Bahi maeneo ya *Matema Beach* kule tutafika pia Oswald Mang'ombe kule Mkoa wa Mara, Mto wa Mbu lakini pia tutakwenda kutoa fidia kwa mradi wa umeme hasa hii njia ya kuelekea Mkoa wa Lindi kutokea Mkoa wa Pwani. Hayo ndiyo maeneo ambayo yatafaidika kwa sasa hivi kwa huu mpango wa fedha bilioni 10 ambazo tumezipata. Lakini kama ambavyo tumesema tutaendelea kuwaomba kwamba muendelee kutuunga mkono ili hatimaye Wizara hii ipewe fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya kuongezea uwezekano wa kuwafikishia wananchi wa vijiji maeneo ya vijijini huduma za umeme.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa kijiji cha Malya nguzo tayari zimeshawekwa na hela zilishatengwa na ulitegemea kwamba umeme utakuwa umeshawekwa pale mwezi Desemba, 2007. Sasa naomba niulize Serikali inatuambia nini wanakijiji wa Malya ule umeme utawaka lini?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tumekuwa tukiwaeleza wananchi kwamba kwa miradi ambayo sasa hivi nimeshamaliza kusema ambayo miundombinu imefika ni mojawapo ya maeneo ambayo tunayapa kipaumbele. Narudia tena kuwahakikishia wananchi wa Malya na sehemu zingine ambazo miundombinu ipo nakumbuka maeneo ya Mheshimiwa Zambi kwamba haya ni maeneo ambayo tunayapa kipaumbele na tutawafikishia huduma. Tulikuwa tunasubiri utokaji wa fedha na kwa kweli tunaamini kwamba baada ya muda si mrefu utekelezaji utakuwa unaendelea kwa sababu mipango kimsingi imeshakamilika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la kupeleka umeme katika vijiji vyetu linaweza kupeleka umeme katika vijiji vyetu linaonekana sasa kuwa ni suala

linalochukua muda mrefu na ni kero kubwa sana kwa wananchi na hasa hao wavijijini, wakiwemo wananchi wa vijiji vya Peramiho, Igawisenga, Wino, Gumbilo, Lilambo na vingine vya jimbo la Peramiho.

Je, Serikali sasa iko tayari kutoa tamko rasmi huu mkakati wa kuweka umeme vijijini ni lini hasa utaanza ukizingatia tumeshatenga fedha katika Bajeti ya mwaka huu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuwakumbusha wananchi tamko tumeshalitoa utekelezaji wa mpango wa kusambaza umeme vijijini umeshaanza. Kama nilivyokwishasema muda mfupi uliopita kwamba sasa hivi tunaanzia na maeneo haya ambayo nimekwishakuyataja. Lakini kwa kweli tuseme kwa moyo wetu kwa kutanua zaidi kutoa huduma hii unatokana na kiwango cha fedha ambacho tunacho, lakini nampa matumaini Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadri tunavyopata pesa tutazidi kuyafikia maeneo mengi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wakati tunaendelea ningependa kwa heshima kutambua kuwepo wa Mama Tunu Mizengo Pinda, mke wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *Speaker's Gallery*. *(Makofi)*

Karibu sana Mama. Karibu sana. (*Makofi/Kicheko)*

Na. 123

**Kuongeza Mahakama za Mwanzo na Mahakimu**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA(K.n.y. MHE. VICTOR MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Chunya ina Mahakama za Mwanzo katika Kata tano tu kati ya Kata ishirini na tatu; na kwa kuwa, kiuhalisia Mahakama hizo zinahudumiwa na Mahakimu wawili tu:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Mahakama za Mwanzo Wilayani Chunya ili idadi ya Mahakama iendane na hali halisi?

(b)Je, Serikali inasema nini kuhusu idadi ya Mahakimu waliopo Wilayani Chunya?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

(a) Wilaya ya Chunya ina Mahakama za Mwanzo tisa (9) ambazo ni Chunya Mjini, Mwambani, Itete, Kupatingatinga, Totowe, Makongolosi, Sangambi, Udinde na Ikumbukwa.

(b) Ninakiri kuwepo kwa upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo nchi nzima ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Chunya. Wilaya ya Chunya kwa sasa inao Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo watatu (3) baada ya hivi karibuni kupeleka Hakimu mmoja. Idadi yao ingekuwa wanne (4) lakini mmoja wao kwa bahati mbaya alifariki dunia hivi karibuni, Mungu alilaze roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mahakama nyingine zinatembelewa na hao Mahakimu watatu waliopo Wilayani. Mahakama ya Tanzania itaendelea kuwagawa Mahakimu kwa kadri watakavyokuwa wanapatikana. Wilaya ya Chunya nayo itapatiwa Hakimu katika utaratibu huu.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri yeye mwenyewe kwamba kati ya Kata 23 kuna Mahakimu watatu (3) tu na kwa sababu Mahakama ndio sehemu pekee ya mwisho ya kutoa haki. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba pengine ingekuwa ni vyema kwa hao Mahakimu watatu (3) wakapatiwa nyenzo za usafiri ili kusudi waweze kuhudumia angalau nusu ya Wilaya ya Chunya?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nimekiri kuwepo kwa upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Ni kweli na nitampa mfano katika Wilaya ya Nachingwea yenye Kata 27 wapo Mahakimu watatu (3) si zaidi. Kweli sasa hivi Wizara yangu inajitahidi sana kutoa msaada wa usafiri kwa Mahakimu wachache ili waweze kuzitembelea Mahakama hizi zingine kutoa huduma hii muhimu kwa watu. Lakini ni mpango mkubwa tulionao kwenye *Legal Sector Reform Programme* kwanza kuongeza namba ya Mahakimu. Kwa hiyo, tunaongeza tunasomesha Mahakimu wengi zaidi ili tuweze kuwagawa watosheleze katika zile Mahakama ambazo tunazo. Masuala ya usafiri tunaendelea kwa kutoa mikopo lakini vile vile sasa kwa mfano kila Wilaya inao usafiri na usafiri huo wa Wilayani ndio unaotumika kuwasafirisha Mahakimu hawa wa Mahakama za Mwanzo kutembelea Mahakama zao.

**SPIKA:** Maswali mafupi tu moja moja kwa Mheshimiwa Luhahula na jirani yako Mheshimiwa Ruth Msafiri.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la Mahakimu lililoko Lupa linafanana sana na tatizo la upungufu wa Mahakimu uliopo Wilayani Bukombe; na kwa kuwa haki ya mwananchi inapatikana katika Mahakama; na kwa kuwa katika Wilaya ya Bukombe kwa muda mrefu sasa tangu niingie Bungeni tumetenga nyumba ambayo itatumika kama Mahakama ya Wilaya; na Serikali imekuwa ikiahidi kwamba Hakimu huyo anakuja. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Bukombe kuhusiana na haki zao za Kiwilaya waendelee kutembea kwa kilomita mia kwenda Kahama au inasemaje?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ni kweli tatizo la Hakimu Wilayani Bukombe tunalifahamu na ninataka nimwahidi sasa kwamba tutalishughulikia kwa nguvu zote ili tutakapokutana tena Bunge lijalo basi yule Hakimu awe amefika pale Bukombe.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ndiyo yaliyoko katika Jimbo la Muleba Kaskazini, ngazi ya Mahakama ya Mwanzo. Lakini tatizo kubwa zaidi na sugu limekuwa katika Mahakama ya Wilaya ama tunapata Hakimu wanaokwenda masomoni au wanaokuja na kuondoka. Je, Serikali inataka kutuambia nini kwa karibu miaka saba sasa tunakabiliana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kama nilivyokiri awali kabisa kwamba tunalo tatizo kubwa la Mahakimu hasa wa Mahakama za Mwanzo lakini pia wa Mahakama wa Wilaya. Hili la Wilaya nataka nimwahidi Mheshimiwa Ruth Msafiri kwamba nalo tutalishughulikia kwa nguvu zote kwa sababu tunaamini sasa hivi karibu tunatoa tena Mahakimu wengine kutoka Chuoni na mara tukishawapata basi tutampelekea Hakimu mmoja pale Muleba ili wananchi waweze kupata huduma hii muhimu ambayo wanaihitaji.

Na. 124

**Huduma ya Bima Nchini**

**MHE. SIJAPATA FADHILI NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya Bima hutakiwa kwa Watanzania wote kwa hali iliyopo sasa huduma hiyo hushughulikiwa na mtumishi wa ofisi *(desk officer)* badala ya Wakala wa Bima anayemjua mteja kuanzia anapochangia (*premium*) kila mwezi mpaka Bima yake inapoiva, hali inayoleta udhaifu kiutendaji wa warithi wa wateja waliofariki kuwa vigumu kulipwa au kuchukua muda mrefu kinyume na mkataba unavyosema:-

(a) Ni lini Warithi wa wateja walifariki watapata malipo yao bila usumbufu?

(b)Kwa kuwa wakala ndiye anayemjua mteja tangu mwanzo wa Bima mpaka inaiva. Je, kwa nini *desk officer* anashika madaraka hayo badala ya wakala?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Warithi wa wateja waliofariki hawapaswi kusumbuka au kucheleweshewa malipo ya Bima mara mteja anapofariki. Maandalizi ya malipo yanapaswa kufanyika mara kampuni ya Bima husika inapopokea taarifa zote muhimu za Bima yenyewe. Hata hivyo uzoefu unaonyesha kwamba mara nyingi warithi wa wateja ama wanachelewesha ama wanawasilisha taarifa pungufu. Taarifa hizo ambazo ni pamoja na hati ya Bima, hati ya kifo, hati ya uthibitisho wa uteuzi wa msimamizi wa mirathi n.k. zinahitajika kwa lengo la kuhakikisha kuwa malipo yanafanywa kwa warithi halali. Warithi wa wateja wa Bima wanaweza kuepuka usumbufu na hivyo kulipwa madai ya Bima kwa wakati iwapo wateja wenyewe wakiwa hai watateua warithi wao mapema ili waweze kuandikishwa

katika mkataba wa Bima. Endapo utaratibu huu mzuri utafuatwa warithi watapata malipo yao mapema mara kifo cha mteja kinapotokea. Hili ni jukumu mojawapo wa Wakala wa Bima kumshauri mteja wake kufanya hivyo mara anapoamua kukata Bima yake.

(b)Mheshimiwa Spika, wakala wa Bima hawawezi kushika madaraka ya mtumishi wa ofisi katika kampuni ya Bima kwa kuwa Wakala siyo mfanyakazi wa kampuni hiyo na wala siyo sehemu ya mkataba wa Bima ambao ni kati ya mteja na kampuni ya Bima. Wakala wa Bima ni mwakilishi wa kampuni ya Bima na kazi yake kubwa ni kutafuta wateja kwa niaba ya kampuni husika. Hivyo jukumu lake linaishia katika kutafuta wateja wa kampuni husika na hulipwa kamisheni kwa kazi hiyo.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Shirika la Bima haliwatendei haki wale wateja wanaokuwa wamepata haki zao na wale ambao wamefariki dunia. Kwa kuwa kuna mtumishi mmoja aliyekufa mwaka 1990 mke wake alishughulikia kutafuta haki hiyo lakini mpaka leo hajaipata na sasa hivi ana miaka kumi bado hajalipwa na mtumishi huyo anaitwa Marehemu Bulakwa Aman Chuma, ambaye alikuwa ni Mwalimu. Je, Serikali inasemaje? Je serikali inataka kuwazulumu waliokufa au vipi? (*Kicheko*)

**SPIKA:** Lakini Mheshimiwa huyu hajadhulumiwa bado hai. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nisikitike sana ikiwa ni kweli kuna mwananchi huyo ambaye kwa maneno ya Mheshimiwa Mbunge amenyanyaswa. Lakini nifafanue kwamba Serikali si Kampuni ya Bima na haiwezekani kuwa Serikali ndiyo imemnyanyasa. Kama ni kweli kanyanyaswa basi lawama tuzipeleke kwenye kampuni yenyewe ya Bima husika na kama atahitaji msaada wa Serikali sisi Wizara ya Fedha tuko tayari kusaidiana na Mheshimiwa Mbunge na kumtambua huyo mwananchi na kuona jinsi ambavyo tunaweza kumsaidia kupata haki zake za Bima ingawaje naomba nitoe tahadhari kwamba hilo si kwa kweli jukumu la fedha lakini tupo tayari kufanya hivyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda umetubana kidogo tuhamie Wizara ya Afya, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Viti maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

Na. 125

**Mafuta ya Transfoma**

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA (K.n.y. MHE. MGENI JADI KADIKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, mafuta ya Transfoma hutumiwa na baadhi ya watu kwa kupikia chips na vyakula vingine:-

Je, mafuta hayo yamefanyiwa uchunguzi kuwa hayaleti madhara kwa afya za binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kutoa maelezo mafupi kuhusu mafuta ya *transfoma* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matumizi halali ya mafuta ya *transfoma* ni kupoozea *transfoma* za umeme na sehemu zake zote ambazo hupitisha umeme mkubwa ikiwa ni pamoja na kuzuia kutu na kukatika kwa nyaya za umeme. Baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa kimaabara uliofanyika na Wizara yangu kwenye sampuli za mafuta ya *transfoma* ulikuwa ni kwa lengo la kuangalia ubora wake pamoja na kuthibitisha uhalisia wa yale yaliyohisiwa kuwa ni ya wizi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina taarifa za ziada kuhusu matumizi ya mafuta hayo ikiwa ni pamoja na kupikia *chips*. Hata hivyo, iwapo mafuta ya *transfoma* yatatumika kwa matumizi ya kupikia *chips* na vyakula vingine yanaweza kuleta madhara yafuatayo kwa watumiaji:-

- Maumivu ya tumbo;
- Kuharibika kwa maini;
- Kichefuchefu;
- Kuharisha;
- Uharibifu wa mapafu kutokana na kuvuta hewa iliyochanganyika na mafuta hayo;
- Ugonjwa wa ngozi; na
- Kansa.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa maelezo haya, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuwatahadharisha wananchi kuwa ni makosa kutumia mafuta ya *transfoma* kwa kupikia *chips* na vyakula vingine.

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa msingi wa kupatikana mafuta haya ni kufikiwa kwa zile *transfoma* zenyewe na wale wanaokwenda kuiba mafuta; na kwa kuwa hata nyumba za kawaida za watu wanaweza kuziwekea umeme ili majambazi wasiweze kuzifikia hivi Serikali inaonaje zile *transifoma* wakaziwekea himaya maalum ili wale majambazi na wezi wasiweze kuzifikia na kuchukua mafuta haya na matokeo yanaleta madhara makubwa kwa watu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba mafuta ya *transfoma* yapo katika maeneo wanaoishi wananchi. Tunachukua wazo lake na tutashirikiana na Wizara husika ili kuweza kuona ni jinsi gani tutashughulikia usalama zaidi ili wananchi wasiweze kuwa na uwezo wa kuyapata haya mafuta ya *transifoma* wasiyatumie kwa matumizi ya binadamu.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mafuta haya pia hutumika kama kipodozi. Je, Mheshimiwa Waziri anatuambiaje yana athari yoyote na kama yanaathari Serikali inasemaje kuhusu matumizi hayo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi nimesema katika matatizo ambayo yanatokana na utumiaji wa mafuta haya ya *transfoma* ni pamoja na kuharibu ngozi. Kama mafuta haya yatatumika kama kipodozi sina shaka kwamba mtu huyo ataathirika. Kwa maana hiyo kama nilivyosema tunashauri wananchi waache kutumia mafuta hayo kwani wataharibu ngozi zao za usoni hasa wale akina mama lakini vile vile watahatarisha maisha yao. Kwa hiyo natoa wito tuwaambie wananchi watusikie kwamba mafuta hayo yana hatari kwa matumizi ya ngozi zao.

Na. 126

**Majaribio ya Dawa ya UKIMWI kwa Watanzania**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, gazeti la nje la Washngton Post limetoa taarifa kuwa, Watanzania wapatao 64 wamefanyiwa majarbio ya dawa ya UKIMWI iitwayo *Virodene PO 58* iliyotengenezwa huko Afrika Kusini ambayo wenyewe wameipiga marufuku nchini kwao:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo na ni chombo gani cha sheria kilitoa kibali cha majaribio ya aina hiyo kufanyiwa Watanzania?

(b) Kwa kuwa taarifa hiyo ilisema kuwa majaribio yalifanyika pia kwenye hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Lugalo, na kwenye zahanati binafsi iliyokuwa inamilikiwa na *IGP* Mstaafu. Je, Serikali inasema nini juu ya hilo?

(c) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa ujumla kuhusiana na jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida vyombo vya Serikali vinavyohusiana na utoaji wa vibali vya utafiti kama huo ni Taasisi ya Utafiti wa magonjwa ya Binadamu (*NIMR*), Mamlaka ya chakula na Dawa (*TFDA*) na *COSTECH*. Hata hivyo, hakuna hata moja ya taasisi nilizozitaja iliyowahi kutoa kibali kwa ajili ya utafiti huo. Kumbukumbu zinaonyesha ya kuwa ombi la kibali cha kufanya utafiti liliwasilishwa *NIMR* Julai, 2000. Hata hivyo, baada ya kufanya tathmini ya utafiti huo *NIMR* ililikataa ombi hilo kwa kuwa andiko kuhusu utafiti wa dawa hiyo *(Research Proposal)* lilikuwa na mapungufu makubwa ya ki-sayansi na ki-maadili. Kwa maelezo hayo ni dhahiri kuwa majaribio ya *Virodene Po 58* kwa Watanzania yalifanyika kinyume na taratibu za utafiti.

Mheshimiwa Spika, hata baada ya kukataliwa kwa ombi la kufanya utafiti wanasayansi hao waliingiza dawa bila kibali cha Serikali na kuanza kufanya utafiti Jeshini Lugalo na wakati huo huo kuziuza dawa hizi kiholela. Baada ya kutambua hali hiyo, mwezi Agosti 2001 Wizara yangu ilitoa agizo la kusimamisha utafiti huo pamoja na kuwafukuza watafiti wahalifu, kuzuia uingizwaji wa dawa hizo ikiwa ni pamoja na kuzirejesha zilikotoka.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu inajitahidi kuongeza uwezo wa Mamlaka ya chakula na Dawa na Taasisi ya Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) kuchunguza tafiti mbalimbali zinazofanywa nchini kuhusiana na dawa na magonjwa ili kuhakikisha kuwa tafiti zote zinafanywa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa suala hili linahusu maisha ya binadamu, na kwa kuwa Watanzania waliofanyiwa majaribio ni Watanzania 64 na kuna Watanzania wengine waliouziwa dawa hizi kiholela; na kwa kuwa taarifa zilizoko zinasema kwamba ni kweli Wizara ilichukua hatua iliyosemekana nataka kujua wale Watanzania walioshiriki kuingiza dawa hizi na kuendelea kufanya utafiti na kufanya maisha ya binadamu kuwa *gin picks* wamechukuliwa hatua gani?

Swali la pili, kwa kuwa taarifa zilizoko na utafiti uliofanywa ambao ninataarifa yake hapa unatamka kwamba viongozi wa jeshi ambao ndiyo waliofanya utafiti huu na ndiyo waoliingiza dawa hii nchini walisema wazi kwamba Wizara ya Afya na kwa maana hiyo *NIMR* haiuhusiki na kutoa vibali wakaendelea kufanya majaribio kwa wananchi kupitia hospitali ya Lugalo pamoja na zahanati ya Mheshimiwa aliyekuwa *IGP* Mstaafu. Serikali inatoa kauli gani na inachukua hatua gani ili jambo hili lifanyiwe utafiti wa kina.? Je, itafanya utafiti huu na kuleta taarifa kamili ndani ya Bunge hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ni kwamba utafiti huu wale walioingiza na kufanya utafiti walifanya

kinyume cha sheria kwa maana hiyo hatua zitakazochukuliwa kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba dawa zile zilirudishwa. Lakini vilevile Wizara ilikaa na jeshi na kuhakikisha kwamba hizi dawa hazitarudishwa tena na hawataendelea. Kwa hiyo, hatua itakayochukuliwa hapa ni kwamba kwa vile wananchi walioguswa ni Watanzania sasa kama itaonekana wanahitaji kufidiwa basi itabidi ifuate mkondo wa kisheria ili waweze kupata fidia yao. Lakini kama sheria inavyoelekeza, kwa sababu tumesema ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, taarifa kwamba viongozi wa jeshi wanasema kwamba hawakuhusika ni kweli kwamba wao walikaa na Serikali na Katibu Mkuu Wizara ya Afya, alikaa na Katibu Mkuu wa kule Lugalo na tukaambiwa kwamba wao utafiti wao wa jeshi hauingiliani. Lakini kisheria *NIMR* inaratibu tafiti zote za afya mahali popote nchini na bila kujali kwamba ipo wapi. Kwa maana hiyo tunavyokwenda Lugalo kufanya utafiti wetu tunaenda kutafiti dawa na hatutafiti vifaa vya jeshi. Kwa maana hiyo tunaomba tupate ushirikiano na Wizara yangu kupitia *NIMR* itakuwa inaendelea kufanya utafiti katika dawa hizi ikiwa ni kule Jeshini ili kuweza kuhakikisha kwamba dawa zote ambazo zinaingizwa kule jeshini na vitu vyote vinafanyika vya kitafiti vinavyohusiana na afya vinafanywa kwa uangalizi wa Wizara kupitia *NIMR*. Kwa hiyo, wale wote ambao wanasema hawakuhusika lakini ni kweli kulikuwepo na mazungumzo na tunaendelea kuwaambia kwamba yoyote anayetaka kufanya utafiti wowote unaohusiana na masuala ya afya ya binadamu, basi ni lazima Wizara kupitia *NIMR* ihusishwe na sisi tutakuwa ni watu wa mwisho kabisa kutoa uamuzi kwamba utafiti huo una manufaa au hauna manufaa kwa wananchi. (*Makofi*)

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dawa hizi ziliingia nchini na kwa kuwa tafiti ziliendelea katika hospitali ya Lugalo ni dhahiri kwamba kitengo cha *TFDA* na *NIMR* kilienda kinyume na sheria. Je, Wizara inatuambia nini kuhusu kuwajibisha vitengo hivi viwili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Wizara kupitia *TFDA* na *NIMR* waliingilia kati kwa sababu walipokea andiko kuhusiana na utafiti huu inaonyesha kwamba lile andiko halikuwa linakidhi mahitaji. T*FDA* ilipoo na zile dawa zimeingia ilichukua hatua ya kuzikamata, kuwafukuza na kuzirudisha kule zilikotoka. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba sisi kama Wizara si kwamba tulizembea, tumefanya kazi yetu kama tulivyotakiwa na ndiyo maana nikasema kwamba *TFDA* na *NIMR* chini ya Wizara ya Afya inaendelea kuhakikisha kwamba tafiti zote zinashughulikiwa. Sisi kama *TFDA* hatukufunya kosa tumefanya wajibu wetu na kuwasimamisha wale walihusika na tutaendelea kuwafuatilia ili suala hili lisiendelee tena.

Na. 127

**Umuhimu wa Kufundisha masomo ya Sayansi**

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Kwa kuwa jamii ya Tanzania sasa hivi inatambua umuhimu wa kusoma masomo ya Sayansi; na kwa kuwa ziko shule nyingi ambazo hazina maabara na hivyo wanafunzi hawajifunzi sayansi kwa vitendo:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kila shule inafundisha masomo ya Sayansi kama inavyostahili?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba shule nyingi zinafundisha masomo ya Sayansi kwa nadharia bila wanafunzi kujifunza masomo ya Sayansi kwa vitendo. Serikali kila mwaka imekuwa ikiongeza maabara kadri ya upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2007/2008 Serikali ilitenga fedha za ujenzi wa maabara 84 kwa nchi nzima. Ili masomo ya Sayansi yaweze kufundishwa kwa vitendo ni jukumu letu sote kushirikiana kuhakikisha kuwa ujenzi wa maabara unapewa kipaumbele katika ujenzi wa shule.

Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya ujenzi wa maabara na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kadri fedha zitakavyopatikana ili hatimaye wanafunzi katika shule za sekondari wajifunze sayansi kama inavyostahili. Kwa sasa shule zinaweza kununua vivunge vya Sayansi ambavyo vinaweza kusaidia kwa sehemu katika kujifunza Sayansi kwa vitendo.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza sasa hivi kwa siku nyingi zaidi ya miaka 15 hivi shule zaidi ya nusu za sekondari wanafundisha Sayansi kwa nadharia tu. Je, Naibu Waziri anaweza kunihakikishia kwamba hii haichangii kuwapata wataalam wabovu, vihiyo kwa mfano madaktari wabovu, mainjinia wabovu kwa kukosa msingi wa Sayansi?

Swali la pili, kwa kuwa somo la Sayansi inabidi lifundishwe kwa nadharia na kwa vitendo na ufundishaji wa Sayansi kwa nadharia ni kukiuka kanuni bora za ufundishaji wa masomo ya Sayansi. Kwa nini sasa Wizara yenyewe ya elimu inaruhusu wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne kufanya mtihani wa nadharia tu ambao unaitwa *alternative to practical?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikiri kwamba ni kweli ujenzi wa shule hizi zimekuwa ni nyingi na upatikanaji wa maabara umekuwa ni tatizo kidogo. Hata hivyo kama nilivyojibu kwenye swali la msingi,

Serikali inajitahidi kila mwaka kuongeza idadi ya maabara kama ulivyoona mwaka jana kwa maana ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 tulitoa maabara 42 na 2007/2008 maabara 84 Mwenyezi Mungu akitujalia katika Bajeti hii tunaweza tukazio ngeza maradufu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba wanafunzi wengi zaidi wangependa kujifundisha kwa nadharia. Hata hivyo tunazo shule nyingi ambazo zina maabara na huko ndiko tunakoendelea kupata wataalam waliobobea na kwamba wale ambao wanafanya *alternative* ni kwa zile shule chache ambazo kwa kweli zinakuwa na vifaa na mambo mengine hakuna.

Hata hivyo Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Serikali tutajipanga vyema na katika Bajeti ya mwaka huu 2007/2008 tumeweka kipaumbele katika vifaa vya kufundishia na kujifunzia zikiwemo maabara na kemikali mbalimbali katika maabara zetu. *(Makofi)*

Na. 128

**Kukabili Tatizo la Upungufu wa Walimu**

**MHE. ANIA SAIDI CHAUREMBO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeamua kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari nchini (MMES); na kwa kuwa, kabla ya mpango huo wa MMES kulikuwa na mkakati wa kuwaandaa walimu kupitia kozi za muda mfupi na muda mrefu ili kuweza kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hilo.

(a) Je ni Wilaya ngapi ambazo zimefanikiwa kupata walimu wa kutosha na ni wilaya gani zina upungufu zaidi kwa majina?
(b) Je, ni walimu wangapi wastaafu ambao wamejitokeza hadi sasa kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Saidi Chaurembo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya zote zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu. Hivyo hakuna Wilaya yoyote ambayo imefanikiwa kupata walimu wa kutosha mpaka sasa. Upungufu huo unatokana na Wilaya zote kuendelea kufungua shule katika kila Kata ili ziweze kudahili wanafunzi wote waliomaliza Mtihani wa Elimu ya Msingi.

Hata hivyo upungufu mkubwa wa walimu unajitokeza zaidi katika Wilaya za Mikoa ya pembezone kutokana na hali duni ya miundombinu na mazingira ya kufanyia

kazi. Mikoa na Wilaya hizo ni Shinyanga, Singida, Tabora, Lindi, Mtwara Kigoma, Rukwa Pwani (Mafia na Rufiji) Manyara (Kiteto na Simanjiro), Arusha (Ngorongoro), Morogoro (Ulanga), Ruvuma, Kagera (Biharamulo) Mara (Musoma Vijijini, Tarime na Serengeti), Mwanza, Tanga (Handeni, Kilindi na Lushoto) na Mkoa wa Dodoma Wilaya za Kongwa, Kondoa na Bahi). Wizara kwa sasa inaandaa mkakati wa kupata Walimu watakaokidhi mahitaji ya shule za Sekondari katika Mikoa na Wilaya zote.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu ilipata kibali cha kuajiri walimu 250 ili kukabiliana na tatizo la upungufu mkubwa wa walimu katika Shule za Sekondari.

Nafasi hizo zote 250 zilijazwa na walimu hao wapo kazini. Aidha, katika mwaka huo Wizara ilipata kibali cha kuajiri jumla ya walimu 14,490 ambapo zoezi la ajira hizo linaendelea. Ifikapo Desemba 2008 Wizara inatarajia kupata walimu 11,481 wakiwemo 9,231 wa Stashahada na 2,250 wa Shahada.

Kutokana na tatizo la upatikanaji wa walimu Wizara ina mpango wa kuomba tena kibali cha kuajiri walimu wastaafu 500 katika kipindi cha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa walimu wastaafu watapatikana ili kupunguza tatizo la upungufu wa walimu katika Shule za Sekondari hapa nchini.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Waziri, Waziri amekiri kwamba bado kuna tatizo kubwa la upungufu wa walimu nchini:-

(a) Kwa kuwa Serikali inaendelea kutatua tatizo la upungufu wa walimu hasa wa sekondari; je, walimu ambao wanafundishwa kwa muda mfupi, Serikali italihakikishia vipi Taifa kwamba wanastahili kile kiwango ambacho kinatakiwa watakuwa wamekikamilisha?

(b) Kwa kuwa Serikali inaendelea kuajiri walimu wastaafu; na kwa kuwa walimu wastaafu kwa muda mrefu walikuwa katika maeneo yao; je, walimu hao watamudu vipi mitaala ya elimu ambayo imerekebishwa hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, walimu ambao walipata mafunzo ya muda mfupi wanaendelea kupatiwa mafunzo wakiwa kazini na wengi wao wanaendelea kusoma katika Chuo Kikuu Huria na walio wengi wanagharamiwa na Serikali. Ni matumaini yetu kwamba walimu hawa kwa kuendelea kupata mafunzo wakiwa kazini watakuwa walimu bora na kwa kweli wanatoa msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, pili, walimu wastaafu waliochukuliwa ni wale ambao wangali na afya bora na timamu; ni wale ambao wana nguvu na wenye uwezo. Walimu hawa wanachukuliwa mwisho waliostaafu mwaka 2004 kama afya zao ni nzuri. Lakini wengi wamechukuliwa waliostaafu mwaka 2005 na kuja mbele.

*(Hapa kipaza sauti kilitoa kelele)*

**SPIKA:** Nadhani kuna tatizo kwenye hiyo *mic*. Labda utumie ya Mheshimiwa Masoud. Mheshimiwa Masoud washa…!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kujenga shule nyingi kwa mpango wa MMES na mpango wa MMEM; na kwa kuwa shule hizi bado zinakabiliwa na upungufu mwingi ukiwemo walimu, nyumba za walimu, maabara na mengine mengi; na kwa kuwa Serikali ina mkakati wa kuanza mpango wa kujenga zahanati; je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kuahirisha mpango wa kujenga zahanati na badala yake kuboresha shule hizi nyingi ambazo zinapungukiwa na mambo mengi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kiongozi wetu wa kwanza wa nchi yetu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alituambia kwamba kupanga ni kuchagua. Tulikwisha chagua na kuweka vipaumbele.

Katika Kata zetu nyingi ujenzi wa shule unakwenda vizuri sambamba na wale ambao wamekwishaanza kutekeleza malengo ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na wenyewe unakwenda vizuri. Tusifike mahali tukaahirisha mipango yetu kwa sababu ya kuogopa. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba watanzania wote kufanya kazi kwa bidii ili tujiletee maendeleo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda wa maswali sasa umepita, tumebakiza swali moja na nilichukua muda kidogo kutoa matangazo pale awali, kwa hiyo, tumalizie basi swali la Wizara ya Miundombinu linaulizwa na Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo wa Tandahimba.

Na. 129

**Ujenzi wa Ofisi ya Posta – Tandahimba**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Tandahimba ambao Makao Makuu ya Wilaya ya Tandahimba hayana jengo rasmi kwa ajili ya huduma za Posta; na kwa kuwa hivi sasa huduma hiyo hutolewa kwenye kontena, hali inayofanya shughuli za posta kuwa kama soko la mitaani:-

(a) Je, Serikali inawaahidi wananchi hao kuwa ni lini Shirika la Posta litajenga ofisi yake ya kudumu Wilayani Tandahimba?

(b) Je, ni lini *TTCL* watatoa huduma za mawasiliano ya *Fax*, *EMS* n.k. wilayani Tandahimba?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba mji wa Tandahimba ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Tandahimba hauna jengo rasmi kwa ajili ya huduma za Posta na badala yake kontena hutumika kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, hali kama hii ya kukosekana majengo rasmi ya posta ipo pia katika Wilaya nyingine nchini hasa mpya, kutokana na hali mbaya ya kifedha inayolikabili Shirika la Posta Tanzania. Hata hivyo, baada ya Serikali kufanya maamuzi yenye lengo la kuliweka Shirika la Posta Tanzania katika hali nzuri zaidi kifedha, Shirika hilo litaanza kutekeleza mikakati yake ya kibiashara ikiwa ni pamoja na kujenga majengo yake katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania limekwishapata nyumba ya kukodi katika mji wa Tandahimba ambayo itafanyiwa marekebisho na kutumika kwa ajili ya huduma za Posta ambapo baada ya marekebisho hayo kufanyika, Posta ya Tandahimba itapandishwa daraja na kuwa Posta kamili.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya *TTCL* haitoi huduma za *money Fax*, na *EMS,* huduma hizo hutolewa na Shirika la Posta Tanzania. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa pindi Posta ya Tandahimba itakapopandishwa daraja na kuwa Posta kamili huduma zote za Posta ikiwa ni pamoja na huduma za *money Fax* na *EMS* zitatolewa na Posta hiyo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri. Hata hivyo, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wafanyakazi na wakulima wa Tandahimba husafiri safari ndefu kwenda Newala kwa ajili ya huduma ya *Fax, E-mail* na shughuli nyingine za Posta ambazo huwaletea usumbufu kwa wananchi hao na kuwapunguza tija ya kazi; je, Serikali sasa inaweza kuliona jambo hili kama la dharura na kwa hiyo, wananchi waahidiwe shughuli hii ya Posta kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba wafanyakazi na wakulima wanasafiri kwenda Newala kwa ajili ya kupata huduma hizi. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kujipanga vema katika Wizara mpya ambayo imeundwa hivi

sasa, nina hakika suala hili tutalichukua kwa uzito wake na suala la watu kusafiri kwenda Newala, huduma hizi za Posta na *Money Fax*, sasa zitapatikana hapo hapo. Tutahakikisha kwamba Posta hiyo iwe Posta kamili na iweze kutoa huduma zinazotakiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatimaye sasa maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Matangazo, nitaanza na wageni wetu: Tunao wageni mashuhuri pale kwenye *Speaker's Gallery* ambao ni wawakilishi wa *Development Partners* wetu - nchi ambazo tunashirikiana vizuri katika maendeleo.

Nitaanza kumtambulisha Bwana John Bradshaw - *Political and Press Officer, British High Commission.* Yule pale, asante! Hester Somsen – *First Secretary Political and Cultural Affairs, Embassy of the Kingdom of the Netherlands. Theo Kaspers - Counsellor, European Commission* na Joseph Kithama, *Policy Officer – Embassy of the Kingdom of the Netherlands. We are happy to welcome you to the Chamber, some of you once again. It is always a pleasure to have Development Partners' representatives here in the Chamber because one of our major responsibilities is to discuss development of our people. Thank you very much for being here.*

Wageni wa Mheshimiwa Getrude Mongella ni kikundi cha akina mama cha Faraja *Women Development Trust Group* cha Dodoma kikiongozwa na Mwenyekiti wake Bibi Mary Bulegi. Mlezi wa kikundi ni yeye Mheshimiwa Getrude Mongella. Asante sana, karibuni sana. Tunawatakia mema katika kazi zenu. Kuna wageni wa Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya ambao ni wanafunzi wenzake wa kozi ya *MBA – Executive Programme* ya Dodoma *Centre*. Wao ni Bwana Mwilapwa, sijui wako wapi…? Naomba wasimame. Mwilapwa, Tibuza, Bwana Haule na Dr. Lazaro Swai ambaye ni *Course Instructor*. Asante sana. Tunawatakia mema katika masomo, nchi inawahitaji *MBA* wengi sana kwa sababu ya masuala ya biashara na uwekezaji.

Nina heshima kuwatambulisha pia wageni wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa John Magufuli. Hawa wanatoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Magese Kachwele. Wamesimama wote! Mheshimiwa John Magezi ni Makamu wa Mwenyekiti, Madiwani 13, Afisa Mipango, Bwana Deus Luziga na Afisa Ardhi na Mazingira, Ndugu Fredrick Nyoka. Karibuni sana Waheshimiwa! Tunaipongeza sana Wilaya mpya ya Chato na mna Wabunge wazuri tu, kwa hiyo, maendeleo yako mbele yenu, kazi kwenu! *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeona wanafunzi pale, naomba wanafunzi msimame na walimu wenu upande wa kushoto hapo. Lakini sikutaarifiwa ni shule ipi, lakini wote mnakaribishwa. Ni vizuri vijana wetu wakaja kuona wao wenyewe jinsi demokrasia inavyoendeshwa katika Bunge lao. Asante sana, karibuni sana!

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara wakutane leo saa 8.00 mchana, Ukumbi Namba 231, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Shah, Mwenyekiti wa Chama cha *Scout* Bunge, anaomba wanachama wote wa chama cha *Scout* kuwa leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 227. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao ni wanachama (*scouts)*, mnaombwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Shah, mkutane saa tano ukumbi namba 227, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, Shirika la *TAYOA (Tanzania Youth Alliance)* limewapatia Wabunge wote kanda ya nyimbo zinazotoa elimu juu ya janga la UKIMWI. Hivyo, Waheshimiwa mchukue fursa hii kujipatia kanda hizo ambazo zinapatikana katika lango kuu la ukumbi wa Bunge. Mtawakuta vijana pale mnapotoka, watawakabidhini kanda hizo, ni nzuri na zinasaidia sana kuhamasisha vita yetu dhidi ya janga hili la UKIMWI.

Pili, Benki ya *National Microfinance Bank*, *NMB* imewapatia Waheshimiwa Wabunge wote *Tyre covers* – Kiswahili hapa inakuwa tabu, lakini ni plastiki za kufunika matairi hasa kwenye magari ambayo yana *spare tyre*, inakaa nyuma. *Tyre covers* hizo zinapatikana kwenye kituo cha malipo cha *NMB* hapo hapo Bungeni pale kwenye Jengo la Utawala, *ground floor*, mnaweza mkapata *tyre covers*. Nimeombwa na Katibu wa Kamati ya Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kuwataarifu kwamba leo saa 7.00 mara baada ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge mchana huu, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, mkutane pale katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Bunge imekwishawagawia ama zinagawiwa hivi sasa, fomu za nyinyi kupendekeza Kamati zipi mtapenda kuwa wanachama au wajumbe kuanzia Mkutano ujao. Kama mnavyofahamu, sasa tumefika nusu ya muda wetu na Kanuni zinahitaji kwamba ujumbe katika Kamati unabadilika kwa kiasi fulani. Kwa hiyo, fomu zinajieleza zenyewe, unaonyesha Kamati ambayo unaipa kipaumbele, ya pili, ya tatu na kadhalika.

Ofisi itajaribu kuzingatia kadri inavyowezekana, mapendekezo yenu. Lakini, si rahisi kwa sababu Kamati nyingine zinaweza kuwa na watu wachache na mkumbuke Kamati zimeongezeka pia, kwa hiyo, kuna umuhimu wa kubadili badili baadhi. Nimejiwekea mwongozo kwamba angalau hadi kufikia theluthi moja ya wajumbe wawepo katika Kamati wale wale waliokuwepo ili kujenga tunachoita *continuity*, hilo ndilo nimeweka msingi. Kwa hiyo, mathalani, Kamati iliyokuwa na Waheshimiwa Wabunge 21, tutahakikisha 7 ni wale wale waliokuwepo. Lakini wengine 14 itabidi tubadilishe waende katika Kamati nyingine. Mwisho wa matangazo, sasa nitamwita Katibu kwa shughuli inayofuta.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza Mchakazo wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura Ulioipa Ushindi “Richmond Development Company LLC” ya Houston, Texas - Marekani Mwaka 2006

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia katika mjadala wa kujadili Taarifa ya Kamati Teule kuhusu umeme wa dharura wa Richmond, napenda kusema yafuatayo:-

Kwa mujibu wa ratiba yetu na baada ya kushauriana na Serikali, ingependeza sana ikiwa tungemaliza shughuli zetu kesho saa 7.00. Ingependeza! Na hii inatokana tu kwamba tuna ugeni mzito wa kitaifa Dar es salaam ambao utawahusu kuanzia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wengi sana kwa sababu ya zile fedha za *Millenium Challenge Corporation.* Na hilo ni jambo kubwa, baadhi ya maswali yetu mengi hapa yaliyohusu huduma za maji, miundombinu na kadhalika yatajibiwa kutokana na kufanikisha fedha hizo za *MCC*.

Sasa tukiendelea hadi jioni, itakuwa vigumu sana na ni hatari pia kwa Mawaziri kuondoka usiku kwenda Dar es salaam ili kuwa tayari kuwapokea wageni. Lakini la pili, mjadala huu, na bahati njema nimepata karatasi nyingi tu za Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuondoa majina yao, na hii ni kuthibitisha hali halisi iliyo wazi kabisa kwamba Serikali hata haikusubiri mjadala, imechukua hatua za aina mbalimbali kuhusu suala hili. Lakini la tatu, nataka kuwakumbusha Kanuni inayokataza kujirudia rudia. Haisaidii tu kuunga mkono, kuunga mkono kwa namna ambayo unarudia rudia yale yale waliyosema wengine.

Sasa kwa sababau zote hizo tatu, mpangilio ambao mmegawiwa hauwezekani kabisa. Kwa hiyo, nimejaribu kutengeneza orodha mpya ambayo inazingatia uwakilishi wetu ndani ya Bunge kwa jinsia, kwa vyama vya siasa, kwa kanda za nchi yetu na kadhalika. Kwa hiyo, nitategemea kwamba hawa ambao watatangulia, wataweka mtiririko ambao utatusaidia ili nitoe nafasi ya kutosha baadae kwa mtoa hoja na wenzake waweze kuhitimisha hoja, ikiwezekana hiyo kesho asubuhi.

Kwa maelezo hayo, napenda sasa kuwatamka wafuatao:- Nitaanza na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, atakuwa msemaji wangu wa kwanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, halafu atakuja Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Grace Kiweru, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Charles Keenja na kwa uzoefu wetu huwa inawezekana wanane au tisa wakaongea kwa asubuhi. Basi tutamalizia na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, halafu nitatangaza mchana jinsi tutakavyoendelea baada ya saa 11.00. Asanteni sana kwa uvumilivu wenu. Sasa nitamwita Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ajiandae Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili nami nitoe mchango wangu kutokana na hoja ya Kamati Teule ambayo imefanya kazi nzuri, siyo ya maandishi, lakini ya vyambatisho mbalimbali ambavyo vimetusaidia sisi Wabunge kuweza kuelewa kina cha tatizo ambalo tunalo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote katika Taarifa hii nimekuta jambo ambalo limenishitua sana. Bunge lako Tukufu limepitisha sheria mbalimbali na miongoni mwa sheria hizo ni kuanzisha taasisi mbalimbali. Moja kati ya Taasisi ambazo tumezianzisha ni Taasisi ya Manunuzi. Taasisi hii imefanya kazi nzuri na imetoa miongozo mizuri na mingi kwa Taasisi zetu ili tuweze kufuata.

Kwa bahati mbaya inasikitisha sana kwamba Serikali ambayo ingetakiwa kuwa kioo chetu katika kutekeleza na kusimamia sheria za nchi, yenyewe ndiyo imekiuka sheria za nchi. Sasa nasema hii ni hatari kwa sababu tusipojengea utamaduni wa kuzithamini Taasisi zetu na sheria tunazozipitisha ndani ya Bunge hili, basi tutakuwa kwenye matatizo makubwa mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tendo hilo, *TANESCO* imeingia mikataba na makampuni matano, mojawapo ikiwa ni Richmond. Katika makampuni matano haya, ni kampuni moja tu ambayo imetumia sheria na kanuni za *Public Procurement* tuliyonayo sisi. Makapuni mengine yote yamekwenda kuchukua katika *archives* ya *World Bank* mikataba ambayo Tanzania imetutia hasara. Na ni mkataba huu mmoja tu wa *TANESCO* na *WARTSILA* ambao ndio *TANESCO* wamepata manufaa. Mikataba mingine yote ambayo tumechukua kama *mode* kutoka *World Bank*, ndiyo imeizamisha *TANESCO* mpaka kufikia kiwango tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Mkataba na Richmond, *TANESCO* inalipa dola milioni 54.8 kwa mwaka, mkataba mmoja tu na Richmond kwenye *capacity charges*. Kwenye *AGGREKO* wanalipa dola milioni 21.8, *AILSTROM* wanalipa dola milioni 27.4, *SONGAS* wanalipa milioni 99.6 na *IPTL* milioni 40.5. Jumla ni dola milioni 195.252 au shilingi bilioni 444.1 kwa mwaka na hatuna hasara yoyote tunayoipata au hasara kubwa tunayoipata kwa mkataba ambao tulitumia sheria ya *Procurement Act* ambayo tunayo katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema ni vema Serikali ikatueleza, ni sababau zipi za msingi zilizoacha sheria zetu sisi wenyewe za ndani, taasisi zetu za ndani, tukahemea sheria ambazo zinaikandamiza na kuiumiza nchi yetu. Hilo lilikuwa jambo la kwanza ningependa nilifahamu.

Mheshimiwa Spika, la pili katika hili ni kwamba, katika mikataba yote ukitazama hii na hasa huu wa Richmond, *TANESCO* siyo tu inalipia hizi *capacity charges*, lakini hata gharama nyingine za mafuta, gharama za kodi na kadhalika. Kila kitu *TANESCO* inalipa! Sasa tunajiuliza, huyu mkodishaji alikodisha kwa misingi gani? Watu wetu ambao wanasimamia sheria hawafahamu sheria za nchi? Hawafahamu sheria ya *Procurement* tuliyoipitisha ndani ya Bunge? Kwa hiyo, utakuta *TANESCO* imebebeshwa mizigo kiasi kwamba ni mahututi.

Mheshimiwa Spika, lakini moja ambalo lilinishitua zaidi wakati Serikali ilipoleta sheria juzi, ukiitizama sheria yenyewe na ukitizama mikataba hii, unaiona tayari *TANESCO* imewekewa kitanzi pembeni cha kuweza kumalizwa. Na hili ndilo jambo linalonishitua zaidi kwamba tunazaa watoto wetu badala ya kuwatunza, tunawawekea

mizengwe ya kuwamaliza. *TANESCO* ni mojawapo! Kama Bunge lako Tukufu halikuwa imara, likasimama kidete, likasema hii miswada kwanza ingoje mpaka tuangalie Richmond, basi leo *TANESCO* ambayo tayari iko *ICU* ingekuwa maiti. *TANESCO* ina mikataba na makampuni mengine ya miaka 20, makampuni mengine miaka 2.

Ni dhahiri kuwa sheria ile kama tungeweza kuipitisha, leo *TANESCO* ingekuwa tayari haipo tena kwa sababu mikataba inasema hata kama kuna sheria nyingine itatungwa kama sheria hiyo itaathiri mkataba na *TANESCO*, *TANESCO* ndiyo itakayolipa gharama. Kwa hiyo, *TANESCO* ingekuwa ni katika kulipa tu.

Waheshimiwa Wabunge kama kuna watu wamepata kusoma kitabu kimoja kinaitwa *"The Economic Hitman"*, watajua asili ya hii mikataba inayotengenezwa na *World Bank* na tunayoletewa sisi ina taathira gani ambayo nchi inaipata. Mikataba hii yote inatulazimisha nchi ibaki na madeni mpaka kiama, na ndiyo matokeo ya mikataba tuliyonayo katika *TANESCO* na makampuni haya matano tuliyonayo hivi sasa, Richmond ikiwa mojawapo. Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, limedai sana mikataba hapa ndani ya Bunge, lakini imekuwa ni kikwazo kikubwa. Hata mimi mwenyewe juzi hapa niliahidiwa kupewa mkataba wa *Alex Stuart* pamoja na ripoti zake, mpaka leo sijaipata. Naliomba Bunge lako Tukufu sasa tuazimie kabisa. Kama wenzetu wa Mongolia wanavyofanya, sasa hivi wamebadilisha utaratibu, hakuna mkataba wowote ambao utaathiri uchumi wa nchi ambao haukupitia Bungeni. Tunaomba sasa Bunge lako Tukufu, lazima liione mikataba hapa ama kwenye Kamati zetu au kwenye Bunge zima ili wananchi wa Tanzania waondokane na tataizo la kuporwa rasilimali zetu kama tunavyoporwa sasa. Kwa hiyo, naungana na Kamati kabisa katika pendekezo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiowa Spika, la tatu, ukiangalia mkataba huu na Richmond, utakuta *TANESCO* inalipa kila kitu, lakini baya zaidi, Richmond haikutimiza masharti yake. Kwa hiyo, uwezekano wa Serikali kuvunja mkataba na Richmond ulikuwepo. Na kwa maana hiyo vipo vifungu kama vinne katika mkataba huu vinawezesha kabisa Serikali kuishitaki Richmond. Tunaitaka Serikali iishitaki Richmond haraka sana iwezekanavyo ili watanzania waweze kupata rasilimali zao walizozipoteza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la nne, wako watu waliozembea kwa makusudi, maana inapokuwa chombo fulani kinaelekeza kwamba jama hapa mnapotea na bado mkashikilia, basi hayo ni makosa ya makusudi. Na hakuna katika sheria zetu zozote zile, ama unavunja sheria kwa makusudi au unavunja sheria kwa kutokujua kwamba huchukuliwi hatua. Tungependa kabisa watu wanaohusika wote wachukuliwe hatua mara moja. Mambo ya kubembelezana katika maslahi ya Taifa letu, hayo hayafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la sita ukiangalia mikataba hii lengo lake moja kubwa ni kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi zinawafaidia wananchi wenyewe lakini mikataba hii yote mitano ukiacha ule wa *WARTSILA* hauwasaidii Watanzania na ndiyo maana Tanzania imebakia mpaka leo tuna asilimia kumi tu ya maeneo yetu ndiyo yana umeme na asilimia moja tu katika kumi ndiyo maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika sera ya umeme au sera ya nishati tulikubaliana kabisa katika Bunge hili tukaarifiwa kwamba tutapata umeme vijijini. Ukichukua makampuni yote matano haya hakuna hata moja lililosaidia katika kutatua tatizo la umeme vijijini, ni dhahiri kwamba sera ambayo tumekubaliana tuitekeleze hatukuitekeleza. Je, Serikali inaeleza nini pale ambapo inaingia kwenye mikataba kinyume na sera ambazo tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, jambo la saba *RICHMOND* ilipokuja ilikuja kwa dharura na dharura kubwa ilikuwa ni tatizo la ukame, kwa hiyo, tulitegemea mkataba ulikuwa wa kulinganisha na matatizo yaliyokuwepo wakati huo. Lakini mkataba umekuwa wa miaka miwili badala ya mwaka mmoja, au tungetegemea Serikali kwa kuwa haina uhakika wa hali ya hewa, basi ingesema tungechukua mwaka mmoja na kama ikitokea lazima tuta-*renew* mkataba ule lakini halikutendeka hilo hata kidogo. Matokeo yake tutalipa dola hizi nilizozitaja milioni 54. Mara mbili, maana yake ile ilikuwa ni malipo ya mara moja. Sasa tunalipa mara mbili, mzigo huu anabebeshwa Mtanzania. Mimi nashangaa kama leo tutakwenda kuandamana kufanya nini? Kuandamana kwa kuishinikiza *TANESCO* kwamba iko mahututi sasa inazikwa? Kuandamana kwamba Watanzania wataendelea kulipa shilingi bilioni 244/- kila mwaka? Tutaandamana kwamba bado hatujapata umeme vijijini au tutaandamana kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, mimi nasema tuandamane baada ya Watanzania kupata manufaa na kufaidika na baada ya kuchukuliwa hatua maeneo mengine ambayo bado hatujayashughulia (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatujashughulikia *IPTL*, mkataba wa *SONGAS*, hapa tumezungumza kwa ujumla tu, ndiyo tupo kwenye *RICHMOND*, kuna mikataba ya *TWINS TOWER* huko hatujaishughulikia, tuna mikataba ya madini chungu nzima hatujaishughulikia. Nafikiri hatuna haja ya kufurahi sasa hivi, hiki tulichokifanya ni rasha rasha ya matatizo tuliyonayo, bado hatujaingia kwenye kiini cha matatizo, tuungane pamoja, tushirikiane pamoja tuhakikishe kabisa nchi yetu iishi bila ya kuwa na rushwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote zilizopendekezwa na Kamati yetu Teule, ahsante sana. ( *Makofi*).

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamed Rashid, namwita sasa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Mgana Msindai na atafuatiwa na Mheshimiwa John Shibuda.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu hoja hii. Jambo la kwanza ningependa kuipongeza Kamati Teule ya Dr. Mwakyembe kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, nimefurahia sana maelekezo uliyosema kwa sababu ukiangalia jambo hili utaona kwamba kwa namna moja au nyingine sehemu kubwa kabisa ya taarifa hii imeanza kutekelezwa na Serikali, kwa hiyo, mimi ningependa

kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujali kazi ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha yeye kuteua Waziri Mkuu na kuweka Baraza la Mawaziri na mimi ninayo habari ya kuaminika vilevile kwamba amekwishawakemea Mawaziri kwamba wachunge majukumu yao na wafanye kazi kwa uadilifu. Kwa hiyo, nina hakika Mawaziri wetu watafanya kazi kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya mimi nitaweka mapendekezo lakini nataka niseme mambo mawili makubwa, la kwanza, watu wengi nimekuwa nasikia wengine wakisema kwamba, unajua Baraza la Mawaziri ni vijana hawa. Mimi nataka kusema hawa Mawaziri siyo vijana ni watu wazima na nina hakika watawajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mzee Kawawa alipochaguliwa kuwa Waziri Mkuu alikuwa na miaka 30, na mimi nina hakika wengine hapa wapo zaidi ya miaka hiyo. Rafiki yangu Joseph Mungai alipoteuliwa kwa mara ya kwanza kuwa Waziri alikuwa na mika 29, mimi nilipoteuliwa kuwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara nilikuwa na miaka 31, kwa hiyo, nataka niseme kwa kweli hawa siyo vijana hawa ni Mawaziri watu wazima, wana elimu nzuri, watafanya kazi vizuri na tunawatakia heri.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme pamoja na kuwapongeza naomba wajue kwamba na wenyewe wamekalia moto, kwa hiyo, ni lazima wakazane vijana wakimbie wachemke ili waisaidie Serikali kujibu. Kwa sababu wananchi na Wabunge tunaona uchaguzi wa Rais ni nzuri sana tunampongeza.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda nilikuwa nafikiria mambo mawili: kwanza, Serikali na Mawaziri ni wapya na ninavyoona mimi kama nilivyosema mwanzo utekelezaji umekwishaanza juu ya taarifa hii. Kwa hiyo, napendekeza kwamba tuipe Serikali au baraza jipya la Mawaziri wasimamie utekelezaji wa taarifa iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, alivyokuwa anasema Mheshimiwa aliyenitangulia Mheshimiwa Mohamed Rashid, nakubaliana aliyoyasema yote yapo katika pendekezo namba 3 ya taarifa ya Kamati Teule. Sehemu ya mapendekezo inatoa rai kwa Serikali kwamba ipitie mikataba yote na makampuni ambayo wanataka mikataba ipitiwe yametajwa yote, kwa hiyo, nafikiri wazo hili si baya kwa maana kwamba Serikali watapitia mikataba kwa sababu ni sehemu ya utekelezaji wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuna pendekezo namba 11 ambalo vilevile ni la msingi na mimi nadhani linatoa maelekezo mzuri tu. Halafu vilevile kuna pendekezo namba 12 la taarifa hiyo, sitaki kutoa kitabu kwa sababu nina hakika wewe mwenyewe umesoma taarifa yote, nimeona tu nitaje vifungu hivyo. kwa hiyo, kwa muhtasari nakubali na nafikiri ingekuwa jambo zuri sasa tuiombe Serikali ipitie kwa makini mambo yote yaliyomo katika taarifa hii na kikao kijacho tunaweza tukapata ratiba ya Serikali yenyewe namna watakavyotekeleza mambo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwape muda Serikali waende wakakae wajipange. Hata hivyo, ningependa nikupongeze na niwapongeze pia Waheshimiwa Mawaziri kwa sababu nilidhani hata Bunge lisingefanyika leo kwa sababu nilikuwa nafikiri ni lazima tuahirishe tukimaliza muswada huu. Labda maswali na mengine yasingeweza kujibiwa lakini nataka niipongeze Serikali kwamba hawa walioingia sasa wameweza kujibu maswali vizuri sana, nawapongeza sana (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili baada ya Rais kuchukua hatua na mambo yote yamekwishaanza kutekelezeka, kwa kweli kwa upande wangu sioni kama nina mambo mengi sana ya kusema isipokuwa ni kuipongeza Serikali na kuomba kuwapa muda sasa wapangane waone namna watakavyotekeleza taarifa hii na kisha watakuja kutueleza wenyewe namna walivyojiandaa kuitekeleza taarifa hii. Maana hata wakijibu hawawezi kusema mia kwa mia kwa sababu mambo haya ni makubwa kwa nchi, mimi napendekeza wakae, wafikiri, waone halafu Bunge lijalo watatuletea kwamba wenzenu kutokana na mapendekezo haya utekelezaji utakuwa kwa njia hii na kwa misingi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba pia kuunga mkono taarifa na kuiomba Serikali ifuatilie haya.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, umenisaidia hata kuokoa muda, namwita sasa Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya bila woga. (*Makofi*)

Pili, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi zao. Kwa hili tumeungana pamoja kutotetea na kufichua maovu kwa niaba ya wananchi wetu wote. Kwa kweli nilikuwa nafikiria nijitoe lakini nikasema hapana ni lazima nichangie kwa kuisaidia Serikali. Wenzangu wamekwishasema, tumepata Waziri Mkuu mpya mchapa kazi na waliochaguliwa sisi tuna imani kubwa sana nao na kazi kubwa waliyokuwa nayo ni hii ya kuanzia na mambo ya *RICHMOND*, tunaomba na tunawataka sasa wadhihirishe kwa wananchi kwamba wanashughulikia mambo yote yanayoletwa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa inashughulikiwa kampuni ya *RICHMOND* na wenzetu waliopo kwenye Kamati wamekwenda mpaka kule Marekani, hii kampuni haipo, sasa hizi fedha huwa zinalipwa kwa nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mkataba ulikuwa uwe wa mwaka mmoja wakaongeza kinyemela, tunaomba sasa hivi haya malipo yasimamishwe kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Kampuni ambayo ilikuwa tuingie nayo mkataba haipo, hata hii ya pili waliyoingia wameingia kiujanja ujanja na mimi niseme kama wapo Watanzania walioiingiza hasara Serikali yetu, fedha za walipa kodi zikawa zinalipwa kwa watu wasiojulikana na wao wenyewe kujineemesha, wachukuliwe hatua, ikiwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani na kufilisiwa mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa hii vimetajwa vyombo vyetu, TAKUKURU imetajwa sana, chombo ambacho kwa kweli tulikiamini na tukapitisha sheria humu ndani lakini kwa hili wamejivunjia heshima yao. Na mimi nina imani kabisa Serikali itachukua hatua haraka iwezekanavyo. Nitawapa mfano, juu ya maajabu tuliyoyakuta juu ya TAKUKURU. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa wiki tatu zilizopita tulikwenda Wilayani Kondoa, mambo yanayofanyika kule ni ya aibu, ajabu kwa sababu hawa wamejitangazia kama kaserikali kao, hawafuati sheria tulizopitisha Bungeni, wanakwenda kuwakamata watu ovyo wa Halmashauri ya Wilaya. Sasa hivi Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imesimama, sasa sisi tunamwomba Waziri mpya wa Utawala Bora aliyechaguliwa aanzie Kondoa na siyo siri na vilevile Waziri wa Katiba na Sheria kuna mambo huko Mahakamani yanafanyika ya ajabu sana. Kwa hiyo, waanzie kule na tunamwomba Rais kama hatua alizozichukua kwa kweli aishughulikie TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, kuna Kamati ya Wataalamu ambayo inaundwa na Hazina, Benki Kuu sijui na wengine ni akina nani na Wizara inayohusika hapa ni Wizara ya Nishati na Madini walifanya mambo ya ajabu sana, walitumia ujuzi wao vibaya nao tunaomba washughulikiwe bila woga.

Mheshimiwa Spika, tuwapongeze sana watu wa manunuzi, wao walikataa na hawa wakawaambia lakini hawakujali kwa faida ya watu wachache, hivyo tunaomba wote waliohusika pafanyike marekebisho makubwa ili twende na wananchi wetu watuamini.

Mheshimiwa Spika, kuna wale watu ambao ni wafanyabiashara, matajiri na wengine wafanyakazi wanaacha shughuli zao, kazi yao ni kutafuta mwanya uko wapi ili waiibie Serikali, kama wapo tunaowafahamu wawe Serikalini, kwenye vyama vya siasa nao washughulikiwe ipasavyo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Taifa letu nchi inayosifika sana, tunachafuliwa na watu wachache. Sasa hivi tulikuwa na mategemeo makubwa ya kupata umeme vijijini lakini kumbe kuna ujanja unapitika chini na ujanja unaopitika ni kulihujumu shirika la umeme.

Mimi ningeomba Serikali ijipange upya, pamoja na sheria hizo inazoleta lakini ihakikishe shirika letu la umeme linaendelea na hata kama kuna madeni yaliyoingizwa ya ajabu ajabu, yale madeni Serikali itafute jinsi ya kuwalipa ili hawa watu waanze kazi zao.

Mheshimiwa Spika, tunauhitaji sana umeme vijijini, wananchi wa Iramba wamedanganywa kwa muda mrefu sana kupeleka umeme Nduguti. Umeme umepita Singa hakuna *transfoma*, nimeomba umeme kwenda Chuo cha Msingi hakuna, sasa tunaomba mjipange upya na hiyo sheria itakayokuja ya umeme muwe mmejiandaa, msije kirahisi rahisi, mikakati ya kuhakikisha kwamba tutapata umeme ili tuipitishe, hiyo kazi ianze mara moja.

Mheshimiwa Spika, nirudie kuiomba Serikali kwamba kusiwe na mchezo, Mawaziri wote waliochaguliwa wanaaminika na wanaweza na pia wamekwishasoma kwa

wenzao kwamba ukilegea kidogo mambo yataharibika, kwa kifupi niishie hapo lakini tuipe muda Serikali ikafanye mambo mazuri kwa niaba ya wananchi wetu.

Nakushukuru Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msindai, sasa ni zamu ya Mheshimiwa John Shibuda, hayupo….! Sijui Mheshimiwa Tatu Ntimizi yupo tayari, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Kiwelu.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Samahani Mheshimiwa Spika, mashine inakorofisha kidogo, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa machache niliyokuwa nayo katika mjadala huu wa *RICHMOND*.

Kwanza niishukuru Kamati kwa kazi ambayo wameifanya, hata kama ukifanya kazi nzuri namna gani si wote lazima wakusifie, unaweza ukapata misukosuko na wachache wakakulaumu lakini nashukuru kwamba wametoa ripoti ambayo imetoa mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nilikuwa naomba kwamba yaliyojitokeza katika Kamati hii basi si wanasiasa tu ndiyo wawajibike, mimi ningeshauri wote waliotajwa hata watumishi waliosaidia wanasiasa basi nao wawajibike, na kuwajibishwa kwao ni kustaafishwa kwa manufaa ya umma halafu taratibu zingine za sheria zifuate kama lazima lakini kuwawajibisha wanasiasa peke yao halafu wengine tukawaacha hatutawatendea haki wale ambao wamewajibishwa au wamewajibika wenyewe. Ni pesa nyingi sana ambazo zinazungumzwa, na pesa za walalahoi ambazo zingewasaidia katika huduma mbalimbali za jamii lakini huduma nyingine zimekwama kama zimeenda lakini hazina ufanisi kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti wangu mdogo nilioufanya TANESCO kila mwezi wanakusanya shilingi bilioni 30 na wakishakusanya bilioni 21 zote zinalipwa haya makampuni hewa. Anayeongoza kupewa ni *IPTL*, anafuata *RICHMOND*, *SONGAS AGGREKO*, *AGGREKO* yeye ndiyo kalala kabisa, yeye ni *sleeping giant.* Mwanza kule hakuna kinachofanyika, lakini kila mwezi lazima hizi bilioni zipelekwe, sasa kama wamefanya kazi wana haki ya kulipwa lakini ni kazi ipi ambayo wametufanyia?

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye utafiti wa *TANESCO* kila kinachotafutwa na makampuni lazima kitoke *TANESCO*, kifaa kimeharibika *TANESCO* anunue, hakuna nyaya mahali fulani *TANESCO* wapeleke ina maana msalaba anaobebeshwa *TANESCO* siyo wake, matokeo yake tunamlaumu *TANESCO.* Sasa hili Shirika tutaliendeshaje kama makupe wengi namna hiyo, anashindwa hata namna ya kujikuna huyu *TANESCO*, kupe wanamzidi ambao hawapati chochote, wanaishi kama ombaomba *TANESCO*, wanalazimishwa kupandisha bei, kwa sababu fedha hizi ni lazima zitoke ziende kwenye haya makampuni, hivi kuwepo makampuni haya kunasaidia nini?

*SONGAS* ni yetu, wao wamesaidia kuvumbua, sasa jamani tuwe wakweli ndugu zangu Serikali tunaipenda na Watendaji tunawapenda lakini wawe wawazi, mahali penye

uchungu wawe tayari kumeza shubiri hiyo. Lakini kukubali kuwa tunalipa haya mashirika mimi ningeomba sasa hivi tufanye hadidu za rejea, hiyo mikataba ambayo tulikuwa hatuioni wenzangu wamezungumza tuitazame, mkataba wowote ule una haki ya kushitaki na kushitakiwa, tunachoogopa Serikali kushitakiwa ni kitu gani? Kwa sababu huwezi kusaini mkataba kama masharti ya kushitaki na kushitakiwa hujayakubali kisheria.

Mheshimiwa Spika, ikiwa *City Water* tumevunja sasa inakuwaje haya mengine tusivunje, ndiyo maana tunapata sababu ya kuzungumza nani kahusika, labda mkubwa fulani kahusika kwa sababu ya usiri, lakini nilidhani *City Water*, pengine kulikuwa hakuna anayehusika ndiyo maana tukavunja tukapelekwa Mahakamani na kesi zikaendelea kwa utaratibu wa sheria, sasa huyu je, tunamwogopea nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli haya yamenikera, hata *rural electrification* haianzi kama tulivyokuwa tumedhamiria. Jimbo langu la Igalula linahitaji umeme lakini hakuna fedha, na ni kilomita 47 tu kutoka Tabora ambako kuna umeme wa uhakika. Lakini kama *rural electrification* ingeweza kufanyika Igalula leo ingekuwa naamka kwenye umeme badala ya kutumia majenereta badala ya kutumia *solar,* na ni Makao Makuu ya Jimbo. Itafika lini? Reli iko pale, umeme ungefika huduma za reli zingekuwa hazina tatizo matatizo, barabara ya Itigi ndiyo hiyo inapita katika Jimbo hilo, umeme kama ungekuwepo nina hakika kabisa hali ya uchumi katika Jimbo langu la uchaguzi isingekuwa na matatizo, sasa yote haya yanatokana na *mis appropriation of funds.*

Mheshimiwa Spika, naomba sana watazame mikataba tena upya hata kama kabla haijaletwa Bungeni, wenyewe wafanye hizi kazi haya makampuni faida yake ni nini wamekaa kama dudumizi wanakula taratibu kama moto wa kifuu kula hela zetu za wananchi. Naomba sana chambueni wakati wa Bunge la mwezi wa Nne Wabunge tupate taarifa kwamba kuna haya yamefanyika kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana kuleta mikataba hii, ni kweli tunaambiwa kwamba si rahisi Serikali ikafanya kazi hiyo halafu ikaletwa katika Bunge tena kabla ufanisi haujaonekana, lakini kutokana na haya yanayojitokeza nawaomba sana mkubali jambo la kuleta mikataba huku Bungeni ili huu uwazi uonekane. Hizi ni zama za ukweli na uwazi, tusiwe na matatizo ya kuletewa hisia zingine tena, kwamba jamani pengine mkataba una maslahi, mnachaguliwa vizuri, mnafurahiwa na tunawapongeza, huu ni mchezo wa kijiti wa kupokezana, lakini urasimu huu ndiyo unaotufikisha mahali pagumu.

Mimi nimeona nizungumze haya machache lakini hizi kampuni hata wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanalazimika kukusanya pesa kwa muda wote kupata shilingi bililioni 30 walizowekewa. Lengo wanazipata lakini matokeo yake zaidi ya shilingi bilioni 20 zinakwenda holela, wenyewe mishahara yao ni shilingi bilioni 8, zingine zote zinakwenda kulipa madeni lakini kwenye vifaa malighafi wanaambiwa tafuteni mmpe *AGGREKO*, *SONGAS*, *IPTL*, *DOWANS*, *RICHMOND*, hivi kweli jamani

mtu anafanya kazi ili aoneshe ufanisi kumbe anafanya kazi kwa manufaa ya makampuni ambayo hajui hatima yake.

Mheshimiwa Spika, mikataba isiyofahamika, tunaongeza mikataba kwa maslahi ya nani? Mimi nafikiri uchambuzi, na kurudi nyuma si kushindwa uongozi, kurudi nyuma kutafakari hayo uliyoyafanya halafu baadaye urudie. Lakini narudia tena wote waliotajwa katika *RICHMOND,* hata hiyo, Benki Kuu itakayokuja huwezi kutajwa kama jambo halipo, kama halipo laja. Kwa nini wasimtaje Spika? Kwa nini wasimtaje Tatu Ntimizi? Mbunge wa Igalula unatajwa kwa sababu unahusika na unajua wanasheria bahati nzuri Waziri Mkuu wetu ni Mwanasheria, Mwanasheria ndiyo huyo Mwanasheria mnasema *circumstantial evidence is the best evidence to convict* na huwezi kutajwa kama hukuhusika, kwa nini utajwe wewe? Sasa kutajwa tajwa kunakosesha sifa, kunaleta hisia za ubadhirifu, naomba sana haya makampuni yaliyoletwa kwa njia nzuri, yafanyieni kazi kipindi cha mwezi wa nne tupate jibu muafaka isije tena tukaanza kulumbana, hatutaki, tunataka mfanye kazi kwa utulivu.

Mheshimiwa Spika nimeona nichangie hayo machache lakini Watendaji wote waliohusika wanakuja kukana, tena ushahidi huu siyo wangu, ulipokuwa unasema ulikuwa wapi mpaka leo uanze kukana, hapa unakuwa Petro na Yesu sasa anakana mara tatu. Wewe mtu mzima mwenye madaraka unaandika maelezo yako kwa hiari yako mwenyewe baada ya kuleta taarifa, unasema kwamba sikuwepo au sikusema hayo ni ya watoto wadogo wa *kindergarten.* Hata wa *primary* hawazungumzi maneno hayo, kwa hiyo, hawa wote wawajibishwe mara moja mwezi wa nne tukija hapa tusikie hawapo kama hawa wanasiasa walivyoondoka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante sana (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ntimizi, namwita sasa Mheshimiwa Grace Kiwelu, wakati huo ajiandaye Mheshimiwa Charles Keenja na kama Mheshimiwa Lyamba yupo basi ndiye atakayefuatia baada ya hawa.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujadili hoja muhimu ambayo ililetwa na Kamati Teule ya Bunge. Kabla ya yote niunge mkono maoni yote ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukupa hali halisi ambayo ilitokea ndani ya Bunge siku ile ya semina na wewe ukapokea wito na kuweza kurejea tena na kuahirisha safari yako ya Marekani. Vinginevyo hali ingelikuwa mbaya zaidi. Nakupongeza sana kwa kuweka maslahi ya Taifa mbele na kuahirisha hayo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na baada ya kusoma hivi vitabu nilikaa na kujiuliza, hivi mzalendo wa nchi hii ni nani? Kwa sababu katika maelezo ya watu waliotoa ushahidi humu ilionyesha jinsi viongozi wetu wale walioaminiwa na kupewa madaraka na wananchi ili waweze kuwatetea na kusimamia maslahi ya Watanzania walivyoweza kujiingiza katika sakata hili la *Richmond*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ilinisikitisha sana na niwapongeze wale walioweza kujiuzulu na hatimaye Rais akalivunja Baraza. Mimi nasema kuvunjwa kwa Baraza bado haitoshi. Wale wote waliohusika kwa njia moja au nyingine wote wachukuliwe hatua. Niweke tu tahadhari, ni vizuri wale wote waliotajwa pasipoti zao ziweze kuzuiliwa, wasiweze kutoroka nchi, kwa sababu tuhuma zilizoko humu ni kubwa sana. Kila unaposoma kila mmoja anasema sikuwepo, nilikuta faili limekwishapitishwa; na kwa kuwa mradi huu ulikuwa ni wa dharura kila mtu anajitoa na kujitetea. Kila mtu anatakiwa kuwajibika katika kazi yake, hata kama ulikuwa likizo na ukakuta faili limepita ulitakiwa ulipitie na kutoa mapendekezo yako. Kama kuna mahali palipokosewa basi paweze kurekebishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikushukuru kuna mmoja alianza kujitetea kwamba ushahidi amesingiziwa, hakusema hivyo. Naamini kabisa Mwenyekiti wa Kamati aliwaambia kila anayeongea pale vile vitu vinakuwa *recorded*. Hansard zipo na *tape* zipo. Hakuna walichosingiziwa, inawezekana ni vitisho wanaogopa, sasa wanaukana ukweli. Hao wote tunaomba wachukuliwe hatua kali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme lililowaingiza Watanzania hasa wale maskini kwenye matatizo makubwa, uchumi wao uliporomoka hasa wale wa hali ya chini. Wale wakubwa waliweza kununua majenereta, waliweza kuendelea na shughuli zao. Nitawazungumzia sana akina mama waliokuwa na shughuli zao ndogo ndogo kama *Salon* na vijana walishindwa kufanya kazi zao kwa sababu ya tatizo la mgawo wa umeme. Hili haliniingii akilini na Watanzania walitegemea kabisa baada ya kuambiwa unakuja umeme wa dharura kwamba kazi hii itafanywa vizuri. Lakini kinyume chake waliweza kuipa Kampuni ya *Richmond* ambayo tunaambiwa ilikuwa haina sifa wala fedha ya kuweza kufanya kazi hiyo. Lakini kwa wale wachache ambao walijua wana maslahi ndani ya kampuni hiyo, waliweza kuidhinisha *Richmond* ikapewa kazi ile ambayo ilishindwa kuitekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mamilioni ya fedha zaidi ya shilingi bilioni 200 yaliingia katika ule mradi. Watanzania bado wana shida nyingi, hatuna shule za kutosha, hatuna zahanati, hazitoshi na kama zipo hazina dawa, walimu wanalalamika. Wiki iliyopita walimu walisema wataitisha mgomo kwa sababu wanaidai Serikali marupurupu yao, nauli zao, likizo bado hawajalipwa. Lakini watu wachache wanadiriki kwenda kuingia mkataba mkubwa namna hii na kuacha Watanzania wakiumia. Hili hatutakubali na Bunge tutaendelea kusimama imara na naomba wenzangu wa upande wa CCM katika maslahi ya taifa wote tushirikiane na tuwe kitu kimoja kutetea maslahi ya Watanzania. Tusiogope. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lilisemwa sana kwamba tumepoteza mwelekeo, hatuna kazi tunayoifanya hapa. Lakini kwa hili tu la Richmond Watanzania wamerudisha imani kwa Bunge lako. Tunawaahidi Watanzania kwamba tutaendelea kutetea maslahi ya Watanzania bila woga na kama ni siasa basi tutakutana nje ya *gate* ya Bunge na si ndani ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitasema machache tu kwa sababu wenzangu walishasema mengi. Kama nilivyoanza kusema kwamba wale wote waliotajwa kwenye hili sakata la Richmond wachukuliwe hatua za kisheria. Wapo wanaolalamika wameonewa, haki inapatikana mahakamani. Kama kuna wanaodai wameonewa tungeomba pia suala hili liweze kufikishwa mahakamani, ukweli ujulikane nani amehusika, nani hakuhusika. Wale waliohusika ikibidi kile chochote walichokipata kutoka Richmond kirejeshwe kwa Watanzania ni mali ya Watanzania na wachukuliwe hatua zote kisheria. (*Makofi*)

Kama nilivyosema mwanzo, tuweze kuzishika pasipoti zao ili wasikimbie waweze kujibu tuhuma zinazowakabili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, machache naomba niungane na Kamati Teule ya Bunge kuunga mkono hoja zote zilizoletwa na Kamati hiyo. Tunawaomba wasiogope, najua wanapata vitisho vingi, lakini kazi waliyoifanya ni ya Watanzania na tuko pamoja nao na tutaendelea, tunaomba pale itakapoletwa hoja na kuona kwamba ina maslahi ya Watanzania basi Kamati Teule za Bunge ziundwe kufuatilia, maana yake yako matatizo mengi, ipo mikataba mingi ambayo inaendelea kuliingizia taifa hasara. Tungeomba kama walivyokwisha kusema wenzangu sasa ufike wakati mikataba ije mbele ya Bunge, wale tuliotumwa na wananchi ndani ya Bunge hili tuweze kupitia na kutoa ushauri kama mikataba hiyo ina manufaa na maslahi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace Kiwelu. Namwita sasa Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, atafuatiwa na Mheshimiwa Lyamba, sijui yupo! hayupo basi kama hayupo ningeomba ajiandae Mheshimiwa Ruth Msafiri na baada ya hapo Mheshimiwa Said Nkumba.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika suala hili. Lakini kabla ya kuchangia nilikuwa naomba niseme jambo moja dogo. Naomba Wabunge wa Upinzani waepuke sana hiki kishawishi cha kujifanya kwamba wao ni watetezi wa wananchi wa nchi hii na kwamba sisi wa CCM siyo. Nataka niwahakikishie kwamba wananchi wanaridhika na utetezi wanaopata kutoka kwenye Chama cha Mapinduzi na ndiyo maana tunapata kura nyingi za kutufanya tuongoze Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua zilizochukuliwa na Serikali hivi karibuni za kumteua Waziri Mkuu mwenye uwezo mkubwa sana na Baraza jipya la Mawaziri, hasira zetu zimepungua kwa kiasi kikubwa sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua hizo alizochukua ambazo zinajaribu kurudisha nchi yetu kwenye reli ili tuendelee kama tulivyokuwa tumepanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada tu ya uchaguzi wa mwaka 2005 lilipitia wimbi la ujambazi wa kutumia silaha kwenye mabenki, likadhibitiwa, tunaipongeza Serikali.

Inaelekea sasa kuna wimbi la wizi wa kalamu wa kutumia makampuni ya bandia. Hii *Richmond* ni moja, lakini tuliposikia ule uchafu kwenye Benki Kuu yalikuwa makampuni zaidi ya 13, yote yaliyoundwa mahususi kwa ajili ya wizi. Tunaomba Serikali ijizatiti, kama ilivyojizatiti na ujambazi wa silaha, tupambane tena na wimbi hili la wizi wa makampuni hewa. Bunge hili pamoja na wananchi na vyombo vyote vya umma tushirikiane kuhakikisha kwamba tunashinda wimbi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili suala la *Richmond* na nafikiri na makampuni mengine ya umeme ambayo hayakuzungumziwa kwa undani humu, lilifanyika kwa makusudi, halikufanyika kwa bahati mbaya wala halikufanyika kwa uzembe. Ingekuwa ni bahati mbaya na uzembe Bunge hili lingesamehe. Lakini lilifanyika kwa makusudi, watu walijua ni nini wanafanya, wakafanya kwa makusudi na hapo ndipo panapokuwa pagumu sana mtu kusamehe kwa sababu walishauriwa. Walishauriwa na *TANESCO*, *PPRA*, walishauriwa na kila chombo kilichotakiwa kuwashauri lakini bado wakaendelea kututumbikiza katika hali hii ambayo tuko sasa hivi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, inabidi tukubaline kwamba hatua za kuchukuliwa lazima ziwe kali kweli kweli, bahati mbaya sana jambo hili linaathiri wananchi wa Tanzania ambao tunachangishwa kulipia uchafu huu. Tunachangishwa umeme, ulipandishwa kwa asilimia 23, wiki mbili zilizopita ulikuwa upandishwe tena, tunachangishwa ili tulipie gharama zinazotokana na vitendo hivi vya makusudi. Mimi nafikiri ifike mahali tulionee taifa hili huruma, tuwaonee Watanzania walio maskini huruma, watu wachache wanajaribu kujinufaisha na mimi nahisi hawa wanaojinufaisha na mapesa haya ni Watanzania wala sio Wamarekani wa *Texas*. Kwa hiyo, tuwabaini na tuwadhibiti, tuhakikishe kwamba wamechukuliwa hatua za kutosha kabisa zitakazo kuwa fundisho kwa wengine, wasirudie vitendo vya namna hiyo, vinginevyo taifa hili litafika mahali litaangamia kwa sababu tu limeingiliwa na mchwa ambao unalitafuna kutoka ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba hili tulititilie maanani na Serikali ihakikishe kwamba inachukua hatua zinazostahili. Matokeo ya matendo haya, moja, nililosema la wananchi kuchangishwa ili tulipie gharama hizi, lakini la pili uchumi wetu unaathirika vibaya sana kwa sababu mapato ambayo tungeweza tukayatumia kwa shughuli nyingine ndiyo haya tunayoyatumia sasa kuwalipa hawa ili wanenepeshe matumbo yao na mimi nafikiri kwa kweli hili jambo halistahili huruma hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia vitendo hivi vilifanyika ndani ya Serikali, havikufanyika ndani ya *TANESCO*, *TANESCO* tunaambiwa waliitwa tu kutia saini na wakati mwingine walisita, mara nyingi walishauri kwamba jambo hilo halikuwa sawa sawa, walitaka kuchukua hatua za kutunusuru, lakini bado Serikali ikalazimisha kwamba hatua zichukuliwe. Sasa haya matokeo yaende wapi? Yaende kwa *TANESCO* ama yaende kwa wananchi ama yarudi kwenye Serikali? Mimi nafikiri Serikali lazima ikubali kuwajibika na hizi zilizotokana na vitendo hivyo na itutafutie hizo pesa huko zinakolipwa ili zirudi kujazia pengo hilo. (*Makofi*)

*TANESCO* sasa hivi tunaambiwa iko *ICU* taabani, mahututi, haijimudu hata kidogo, kutokana gharama hizo inayolipishwa, *Richmond* peke yake shilingi milioni 152,

hivi zingejenga shule ngapi za sekondari, zingejenga shule ngapi za msingi, zingenunua vitabu kiasi gani watoto wetu wakasoma? Ama zikanunua madawa hospitali zetu zikaweza kutibu wagonjwa. Pesa hizi zinalipwa, zinaingia kwenye mifuko ya watu na zinalipwa na wananchi hawa walio maskini, tunaomba sana Serikali itafute hawa wanaohusika warudishe pesa hizi zinazolipwa, na ibebe jukumu hili ili *TANESCO* iweze kujiimarisha tena, iendelee kufanya majukumu yake na ipunguze kututoza sisi wananchi tunaotumia umeme gharama za kulipia gharama hizi. Natambua kama Serikali ikibeba mzigo huu kama ilivyobeba mzigo wa *IPTL* itakuwa na maana kwamba kuna mambo ambayo tutafanya na mimi nasema wakati Serikali inakubali kubeba huu mzigo iwatafute wanaohusika warudishie pesa hizi ili huduma zetu zisiathirike ili tusiache kufanya yale mambo tuliyopanga kufanya kwa sababu tu kuna watu waliokuja wakatuibia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili jambo linaudhi, linauma na sijui ni maeneo gani mengine ambayo mambo machafu kama haya yanayotokea ambayo hatujayaona. Kwa kweli inabidi Serikali ikae sasa iangalie sekta zote na kuangalia tunafanyaje. Tumekuwa na malalamiko juu ya madini, tumekuwa na malalamiko sasa juu ya umeme na mambo mengi machafu. Hata Benki Kuu ambayo haijapatwa kuzungumzwa tangu tupate uhuru imeingia katika uchafu kama huu, inabidi tukae tuangalie ni nini kilichotuingia sasa hivi ambacho kinatuletea matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, nafikiri inabidi tuangalie vyombo vyetu vya usimamizi. Tumeambiwa TAKUKURU ilitoa taarifa kwamba hakuna uchafu wowote uliotokea, kwamba waliangalia mambo wakayaona safi isipokuwa kwa matatizo madogo madogo. Kamati yetu ilipokwenda kuangalia ikakuta huo ulikuwa ni uwongo mtupu kwa sababu uchafu ulikuwa ni mwingi na ulikuwa uko juu juu wa kuonekana kwa kila mtu. Sasa tunaulizana hivi kwa nini TAKUKURU chombo chetu cha usimamizi kilishindwa kusema ukweli kikasema uwongo?

Nani alikishinikiza? Je, ni tatizo gani lilikifikisha hapo? Haiwezekani kwamba kwa kuwa kinawajibika kwa wale wale wanaosimamia katika Serikali ndiyo maana kikafika hapo? Sasa sina hakika kama tukikiweka chombo hiki chini ya Ofisi ya Rais kitafanya kazi yake vizuri zaidi, kwa Rais wa sasa nina hakika kitafanya vizuri kwa sababu hataki upuuzi, lakini je, akija Rais na yeye akachukua mambo kilegevu legevu itakuwaje?

Haya tuna Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, naye anaripoti Serikalini huko huko lakini anasimamia mapato haya haya ya wananchi. Inabidi tukae tuangalie vyombo hivi viwekwe wapi ambavyo vitakuwa na uhuru kamili wa kusimamia na kuikagua Serikali na kupendekeza kwa Bunge hili hatua za kuchukuliwa pale panatokea uchafu. (*Makofi*)

Lakini tukiviacha huku ambako hatuna hakika juu ya usafi wake kwamba kila siku patakuwa pasafi tutapata matatizo makubwa sana siku zijazo. Kwa hiyo, napendekeza tuangalie vyombo hivi viwekwe wapi na kama inawezekana viwekwe hata chini ya Bunge moja kwa moja. Kwa hiyo, vinatumwa na Bunge, vinaripoti kwa Bunge, vitakapoona uchafu vitakuja kutuambia hapa tumeona uchafu na sisi tutaamua ni hatua

gani zichukuliwe, kama ni kuunda Kamati nyingine ama tutachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba uchafu huo unaondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba niunge mkono hoja ya Kamati Teule na niipongeze sana kwa kazi nzuri sana iliyofanya. Tunategemea kwamba siku zijazo kukitokea uchafu katika nchi hii tutaunda Kamati za Bunge, ambazo zitatufanyia kazi nzuri kama hii iliyofanywa na Kamati ya Mheshimiwa Dr. Mwakyembe. Tunaomba mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii pamoja na yale yatakayotolewa katika mjadala wa taarifa hii yatekelezwe na Serikali na tunaiomba Serikali ituletee taarifa ya utekelezaji ili tuwe na hakika kwamba kweli hayo marekebisho yamefanyika. (*Makofi*)

Hii mikataba na hivi vyombo vya umeme kuanzia na *IPTL* itazamwe upya na hatua zichukuliwe kusitisha mikataba hii ambayo inatuingizia hasara. Hatuwezi kuendelea kuwalipa *IPTL* shilingi bilioni 3 kila mwezi kwa kutokufanya lolote, wakitupa umeme tutalipa, wasipotupa umeme tunalipa, mimi sijapata kuona nchi ambayo inaweza kuendeshwa namna hii! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ichukue hatua mahususi na Serikali itoe taarifa hapa Bungeni kwamba imechukua hatua gani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Nalipongeza kwa dhati Bunge lako Tukufu kwa kukubaliana kuunda Kamati hii. Nakupongeza kwa uteuzi mzuri kwa wajumbe wa Kamati hii na vilevile naomba niipongeze kwa dhati kweli kweli Kamati yenyewe kwa jinsi ilivyofanya kazi yake kwa umakini wa hali ya juu sana, kwa uangalifu, kwa uzalendo, kwa uwazi, kwa ukweli na kwa hakika kuweka bayana kila kile walichokuwa wamekiona kwa kina kwa imani waliyonayo. Kwa kweli nawapongeza sana, na ni mfano wa kuigwa kwamba Bunge hili kwa jinsi ambavyo ziko hoja nyingi tete mbele yetu, inaonekana kwamba kutakuwa na umuhimu wa kuwa na Kamati mara kwa mara teule za Bunge, Kamati hizo ziige mfano wa Kamati hii wawe wakweli, wawazi na hakika wakusudie kuliletea Bunge kitu ambacho ni kizuri na kitasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Kikwete, jinsi alivyolipokea suala hili kwa uangalifu wa hali ya juu na hata akaweza kuunda Baraza jipya la Mawaziri, nampongeza sana. Lakini nashukuru jinsi alivyoliangalia suala hili kwa sababua aliacha na shughuli zake nyingine akamwita na Makamu wake wa Rais, ili wakae pamoja waone hili jambo wanalipeleka vipi kwa sababu aliona ulikuwa ni wakati wa kulishughulikia kwa makini, kwa kweli nilifurahi sana nilipopata taarifa hizo na nimeona Rais wetu anajali sana Tanzania yetu. Mwenyezi Mungu amzidishie hekima na busara na hata mengine yatakapokuwa yanakuja mbele yake basi yaweze kupita kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme siku ilipokuwa inasomwa hoja hii Bungeni, katika kitu kilichonikasirisha cha kwanza, nikasikikitika kweli kweli, kilikuwa ni chombo cha TAKUKURU. Tulikuwa na imani kubwa sana kwa TAKUKURU, siku hiyo nilisikia nimedhoofika, nilisikia nimekata tama, nikajiuliza sasa kama kuna chombo ambacho kinaonekana eti tunakiamini tumekipa nguvu kubwa, tumekipa madaraka makubwa juu ya viongozi maisha yao na mali zao juu ya vyombo vyetu halafu hicho hicho kinakwenda kutuambia uwongo, nilisikitika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naungana mkono na wenzangu kwa yote waliyokwishapendekeza juu ya hatua za kuchukuliwa dhidi ya watendaji ndani ya Serikali na ndani ya vyombo siyo tu kwa viongozi pekee, naunga mkono hatua hizo zichukuliwe kwa wote wanaohusika, wote wawajibishwe na pale inapokuwa kuna haja ya kuwapeleka mbele ya sheria zaidi wafikishwe huko juu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili naomba uzalendo uwepo kwa kila mmoja. Katika taarifa inasema kwamba baadhi ya wajumbe ama watendaji walioitwa na Kamati kwenda kutoa ushahidi walionekana kwamba walikuwa wanatoa ushahidi kwa namna ya kufundishwa fundishwa hivi hivi. Sasa kama kuna mtu anakufundisha unaweza ukasikiliza, lakini wewe uliyefundishwa na wewe si una uzalendo wako, wewe umekuwaje kuwaje Mtanzania kama kuna mtu anaweza kukufundisha uwongo na wewe ukaupokea? Sasa hali hiyo mimi niliona kwamba si pekee ni vitisho lakini labda na ubinafsi umepamba mno watu wanajiangalia sana nafsi zao wenyewe badala ya kuangalia taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo sio utamaduni mzuri, naomba watu wasipende sana vyeo wapende kutumikia Watanzania, wawe tayari kuachana na hivyo vyeo inapokuwa hoja iliyo mbele yao inalazimisha hivyo wawe tayari. Lakini kama kuna hoja unatakiwa kutoa ufafanuzi naomba uwe tayari kwa sababu unatumikia nchi yako, unatumikia nafsi yako, unatumikia wenzako, hujajibeba wewe mwenyewe hata kama ni cheo ulipopewa wewe wenzako waliachwa si kwa sababu ni bora sana kwa sababu ulionekana wewe wakupe kwanza nafasi basi uende ukawakilishe wenzako, ni lazima uwe mkweli. Kama unalipwa mshahara jua kwamba unabeba jasho la wenzako, usipende mshahara peke yake ili wenzako kuwaumiza, kwa kweli nimesikitika sana. Kwa hiyo, ninachopenda kuomba ni kwamba ile hali ya Watanzania kuwa na ujasiri wakati wowote ndiyo itawale nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa sababu wenzangu wameshachangia sitaki kurudia sana lakini basi niseme moja, yale yote malipo wanayolipishwa *TANESCO*, si halali, si halali kuiua *TANESCO* kwa sababu tu wameshinikizwa kuingia katika mikataba ambayo hawakuitaka. Watanzania sasa hivi wanaumia, wanataka umeme, hawawezi kupata umeme walionao, tayari matatizo kila siku lakini malipo kila siku yanapanda, wengine na mimi nikiwemo tulikuwa tunailaumu *TANESCO*, sasa tumekwishajua tatizo. *TANESCO* iachwe ikusanye pesa zake halafu izitumie kwa kujiendeleza yenyewe. Serikali ikubali ibebe gharama zote ilizoibebesha *TANESCO* sasa ziwe zake yenyewe, ndiyo ibebe mzigo, hakuna namna, mzazi wa *TANESCO* ni Serikali, hakuna namna, hayo

yaliyopelekwa yakaibebesha *TANESCO* sasa yabebwe na Serikali. Shilingi milioni 152 za kila siku ambazo hata leo wanazilipa *TANESCO*, zilipwe na Serikali, maeneo mengine yote yaliyotajwa na wenzangu *SONGAS, IPTL, AGGREKO* yote Serikali ikubali iyabebe. (*Makofi*)

*TANESCO* iachwe iendelee kutoa huduma kwa Watanzania kwa kadri inavyoweza na kigezo kilichokuwa kimeanza kujitokeza sasa hivi kwa *TANESCO* kwamba wanaweka biashara mbele badala ya kuweka huduma mbele suala hilo si sahihi kabisa. *TANESCO* ikubali kutoa huduma kwenye shule zetu za msingi na sekondari bila kujali kwamba wanapata faida, hakuna faida pale lakini wale wanaokwenda kuwasaidia waweze kujifunza vizuri ndani ya maabara ama ndani ya mitambo ya kompyuta. Wanawaandaa kuwaWatanzania wazuri wa kesho, sasa kuwanyima umeme eti kwa sababu hawana faida si sahihi, wanavijiji wana vinu vyao kidogo, wanasagia mahindi wawapelekee umeme. Hii ni huduma, hicho kidogo walichokuwa wanapata watapa. Bei ya umeme ishuke ili watumiaji wawe wengi sana, viwanda vingi vianzishwe viweze kutumia umeme, *TANESCO* izalishe kwa kadri inavyoweza ikiwa inajua itafanya yote mawili. Kwanza huduma, pili, pesa inazopata ndiyo biashara yenyewe. Lakini kutanguliza biashara ikaacha huduma kwa Watanzania jambo hili halifai kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naunga mkono mapendekezo yote ya Kamati Teule ya Bunge, yote yachukuliwe hatua, ahsante naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kama ulivyotangulia, mimi sipongezi, naanza moja kwa moja. Kwanza, nimeisoma ripoti hii ni safi, haina fitina majungu wala haikuwa na nia ya kuwaharibia watu majina, naipongeza sana ripoti kwa usahihi kama jinsi ambavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, ameiwasilisha ripoti yake kwa mbwembwe hata mimi kama ningepata hiyo nafasi ningewasilisha kwa mbwembwe kwa sababu alikuwa na uhakika na kile alichokifanya.

Timu kama inashinda dakika za mwisho basi una uhakika wa kupiga chenga kama unavyotaka, kwa hiyo, mbwembwe zile zilikuwa ni mbwembwe za kuhakikisha kwamba kile ambacho tulimtuma Mheshimiwa Dr. Mwakyembe na Kamati yake wamekifanya kwa usahihi, nawapongezeni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wote waliochangia wameunga mkono, wengine wameunga mkono kwa kusema, wengine wameunga kwa kukaa kimya, wengine wameunga mkono kwa kujiuzulu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kwa maslahi matatu, kwanza, kwa maslahi ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Sikonge wanaoteseka na bei kubwa ya umeme, lakini pili kwa maslahi ya taifa ambalo limedhulumiwa na watu wachache ambao tumewakabidhi dhamana za kuongoza umma huu wa Watanzania, lakini wamekosa uadilifu, wamekosa uaminifu wa viapo walivyoapa kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Lakini tatu, nimesimama hapa kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi, hadidu zako za rejea, hadidu ya kwanza ilikuwa ni kutaka Kamati itupe maelezo *Richmond* ni ya akina nani. Ukiisoma ripoti, ukaimaliza yote, ukairudia tena utajua *Richmond* ni hawa ambao kwa sababu Marekani hawap, wale wote waliohakikisha kwamba *Richmond* wanapata mkataba ule, hao ndiyo *Richmond* hakuna wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niende kwenye suala la *TANESCO*. Shirika hili liliundwa kwa madhumuni makubwa ya kuwapa unafuu wananchi wetu wa gharama hii ya Nishati ya Umeme. Lakini mkataba huu mbovu uliojaa mizengwe na harufu ya rushwa umewabebesha Watanzania kwa kweli mzigo wa kulipa fedha nyingi sana. (*Makofi*)

Sasa tarehe 23 Juni, 2006 waliweka mkataba na Richmond na baadaye *DOWANS* ambayo mmoja wa Wabunge wenzetu hapa Mheshimiwa Rostam Aziz ametajwa kwenye ukurasa wa 9 wa ripoti kuwa na uhusiano nayo, ndiyo ambayo inaendelea kupokea hizo fedha shilingi milioni 152 kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu, fedheha kubwa. Mimi niombe wale wote waliohusika pamoja na wale ambao hawakuwa katika madaraka ya Serikali, wengine wako katika madaraka ya kichama, wengine wako katika madaraka ya Ubunge, lazima hatua za kinidhamu zichukuliwe. Jambo hili hatuwezi tukaliacha hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeibiwa, badala ya fedha hizi zijenge barabara vijijini, zinunuwe madawa kwenye Zahanati zetu, wananchi wapate maji safi na salama, tuongeze uwezo wa kupeleka pembejeo za ruzuku kwa wananchi wetu wakulima, badala ya fedha hizi tuwalipe walimu wanaodai malimbikizo na ujenzi wa madarasa, watu wachache wanaliibia Taifa!

Mheshimiwa Spika, suala la kujiuzulu haliwezi kuwa ndiyo suala la mwisho. Bado hatua za kinidhamu, hatua za dharura za kuhakikisha kwamba Watanzania wanaridhishwa, hatua sahihi bado zinastahili kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati hii inaendelea na kazi yake, Mheshimiwa Rostam Aziz, na Mheshimiwa Ndugu yetu Daniel Yona waliitwa kwenye Kamati, hawakufika! Na Kamati katika maelezo yake mwishoni, haikutoa maelezo ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya hawa watu. Sasa naomba waongeze pendekezo la kuchukuliwa hatua wakati wanamaliza kujibu hoja yao hapa. Kuchukuliwa hatua watu wote waliodharau kazi ya Bunge. Kwa sababu kwa kutotii mamlaka hayo ya kuitwa wamemdharau Spika, wamelidharau Bunge, wamedharau Watanzania, jambo hili haliwezi likaruhusiwa liendelee. Naomba hatua zichukuliwe na mapendekezo ya Kamati mwishoni basi yatuonyeshe njia kwamba ni hatua gani zitachukuliwa dhidi ya hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la uadilifu wa viongozi. Sehemu ya tatu ya Azimio la Arusha linahusu Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kwenye kifungu cha uongozi bora. Ukurasa wa 39, kinasema: Naomba ninukuu: "Viongozi lazima wawe mfano mzuri kwa wananchi kwa maisha yao". Nataka niseme hapa, kuna hii hoja ya Biashara na Siasa.

Nataka niseme kwamba si wafanyabiashara wote si waaminifu. Lakini wapo wafanyabiashara si waaminifu na wanatafuta kila namna ya kuingia kwenye siasa ambayo ndiyo wanaona ni kinga. Akisha kuwa kwenye siasa atapata kila kitu. *(Makofi)*

Wanasiasa wa namna hii lazima wabainishwe na huu ni mfano uliojionyesha kwenye Richmond. Ni mfano tu. Leo hapa hata ukienda katika maeneo mengine yote, utaona tenda kubwa kubwa zina watu maalumu. Wewe mwingine lazima ukapige magoti kwao ndiyo upate tenda, hata wafanyabiashara wengine nafikiri watakuwa wananiunga mkono. Lazima ukapige magoti kwao ndiyo upate tenda. Hata wafanyabiashara wengine watakuwa wananiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tulikuwa na wafanya biashara waadilifu. Akina Mzee Syks, akina Mzee Rupia, akina Amir Jamal, walikuwa waaminifu na wamefanya kazi nzuri mpaka leo wanaheshimika. Siyo baadhi ya wafanyabiashara wa leo. Kwani kuwasaidia wananchi, kuwapelekea maji wananchi, kuwapa msaada wananchi wasiojiweza ni mpaka uwe Mbunge au Diwani? Unaweza ukafanya hivyo bila ya kuingia kwenye ubunge wala udiwani! *(Makofi)*

Unaweza ukafanya hivyo, bila ya kuingia kwenye Ubunge wala udiwani. Wako watu wengi tu tunawaona hapa, hawajawa na hisia hata siku moja za kuingia kwenye siasa. Kina Mengi hao, tunawaona kila siku wako wanasaidia watu, hatujawasikia wanataka kugombea hizi nafasi. *(Makofi)*

Niwaombe wafanyabiashara tuige mifano ya wazee niliyowataja hapa. Kama umeingia kwenye siasa kwa ajili ya kuhakikisha biashara yako inakwenda kwenye utaratibu ambao wewe unatupeleka sasa kwenye masuala ya matatizo kama haya ya Richmond, sasa tutakuwa wakali kweli kweli. Na hatutaoneana haya humu ndani, tutaambiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, wakati Mheshimiwa Msabaha anachangia hoja yake alisema kwamba anaondoka huko kuja kushughulikia Wanyamwezi na Wasukuma. Kwanza nasema kwamba uwezo wa kuwashughulikia Wanyamwezi na Wasukuma hana. Na sisi Wanyamwezi na Wasukuma enzi za zamani, Watemi wakifa haya ni mambo ya ndani nayasema hapa, walikuwa wanazikwa na wasindikizaji. Sasa Mheshimiwa Msabaha siyo Mtemi wa Wanyamwezi na Wasukuma, kwa hiyo, hawezi kuzikwa na msindikizaji. Anakufa peke yake, atazikwa peke yake. Kwa hiyo, kifo chake sisi tunakisaidia. Sanda yake hii hapa, kitabu hiki cha Richmond. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Loo! Ahsante Mheshimiwa Said Nkumba. Sasa namwita Mheshimiwa Rwilomba, ajiandae Mheshimiwa Magdalena Sakaya na baada ya hapo Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi nami nizungumze kidogo juu ya hoja iliyo mbele yetu ambayo ni tete, nyeti, ambayo vilevile imeamsha hisia nyingi sana na bahati mbaya sana nafikiri ni bahati nzuri,

ningezungunza mwanzoni nilikuwa na machungu mengi na mazito sana. Nadhani ningelia tu kwa sababu ingekuwa ni hatari ukigundua kwamba jamaa anakuibia kwa staili ile badala ya kuzungumzia unakwenda kumshughulikia, lakini sasa Mheshimiwa Rais ameshusha hizi pumzi. Nimpongeze tu Mheshimiwa Rais kwamba amefanya kazi nzuri na wewe Mheshimiwa Spika, umefanya kazi nzuri kuli-*handle* hili jambo. Sasa hivi angalau tunazungumza tukiwa tuna raha kidogo, tunapumua na wananchi sasa hivi wanajisikia vizuri. Wakati inaanza kwa kweli ilikuwa ni zito na tulipata simu kali kali sana kutoka kwenye majimbo yetu. Lakini tunashukuru limeenda vizuri, nakupongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kuwa mwaangalifu na kuwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri aliyoifanya na kweli ni kazi nzuri sana. Niipongeze Tume, kwa kweli tunashukuru kutuonyesha. Mmetuonyesha kitu kizuri, mmefanya kazi nzuri, imerudisha matumaini ya wananchi kwamba si sote ni majambazi, kuna wengine walikuwa wanasoma kwenye magazeti, walikuwa wameanza kutuhesabu wote ni majambazi. Lakini sasa tumeona kwamba mmetuonyesha kwamba wako wahusika na kweli tunashukuru sana Mheshimiwa Dr. Mwakyembe pamoja na wenzako, mmefanya kazi nzuri na mmekuwa jasiri. *(Makofi)*

Mimi kwa sababu ya furaha niliyonayo nilikuwa naiomba Serikali kuwa sasa huu umekuwa ni mwanzo. Kuna mengine yanayozungumzwa, nadhani twende zaidi. Hapa pawe mahali pa kuanzia na huko BoT twende huko. Twende tuweke Tume au walete ripoti tuielewe vizuri, tuijadili vizuri hapa. Wanaohusika washughulikiwe vizuri. Nadhani ni zaidi ya yale ambayo tunayasikia. Nasema hivyo kwa sababu mimi kwangu kulishaanza kuwa ni tatizo. Michango midogo midogo wananchi tulikuwa tukiwaambia, walikuwa wanajitolea sana. Lakini walifikia mahala ukiwaambia tuchange, wanakuambia eeeh! tuchange nyinyi mkale! Sasa ilikuwa ni vigumu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hao watu ambao wanachukua mali zetu ni vizuri tuzidi kuwafuatilia. Nashukuru sana Mheshimiwa Mwakyembe umefanya kazi nzuri sana na nimekuwa nikifuatilia sana hata wengine wanapozungumza, pembeni kuna maongezi yanajitokeza kwamba wengine hawakutendewa haki, hawakuhojiwa! Najaribu kufikiria kwa nini inasemwa hawakutendewa haki, hawakuhojiwa na ni nani anahojiwa huyo? Naweza kukubaliana kwamba hawakutendewa haki kwa sababu tungepata labda wengi zaidi, wangesema wengi washiriki. Washirika wengi wangesema walioshiriki.

Lakini vilevile naangalia je, ni maadili gani? Kwa mfano unakwenda kumhoji Mheshimiwa Pinda pale sasa hivi yeye ni Waziri Mkuu. Nilikuwa nampigia pigia simu ovyo ovyo, sasa hivi nikikutana naye nasimama pembeni, naruka. Ni baba sasa hivi. Sasa unaenda kumhoji baba yako anakulaje, unaongeaje, hiyo ni hekima kweli? Mimi nadhani walitumia hekima kuona kwamba atapima na mwishoni wamesema kuwa atapima. Kwa hiyo, wale wanaosema kwamba hawakumtendea haki Waziri Mkuu nadhani wajaribu kuangalia Waziri Mkuu ni nani? Kwa hiyo, hapo naungana na Kamati kwamba walifanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Ndugu zangu waliopewa jukumu sasa hivi tunaomba sana. Jana Mheshimiwa Rais alisema maneno mazito sana pale, wale ambao mlikuwepo eneo la CCM pale.

Alisema maneno mazito, tusingependa kurudia, lakini naomba tujitahidi tufanye kazi iwe nzuri. Kwa kweli hatutapenda kusikia tunaambiwa jamani kasungura kadogo, kumbe wengine wanakula kote, tunaletewa manyoya. Kasungura kadogo, wewe unakula kote, unatuambia kasungura kadogo, wewe unachukua sehemu yote. Shilingi bilioni 54 zinazochukuliwa na Richmond, mimi juzi tukiwa humu walisema Bukombe wanapeleka umeme kwa bilioni 4.5. Kwenye jimbo langu la Busanda ukipeleka bilioni 2 linawaka lote.

Sasa bilioni 54 unapeleka kwenye familia yako halafu unakuja hapa kasungura kadogo, sijui namna gani bwana! Hili hatuwezi kukubaliana nalo tena bwana! Tutataka uje uthibitishe kadogo kwa namna gani? Kote kamekuja au sehemu mmechukua na wenzako kule chini? Tena naomba tuanzie chini, wote waliohusika washughulikiwe sio waning'inizwe tu wale wa kisiasa kule juu. *(Makofi)*

Kuna wale walioshughulikia *technical data* wakasema hii Richmond inafaa, wale waliohusika. Na wenyewe ni vizuri waweze kuwajibishwa na tuangalie ni wakati gani tunapoingia mikataba, tuangalie ni vipi kama kuna makosa. Ni namna gani tunaweza kuondokana na mkataba huo, wanasheria wanafahamu, wasituambie kwamba eti mkataba, unaingia mkataba ambao huwezi kujinasua. Unaning'inia mpaka mwisho jamani. Hivi kweli unaingia mkataba ambao mpaka mwisho.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana uamzi uliotolewa na Serikali, nakubaliana nao na hasa Mheshimiwa Rais wetu kukubali wenzetu kuachia ngazi. Lakini napenda kusema kwamba wenzetu wawe makini. Kule vijijini ni mateso. Mimi sina umeme kwangu, sasa hivi nachangia shule. Shule wanajenga, wananchi wanahainga tunakamata kuku. Wanauza vitu vyao ili waweze kujenga shule. Lakini nikiangalia ilipotolewa ripoti ya shilingi bilioni 133 ukianza kupiga hesabu ingekwenda wapi? Zingejenga shule ngapi? Tungekuwa hatuna malalamiko sana. Lakini mtu mmoja kachukua. Mimi nafikiri bado tunahitaji twende zaidi na zaidi ili tuweze kupata jjibu.

Mheshimiwa Spika, jana wakati wana-*wind up* Mheshimiwa Waziri Mkuu, alizungumza maelekezo aliyopewa na Mheshimiwa Rais, moja ni la biashara na siasa na uongozi wa umma. Mimi sikatai biashara na uongozi wa umma, lakini tuwe makini. Isije ikawa biashara ndiyo sehemu huku kwenye uongozi wa umma ni kichaka cha kujificha au kwenye siasa ni kichaka cha kujificha. Na hii ndiyo inasababisha mtu unamkuta wakati mwingine ni *mockery* hata kwa wananchi wetu na hivyo unatoa mapesa mengi, unapata kura, unakuwa Mbunge unakuwa sijui kiongozi, unakuwa mahali unajificha, inawezekana hata usihudhurie, kwa sababu kuna wakati utafanya hivyo. Sasa *it is a mockery* kwa wananchi wako na kwa Serikali, *it is a mockery*.

Sasa ndiyo unakuwa ni mwanzo wa rushwa. Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri hilo sisi tutakuunga mkono, hiyo kazi aliyokupa Mheshimiwa Rais kulifanyia kazi sisi tutakuunga mkono. Nyinyi tengenezeni vizuri tu, sisi tutakuunga mkono kwa hatua zote, ikiwezekana kama ni namna ya kupatikana Mbunge ambaye hakutoa rushwa basi ifanyike iwe hivyo. Watu wengine sasa wanaanza kupata hofu, lazima tufanye hivyo,

kufanya hivi kidole jiangalie na wewe. Wewe maisha yako unawazia kuingia kwa rushwa tu. Tutamalizana, kama humu unakuja ili kuja kuwaumiza.

Ndugu zangu kuna maneno mengine hayapendezi, unayasikia pembeni, unayasikia maneno maneno mengine ya pembeni. Labda nitoe mfano mmoja wa Arusha. Ndugu zangu, mimi mwaka jana mlinichangia hapa, kijana wangu kuoa, mkanipa fedha. Nikapeleka kijana wangu kufanya sherehe kubwa tu akafurahi. Sasa ana mke wake, lakini sijaona hata mmoja ananiuliza vipi kijana analalaje na mke wake? Sijaona! Ni kwamba sasa anaishi na maisha yake, mwacheni awe na mke wake sio na wewe tena unaanza kufikiria eti kwa sababu ulichangia sasa na wewe uwe na sauti ya kumpelekesha anavyotaka kuishi na yeye. Mwacheni awe na maamuzi na aone inavyokwenda, sasa ukianza kumsimanga hivyo si vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru sana, baada ya hapo naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kabla ya yote naomba kutoa shukrani zangu za pekee kwa Kamati Teule, na kwa Wajumbe wote kwa kazi nzuri walioifanya kwetu sisi Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla tumeiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo waliosema kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti, kawasilisha ripoti yake kwa mbwembwe nyingi, madaha mengi. Mimi ninadhani kwamba kazi aliyoifanya ana sifa zote za kuweza kuiwasilisha atakavyo, kwa madaha, kwa furaha, kwamba kafanya kazi inayokubalika. Nampongeza sana Mwenyekiti pamoja na timu yake nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nikupongeze wewe mwenyewe pamoja na Wabunge wote kwa kukubali kuundwa kwa Tume hii kwani Kamati hii imetoa matunda mazuri na Watanzania wote tumeiona.

Mheshimiwa Spika, tunakuomba kazi hii isiishie hapa, twende kwenye Mikataba mingine yote, ziundwe Kamati, zichunguze tutajua mengi zaidi ya haya tuliyoyapata Inasikitisha sana kuona kwamba viongozi waliopewa dhamana na heshima kubwa na ya pekee na Watanzania kuwahudumia kwa umakini na kwa uaminifu, wanatumia nafasi zao, wanatumia nyadhifa zao kuweza kujineemesha. Na zaidi kabisa kwa kutumia matatizo ya Watanzania, kujineemesha, kwa kweli inasikitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ambavyo Tanzania iliathirika kwa kiasi kikubwa kwa kukosekana kwa nishati ya umeme mwaka juzi, sikutegemea kabisa wala sikuwahi kuhisi kama yupo mtu mwenye akili yake timamu anaweza kutumia nafasi hiyo kujichotea mali. Sikutegemea kabisa! Lakini kwa kweli tumeona, tumeona wapo wanaofurahia matatizo ya wenzao, tumeona wapo wanaofurahia umaskini wa Watanzania, shida za Watanzania kwa ajili ya kujilimbikizia mali.

Hili ni jambo la ajabu, inaonyesha jinsi gani Watanzania tusivyokuwa na uzalendo. Uzalendo viongozi wetu hawana, tunaomba sana viongozi wetu wawe na uzalendo kwa sababu bila ya uzalendo tutakuwa hatuna uchungu wa nchi yetu, na hatuwezi kuwahudumia wananchi kwa uaminifu na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua wote jinsi gani *TANESCO* imeenda kwenye hali mbaya. Tunatambua jinsi gani gharama za umeme zimepanda. Tunatambua jinsi gani gharama za umeme pamoja na kukosekana kwa umeme ziliathiri taifa hili la Tanzania kiuchumi, kijamii, na kila nyanja iliathirika na ndiyo iliyopelekea mpaka sasa hivi gharama za vitu mbalimbali za maisha zimepanda, ni kutokana kwa kukosekana kwa nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kutumia shilingi milioni 152 kwa siku kwa shirika moja kulipa kwa kitu ambacho hakipo kwa kweli hakuna mtu anayeweza kulaumu kitu kama hicho. Kwanza mimi nadhani mataifa ya nje yanatushangaa, huko tunakoomba misaada tunaomba, tunaomba, tunaomba! Haya tunayojadili sasa hivi wanatushangaa, na kusema, "hivi hawa watu wamelala," tutaamka lini? Natoa rai kwa Watanzania, kwa Waheshimiwa Mawaziri, kwa Waheshimiwa Wabunge, kwamba sasa kila mtu aone kwamba ana wajibu wa kusimama kidete kuweza kupigania rasimali zake, kuweza kuitetea nchi yake, kuweza kuijenga nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mmoja angependa kuwa na umeme. Kila siku Waheshimiwa Wabunge wanasimama Bungeni, kila mmoja na jimbo lake, tunaomba tuletewe umeme vijijini, tunaomba tuletewe huduma ya maji, tunaomba tuletewe huduma ya barabara. Tunachoambiwa ni kwamba kambuzi ni kadogo. Kambuzi ni kadogo? Mbona kambuzi kadogo kanaishia mifukoni mwa wachache? Haka kambuzi kadogo kwa nini basi tusigawane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule vijijini kwa mwendo tunaoendana nao sasa hivi, kwa kuona kwamba Shirika letu wameliua, ninachosema ni kwamba walidhamiria kuliua. Vigezo vilivyotumika ni vigezo hewa kukubali kampuni hewa kuingia mkataba wa kuzalisha umeme wakijua kabisa kwamba hiki hakipo. Ninadiriki kusema kwamba walidhamiria makusudi kwa uchu wao, kwa ufisadi wao na kwa kutumia nafasi zao kwa ajili ya kuligandamiza Taifa hili kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa maskini milele na hawatokaa wajikomboe hata siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi gharama za umeme zimepanda kiasi ambacho kwa namna moja au nyingine zimechangia kikubwa uharibifu wa mazingira kwa wale ambao hawafahamu. Hakuna Mtanzania wa kawaida sasa hivi anaweza kutumia nishati ya umeme kwa ajili ya kupikia jikoni hawezi! Gharama yake ukiweka jiko la umeme huwezi kulipa gharama mwisho wa mwezi. Matokeo yake hata Wabunge hapa, hata Mawaziri wengine wamejikita kutumia mkaa.

Hata tupige kelele, tunaongea, tunapambana lakini haiwezekani kwa sababu mwananchi lazima ale, lazima apike, lazima atumie nishati, atatumia nini? Umeme umepanda gharama, mafuta ya taa hayashikiki, nishati zingine zimepanda, inabidi aende

kwenye nishati mbadala ambayo ndiyo mkaa. Kwa hiyo, tatizo la kupambana na uharibifu wa mazingira na uharibifu wa misitu halitaisha kama gharama za umeme haziwezi kushuka. *(Makofi)*

Wananchi wengine mpaka sasa hivi vijijini, *TANESCO* imetoa gharama kwamba anayetaka kuunganishiwa umeme atoe shilingi laki sita kwa ajili ya kuunganishiwa umeme. Ni Watanzania wangapi wenye nguvu hiyo, wenye uwezo huo wa kutoa laki sita ili waweze kuunganishiwa umeme. Ni Watanzania wangapi? Kwa kazi ipi wanayoifanya? Kwa kipato kipi wanachokipata? Kwa maisha yepi ambayo yamekuwa yakipanda kila leo hapa Tanzania? Matokeo yake unakuta kwamba wananchi wetu huko vijijini wataendelea kukaa gizani milele. Hawatajikomboa, vinginevyo itumike nguvu ya ziada. Na kinachotakiwa hapa ni viongozi wanaohusika walio na dhamana hiyo kuhakikisha kwamba *TANESCO* inafanya kazi. Pale ilipofikishwa wote tumeona. Ni jukumu la viongozi wenye dhamana kuitoa *TANESCO ICU* kuipeleka mahali pazuri ili iweze kufanya kazi kuhudumia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mchakato mzima wa utoaji wa zabuni ya Kampuni hii ya Richmond ambao ulitaliwa na uvunjaji wa Sheria za nchi ambazo tumezitunga sisi wenyewe Wabunge, uliotawaliwa na ukiukwaji wa taratibu mbalimbali, ambao umetokana na shinikisho la viongozi wenye dhamana, na kupuuza ushauri wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (*PPRA)*, utagundua kwamba kuna uovu sana wa viongozi wetu katika utendaji kazi wao.

Siamini kabisa kwamba mtu umewekwa kwenye nafasi yako kwa kutumia utalaamu ulio nao kwa ujuzi wako, kwa taalauma yako na wengine wamewekwa pale kwa sababu ya taaluma maalumu. Lakini anakubali kupokea *order* kutoka juu kwamba fanya hiki akijua kabisa kwamba kile kitu anakwenda kinyume cha taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba watumishi wa umma waondoe woga. Wasimame kusimamia kazi zao kwa uaminifu, wasikubali kupokea *order* kutoka juu wakijua kwamba wanakiuka taratibu. Hili pia wananchi wenyewe sasa hivi waondoe woga, ile hali ya kuwa waoga tumekwishakuwa waoga kwa miaka 46, umaskini umeendelea kutukandamiza, ni muda wa kuamka sasa tusimame kidete, viongozi wasimame kidete, watumishi wasimame kidete kwa ajili ya maendeleo ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU, mwaka jana tulipitisha sheria hapa ya kuipa meno. Sisi Wabunge tulifurahi kweli kweli. Watanzania wote walifurahi sana kwamba sasa ile rushwa ambayo imenuka, imeota mizizi, Tanzania imepata dawa na tuliipa meno ili iweze kushughulikia rushwa vizuri. Lakini kwa jinsi ambavyo TAKUKURU imeonyesha udhaifu kwenye suala hili la kushughulikia mkataba wa Richmond, sisi Wabunge na wananchi wote wamepoteza imani moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba TAKUKURU tuipige chini, Mkurugenzi wake tumchukulie hatua inayostahili. Hiki ni chombo muhimu sana, hatutegemei kabisa kifanye kitu kilichokifanya. Na yamekuwepo malalamiko mengi

kutoka kila kona kwamba TAKUKURU mlioipa meno inatafuna dagaa tu, uwezo wa kula samaki wakubwa haupo. *(Makofi)*

Kambale wanapita tu lakini dagaa inatafuna! Sasa tumethibitisha kwamba TAKUKURU sasa hivi hawana meno ya kutafuna kambale, wanakula dagaa tu! Tumepoteza imani kabisa, inasikitisha kwa TAKUKURU hatuna imani nayo tena. Tunaomba kabisa hatua za msingi zichukuliwe kuhakikisha kwamba tunapata chombo kilicho huru kilicho kiaminifu kitakachotenda kazi kwa kuzingatia maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Siamini kwamba kweli Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wataalamu wake wanaweza kukaa wakajadili suala ambalo wanajua kabisa hii kampuni haipo. Lakini wamekaa vikao wamejadiliana na mihtasari imetolewa na mihuri imegongwa kwamba kampuni hii iwepo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hiyo imeonyesha udhaifu mkubwa sana kwa Watanzania, imeonyesha udhaifu mkubwa kweli kweli na inaonekana kwamba sasa hivi hata imani haipo. Kwa hiyo, naomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu akianzia yeye mwenyewe wajipange, vinginevyo wale wanaoonekana kwamba hawapo kwa maslahi ya Taifa wapigwe chini.

Ni chombo muhimu sana, panapofikia mahali mwananchi anaona kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeshindwa kutenda haki kwa suala la jamii, hata kitakachotokea kingine chochote kile hatuna imani nacho tena.

Kwa hiyo, ipigwe chini kabisa na wale wengine wote sio viongozi waandamizi tu wa juu, wengine wote, wawe ni Makatibu, Wajumbe wa Kamati mbalimbali waliohusika kujadili suala hili wachukuliwe hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nitoe angalizo. Naomba sana kiongozi yeyote yule aliyeshiriki hata kugusa hata kidogo tu kwenye suala la Richmond hatua kali zichukuliwe dhidi yake na wakati huo huo wakati tunajiandaa kuwachukulia hatua, Serikali ihakikishe hawatoki ndani ya nchi hii. Tumeona suala la Gavana Ballali, tusije tukasikia fulani sijui alikwenda Marekani, sijui Uingereza, tunaomba sheria ichukue mkondo wake wakiwepo hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ni watu ambao wamechota Sh.152mil kwa siku moja, sio mchezo. Ni watu ambao wana fedha nzuri, wamefungua akaunti kila mahali, wana uwezo wa kwenda popote na kwa muda wowote, tusipowadhibiti, watakimbia. Kwa hiyo, natoa angalizo kwa Serikali kwamba kuanzia sasa hivi, wahakikishe watu hawa hawaondoki, wahakikishe kwamba Sheria inachukua mkondo wake wakiwa hapa hapa ili hela hizi zirudi kwetu ili Watanzania tuendelee kujinasua kutoka kwenye umaskini ambao umekithiri kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya mikataba. Kila siku tumekuwa tunasimama hapa tukiomba mikataba muhimu iletwe hapa Bungeni. Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, ni kwa nini wanafichwa mikataba hiyo? Kinafichwa kitu gani kwenye mikataba ya wananchi?

Mheshimiwa Spika, majibu tuliyokuwa tunapewa ni kwamba mkataba ni mali ya Serikali na mwekezaji. Sasa tumegundua siri kali ndani ya Serikali ni kitu gani. Tunaomba sasa hiyo siri kali iondoke. Tunaomba mikataba yote nyeti ikiwepo ya madini, ya umeme na mingine ambayo inamgusa mwananchi, iletwe hapa ili sisi tujiridhishe kwa niaba ya wananchi. Ninaamini kabisa, mikataba hiyo haiwezi kupelekwa kwa mwananchi mmoja baada ya mwingine lakini Mbunge ni mwakilishi wa wananchi, ni kwa nini tunanyimwa hiyo haki yetu ya kimsingi ya kuona mikataba hiyo?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Bunge lako linaonekana kuwa ni Bunge la kasi, tunaomba suala la kwanza kwenye Serikali mpya, mikataba yote muhimu iletwe hapa ili Wabunge tujiridhishe.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Bunge linapendwa na wananchi wote kutokana na mambo ambayo yanafanywa na Waheshimiwa Wabunge na wewe ukiwa kiongozi wetu. Kwa hiyo, tunaomba masuala yote yanayomgusa mwananchi, tuyaangalie kwa makini likiwepo la msingi kabisa la mikataba ambayo inadidimiza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu sisi Watanzania wote kwamba Serikali iliyoingia madarakani, sasa itafanya kazi kwa ajili ya manufaa ya wananchi kwa kuanzia na sisi Wabunge, ni matumaini yetu kabisa. Tunawaomba kiapo walichokula viongozi wetu Mawaziri, Manaibu Mawaziri na wengine wote, wakitumie kwa uaminifu. Mungu anatenda, Mungu anaadhibu tena hapa hapa duniani. Tumeona kwa jinsi gani watu wamejikaanga kwenye mafuta yao wenyewe. Kwa hiyo, tunaomba kiapo walichokula, wakiheshimu, wawatendee Watanzania haki kwa kuwahudumia kwa uaminifu ili kusaidia maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze tena sana kwa namna nyingine tena na niombe kwamba ule mkataba wa *BOT* ambao tulíletewa ripoti yake hapa kwa ufupi, kwa juu juu, taarifa kamili iletwe hapa, tuijadili sisi Wabunge ili tuweze kujiridhisha na kuona ndani yake kuna kitu gani.

Mheshimiwa Spika, mengi yamesemwa na wenzangu, sitasema sana kwa sababu hata hasira zangu, zimeshapungua kutokana na mambo yaliyotokea hapa katikati, naomba niishie hapa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zaidi ya 100 na ninaishukuru sana Kamati hii, wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi hii ili niweze kuchangia taarifa ya Kamati Teule kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kweli kwa kuipongeza sana sana Kamati Teule iliyoongozwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe kwa kazi nzuri sana iliyofanya. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana na Watanzania wameridhika sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ndugu yangu, kaka yangu, Dr. Mwakyembe, nilimpongeza huko nje lakini nitumie nafasi hii pamoja na wenzake kuwapongeza rasmi ndani ya ukumbi huu wa Bunge. Hongereni sana, tunawashukuru sana na Watanzania wanawashukuruni sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kwanza nianze kwa kuvipongeza sana vyombo vya habari. Navipongeza kwa sababu vyombo vya habari ndivyo kwa sehemu kubwa vilikuwa chimbuko la mambo mengi na ni chimbuko la mambo mengi ambayo tunayafanya hapa Bungeni na hasa haya ambayo yanafanywa kwa uficho zaidi. Navipongeza sana sana vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi na kipekee, nimshukuru sana sana huyu ndugu yetu anayeitwa Said Kubenea. Yeye ni Mhariri wa gazeti la Mwanahalisi. Gazeti hilo limeendelea kufanya kazi nzuri sana kwa sababu linatupa taarifa ambazo baadaye zikifanyiwa kazi, zinaonekana sio za uzushi kama wengine wanavyoweza kuamini lakini zinaonekana kuwa ni habari za kweli ambazo anakuwa amezifanyia utafiti. Nawapongeza sana na nawaomba wasikate tamaa pengine kwa vitisho vyovyote vile ambavyo wanaweza wakawa wanavipata kwa sababu nina hakika wanafanya hivyo kwa maslahi ya nchi hii na kwa maslahi ya Watanzania wote, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulipokuwa kwenye mkutano wetu wa Chama nilisema kwamba niliwahi kupigiwa simu na Mchungaji fulani akaniambia tunaomba sana sana Mwenyezi Mungu awafungulie ili muweze kuona yaliyopo ndani ya Kamati hiyo. Nikasema hakika Wabunge wamedhamiria kufanya kazi kubwa na kwa umakini juu ya hali hii. Nina hakika Mchungaji huko aliko ameyaona mambo ambayo yameendelea na amefarijika sana lakini na Watanzania wengine wamefarijika sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe mfano mmoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa na ninafurahi kwamba ninalisema hili yupo hapa ndani. Kuna Mfalme mmoja alikuwa anaongoza nchi, alizungukwa na wasaidizi wengi sana. Ndani ya nchi yake kulikuwa na matatizo mengi sana lakini wale wasaidizi wake waliokuwa wamemzunguka kwa sababu wengi walikuwa wanakula, walikuwa wanafaidika na yale ambayo yalikuwa ni mabaya kwa nchi yake, walikuwa hawako tayari kumshauri Kiongozi au Mfalme wa nchi ile. Pale nchi ilipokuwa inakwenda kwenye vita, inataka kuvamiwa na Taifa lingine, wale wasaidizi hawakutaka kumpa hizo habari yule mfalme.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mtu mwingine ambaye wanasema alikuwa na maono, watu wakasema hebu tumchukue huyu aende kwa Mfalme anaweza kumpa

habari za kweli kwa sababu walishakuwa na wasiwasi na wale wasaidizi. Lakini wale wasaidizi tena, wakampinga yule mtu kwenda kwa Mfalme lakini njia zote zikafanywa na Mfalme akasema mleteni huyo mtu mbele yangu. Akaenda mbele ya Mfalame, akasema Mfalme, nchi hii itaingia kwenye vita na wewe usipoangalia utapigwa na ninakusihi tuma Jeshi lako sasa hivi lakini wewe usiende vitani utakufa. Wale wasaidizi wakamwambia huyu muongo, anataka kukuponza ili utumbukie kwenye matatizo. Mfalme hakusikia ile hoja akaenda vitani na kweli akapigwa na akafa, nchi ikatumbukia kwenye maangamizo makubwa na kwenye vurugu kubwa. Nina hakika nchi yetu haikufika huko. Ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, aliwasikiliza washauri wake na nchi haikutumbukia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, ninamtahadharisha Mheshimiwa Waziri Mkuu ajue kwamba amezungukwa na washauri wengi. Ninaomba afanye kazi kwa umakini, sio kila jambo wanalomuambia hao washauri wake kwamba litakuwa sahihi. Nina hakika yeye atakuwa na uwezo wa kupima, kuchambua yale mazuri lakini mazuri ayafanyie kazi na yale mabaya ahakikishe anayaondoa mapema ili nchi yetu isitumbukie kwenye matatizo makubwa kama ambavyo imetumbukia sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa sana suala la TAKUKURU. Mimi nataka nizungumze suala la TAKUKURU kwa kutoa mfano. Wengine wanasema Taasisi hii siyo ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, wameiita ni Taasisi ya Kupamba Rushwa. Inapamba rushwa kwa sababu mambo ambayo wanatakiwa wayachimbue, wao wanayaona mazuri na wanayashabikia. Kwa hiyo, hii siyo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ni Taasisi ya Kupamba Rushwa bila shaka yoyote na nadhani Watanzania wengi wanaona tu ukweli kwamba Taasisi hii haifanyi kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye uchaguzi ndani ya Chama cha Mapinduzi ulioisha, kule Mbeya, kulitokea mambo ya ajabu sana. Kuna watu wamekamatwa kabisa wanagawa pesa, hili naomba tu niliseme kwa sababu ndiyo uwazi wenyewe, watu kwenye uchaguzi wa chama wamekamatwa wanagawa fedha, wameenda Mahakamani, lakini kwa sababu inasemekana walikuwa wa kundi fulani, kundi ambalo haliwezi kuguswa, basi wakubwa wakaagiza hebu waachieni hao na wakaachiwa. Kesi zilikuwa Mahakamani na Mahakamani huko zimekwenda hivyo hivyo baadaye kesi hazipo tena Mahakamani. Hii ndiyo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Watanzania wanaposema hii Taasisi ya Kupamba Rushwa, tuseme nini? Tukatae?

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Sheria yenyewe kama ilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu ni nzuri, tatizo ni watu ambao wako ndani ya vyombo hivi. Ndiyo kelele tunayopiga kwamba Mheshimiwa Rais na hili alione na vyombo vyote ambavyo vimehusika avione na kwa kweli awaondoe. Kwa sababu akijaribu kuangalia sehemu zote wanaoathirika na Sheria hii au na Taasisi hii, ni watu wadogo wadogo, wale wanokwenda kutibiwa, wanaompa Mganga yule Sh.1,000, ndio wanaokamatwa kwamba wametoa rushwa, mbona rushwa kama hizi wanazipamba? Hatujasikia kama wamechukua hatua yoyote. Naomba nishauri na hili pia lichukuliwe hatua kubwa sana na Mheshimiwa Rais ili kwa kweli kurudisha imani ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mikataba. Mikataba mingi na hii wenzangu wamezungumza, katika nchi hii imekuwa na matatizo makubwa sana. Sasa huu ni wakati muafaka wa kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, mimi niko kwenye Kamati ya Bunge ya Miundombinu, tumepata taarifa ya utendaji wa kazi wa Kitengo cha *TICS* kule bandari ya Dar-es-Salaam, naomba niliseme hili kama mfano. *TICS* iliingia mkataba wa kuendesha Kitengo cha Kontena pale Dar-es-Salaam mwaka 2000 ilikuwa mkataba wa miaka 10 lakini ilipofika tarehe 30/12/2005, *TICS* ikaongezewa mkataba mwingine wa miaka 15. Mkataba ule ulikuwa umefika nusu tu, wakaongeza miaka mingine 15 mbele, kwa maana hiyo, mkataba ule ukawa wa miaka 25.

Mheshimiwa Spika, tulihoji kwa nini mmeongeza mkataba kwa miaka 15 wakati kuna miaka mitano bado haijaisha, mmetumia kigezo gani? Taarifa tulizozipata kutoka Wizarani na bandarini, wanasema utendaji wa *Container Terminal,* ni mzuri ndio sababu tumeongeza muda.

Mheshimiwa Spika, kilichosikitisha ni kwamba taarifa nyingine tulizoendelea kuzipata ziliendelea kuonyesha kwamba utendaji kazi katika kitengo kile, ni mbaya kupita kiasi, watu wanalalamika kila siku lakini kuna taarifa zinasema kwamba utendaji wa kitengo hiki mzuri. Tukajiuliza swali moja tukasema, hivi ni utaratibu kuongeza mkataba katikati? Mkataba wa kwanza haujaisha, unaongeza miaka mingine 15 mbele, shida ni nini?

Mheshimiwa Spika, habari tulizozipata ni kwamba wahusika wa *Container Terminal,* ni viongozi wa Serikali na wengine walikuwa viongozi wa Serikali lakini kwa sasa wamejiuzulu lakini bado kuna sababu ya kufuatilia mikataba kama hiyo. Sisi kama Kamati tumesema lazima jambo hili tulifuatilie na tuwaletee wenzetu Wabunge walione na ikiwezekana ule mkataba usimamishwe, wamalize ile miaka mitano iliyobaki ambayo inaisha mwaka 2010 ndipo baadaye kama watakuwa na sifa washindanishwe na wenzao waombe tena, kama watakuwa na sifa, wapate, hatutakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndio sababu tunasema, jamani nchi hii tuna matatizo makubwa sana. Tunatanguliza maslahi yetu binafsi mbele zaidi kuliko maslahi ya Watanzania. Hapa inanikumbusha Mwalimu wangu mmoja aliwahi kunifundisha akasema, unajua kwa nini mapinduzi ya kijeshi ni sifa kubwa sana katika nchi maskini au nchi zinazoendelea? Huwezi kusikia mambo kama haya katika nchi zilizoendelea. Akasema tatizo ni umaskini, tatizo ni tamaa. Vitu ambavyo ni nadra sana kuvipata kwa nchi nyingine zilizoendelea kwa mfano Marekani na Uingereza, huwezi kuona mapinduzi ya kijeshi kule, kuna *smooth transition of Government.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana mikataba hii irejewe upya lakini rai yetu na kama Kamati ilivyosema mikataba yote sasa ili kuondoa usiri iridhiwe na Bunge lako Tukufu. Mimi sioni kuna shida gani kama tunaridhia Maazimio, tunatunga Sheria, mambo mazito kabisa ya nchi hii, lakini mikataba Serikali inakataa kuileta ndani ya

Bunge hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni mpya, sisi tuna matumaini naye, amshauri Mheshimiwa Rais, mikataba ipite Bungeni, iridhiwe na kama kutakuwa na matatizo, yataonekana ni matatizo ya Wabunge wote, ni matatizo pengine ya wawakilishi wa wananchi sisi ambao tuko Bungeni na sio matatizo ya watu wachache ambao tunajua kwa kweli wamefanya hivyo pengine kwa manufaa yao wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie dakika hizi mbili zilizobaki kwanza nikishukuru sana Chama cha Mapinduzi kwanza kwa kuikubali taarifa ya Kamati Teule ya Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, ninakipongeza sana Chama cha Mapinduzi. Kwa kufanya vile, Chama cha Mapinduzi kimeonyesha kwamba kimekerwa na mambo ambayo yanaendelea katika nchi hii. Tena kimeunga mkono mambo yote yaliyo kwenye Kamati, hakijasema kwamba hili hatuungi mkono, yote yaliyomo kwenye taarifa ile, yameungwa mkono na Chama cha Mapinduzi. Nadhani sisi wa Chama cha Mapinduzi, tumepewa heshima kubwa, tumejengewa heshima kubwa kwa wapiga kura wetu lakini kwa wananchi wa nchi hii kwamba Chama ambacho viongozi wake wametuhumiwa kujihusisha katika suala hili na chenyewe kimekiri wazi kabisa kwamba kinaunga mkono hoja ya Tume hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kuzungumzia taarifa za vyombo vya habari. Kuna gazeti hili hapa Mwanahalisi, ni chanzo cha habari kizuri sana. Gazeti hili la Mwanahalisi, toleo la jana, kwa idhini yako Mheshimiwa Spika, linamtaja kabisa, kama walivyosema wenzangu kwamba Richmond ni ya Rostam Aziz, gazeti hili hapa la Mwanahalisi. Sasa mimi nalindwa na Kanuni kwamba kwa sababu nasema hivi, naomba nisiambiwe nasema uwongo, gazeti hili limesema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gazeti hili linamzungumzia pia Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Ikulu, Salva Rweyemamu. Alipohojiwa pia na Kamati, alionekana kujua wazi kabisa kwamba kampuni hii ina mahusiano ya karibu sana na Mheshimiwa Rostam Aziz. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nchi ilipofika ni pabaya na hawa watu ndio wako kwenye Halmashauri Kuu za Chama cha Mapinduzi, wako kwenye vyombo muhimu vya maamuzi vya Serikali hii, tunaomba wachukuliwe hatua zinazostahili. Kama hatuwezi kuamini haya magazeti, basi iundwe Tume ya kulichunguza zaidi suala hili ili na hawa wenzetu wachukuliwe hatua ili Watanzania wajue kwamba Serikali yao sasa inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kusema kwamba naunga mkono Taarifa ya Kamati Teule kwa asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Itabidi niende kwa haraka kidogo lakini mengi ambayo nilikusudia kusema yameshasemwa.

Awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi, nimpongeze Waziri Mkuu, Mawaziri, Manaibu Waziri wote waliopewa dhamana ya kuongoza nchi hii katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, vilevile, naomba nichukue fursa hii, kumpongeza mtu ambaye hajatajwa sana lakini ndio chimbuko la taarifa hii, naye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji, Mheshimiwa William Shellukindo, pamoja na Kamati yake yote. Ujasiri wao kwa kweli umeonyesha mengi. Walikabidhi taarifa yao mwezi wa nne kama walivyotuambia, ikajadiliwa mwezi wa 11 baada ya mashinikizo kadha wa kadha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilipokuwa nataka kuchangia, watu wakaniuliza lakini na wewe nawe jamani, mambo si yameshaisha, unataka kuchangia nini? Mmoja akaniuliza kwanza Kilindi mna umeme maana sisi tuko kwenye hali ya dharura wakati wote na sijui tutaendelea kuwa huko mpaka lini. Lakini nikawaambia hizi ni kodi za wananchi wa Kilindi na vilevile uchumi wa Tanzania nao unawahusu kwa sababu nao ni Watanzania. Kwa hiyo, hilo ni moja.

Mheshimiwa Spika, mwingine akaniuliza, hivi ninyi, Waziri Mkuu na wahusika wengine si wameshajiuzulu? Sasa hapo ndipo ninapolenga suala halikuwa kujiuzulu. Binafsi mimi ni katika watu ambao wamesikitika kwamba watu wamejiuzulu mapema kiasi kile, nilijua itakuja, lakini sikupenda katika kiwango kile cha awali, kwanza, tulitaka tupate majibu ya hoja. Tunachozungumzia sisi ni kashfa ya Richmond, mkataba ule na matatizo yake, hatuzungumzii mtu kujiuzulu. Lakini yametokea yaliyotokea ila yalikuwa yawe mwisho. Mimi nikawaambia kwa sababu najua nazungumzia hoja na sikuwa nazungumzia nafasi ya mtu, hayo yana wakati wake.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kuweka tu msisitizo kwa mengi ambayo yameshasemwa. Kwa kweli kama nilivyosema, kwangu mimi uwajibikaji siyo kujiuzulu hasa kwenye kashfa ambayo inahusu fedha kama hivi. Tangu juzi, jana, mchana kutwa nimekuwa nikisikiliza hoja mbalimbali za Watanzania, wakitoa maoni yao katika vyombo mbalimbali vya habari, wengine wanapiga simu na wengine meseji, wanachotaka sio tena nani kasema nini, ni nini kimefanyika? Ukweli umedhihirika kwamba kumekuwa na kashfa kubwa sana kwenye mkataba ule ambao alipewa Richmond, Watanzania wanachotaka sasa hivi ni fedha zirudi kwa kufilisiwa au kwa taratibu nyingine zote za kisheria, mjadala nani kasema nini, kwa wakati gani, hayo ni maandishi yanabaki kwenye vitabu. Ukweli ni kwamba wanataka kuona fedha imerudi kwa ajili ya maendeleo yao na uchumi wa nchi yetu. Naona bado watu wanaendelea kusema ooh, mimi sikusema, mimi sikufanya, hayo yamepitwa na wakati ndugu zangu, sasa hivi tuangalie tunafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana nilishangaa sana, mmoja akauliza hivi, mbona sasa hivi Wabunge wa CCM wanacharuka wakati huko nyuma walikuwa hawasemi, mbona sasa hivi ghafla tu imekuwa hivyo?

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano, mnaweza mkawa mmezaliwa watoto watano au 10 kwenye familia moja. Kwa sababu mmezaliwa kila mtu kwa wakati wake, hamfahamiani tabia zenu vizuri. Kwa hiyo, mnakuwa mnavumilianavumiliana kumbe mwenzenu mmoja labda jambazi, natoa tu mfano sitaki kuhukumu, itafika mahali mtasema aah, aah, basi akae huko jela. Ndio yaliyofika hapo na ndio maana tumesema hivi tulivyosema.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie wananchi, Wabunge wa CCM si kwamba tulinyamaza, watu tuna taratibu tofauti. Wengine tulikuwa tunaangalia tupate hoja kamili lakini sasa tumepata na ndio maana tunasema kwa ujasiri wote na tutaendelea kusema pale ambapo tunaona tunahitaji kusema bila uwoga, bila hofu na kwa hekima.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka sisi tuliobahatika kusoma enzi za Mwalimu Nyerere, wakati nasoma *Arusha International School,* ilifika mahali baba yangu hana fedha ya kulipa ada tukawa tunafukuzwa. Akaja Baba wa Taifa, akasaini kwa wanafunzi wale kumi wa mwanzo ambao wanafaulu, *signature* yake ikawa JK, ndio *signature* yake, naikumbuka ile karatasi mpaka leo ninayo. Sasa nilivyokuwa nikiangalia *signature* ya Rais wa sasa hivi ni JK, nilikuwa najiuliza maswali mengi. Nikasema huyu ni JK na huyu ni JK, hivi vitu vinakuwa tofauti kiasi gani? Kumbe JK huyu naye ana busara anakwenda taratibu, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati hapa ilijibiwa kwamba Serikali ilikuwa haijui habari za *Richmond*. Mimi hapa sitaki kusema ni uwongo lakini nataka kusema sidhani kama ni ukweli. Kwa sababu gani? Mwaka 2004 kuna kampuni ilikuwa inaitwa *Africommerce,* walikuja watu hapa, wakati huo sisi wengine tulikuwa hatupo, lakini walikuja watu hapa kiongozi wake alikuwa ni Bwana Muro. Hawa watu walikuwa wamepewa nafasi ya kufanya utafiti na hatimaye kwenda kutekeleza mradi wa bomba la mafuta kutoka Dar-es-Salaam mpaka Mwanza. Kwa sababu habari yenyewe ni ndefu na muda wenyewe ni mfupi niseme tu kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, hawa watu baada ya kufanya utafiti na kutumia fedha nyingi, kuna maeneo ilibidi watumie fedha kulipa Jeshi ili waweze kupita na kufanya shughuli zao, baadaye kwa njia za utata, *Richmond* wakaja wakapewa ule mkataba japokuwa Serikali ya Marekani katika utafiti wake ilitoa kabisa maelezo kwamba hii kampuni haitaiweza kazi hiyo. Hilo lilitokea mwaka 2004 ambapo watu hawa akina Muro waliweza kufika Bungeni kutaka kusaidiwa na Wabunge. Waliweza kufika kwenye mikono ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuzuia Rushwa ya Wabunge, Mheshimiwa Zainab Gama pamoja na Wabunge wengine waliokuwepo wakati ule, walizungumza nao na mengi yalisemwa ndio maana ninashangaa mtu akisema hajahojiwa au si kweli, inatisha.

Mheshimiwa Spika, walieleza mengi na kwamba kampuni ni ya akina nani na ni vipi wamepata huo mkataba, yote hayo yalisemwa wakati ule, hawa watu wakashindwa kazi hiyo. Baadaye wamekuja tena watu hao hao ambao Serikali inasema haijui, wamekuja kuwapa tena mkataba mwingine, wameshindwa. Pengine lisingelipuka hili, tusingejua wangeweza kupewa tena na mikataba mingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nasema, hali hii inasikitisha na imefika wakati Serikali waseme ukweli. Mimi nasema kwa sababu namfahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu wa sasa kwa ukaribu sana, nina hakika ukweli utasemwa vinginevyo usiposemwa, hatutasita, tutaendelea kutafuta ukweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAKUKURU. Mimi nashukuru kweli habari hizi zimelipuka. Hata mimi nilikuwa najiuliza mara nyingi TAKUKURU ni ya watu gani? Ni ya watu wadogo au watu wakubwa? Utakumbuka, ooh, Mheshimiwa Spika, naomba radhi hapa kwa sababu kesi yenyewe iko Mahakamani lakini niigusie juu juu, kesi ya Wabunge wa kule Arusha ambao walikuwa wanagombea. TAKUKURU walifanya vitu vya ajabu sana ambavyo ukielezwa inashangaza lakini tukawaachia hivyo hivyo wakaendelea na ni kitu kidogo ambacho pengine hakina ukweli, hatuwezi kusema ukweli kwa sasa hivi kwa sababu iko Mahakamani lakini ni kitu ambacho kwa kweli TAKUKURU walitushangaza wengi labda kulikuwa na mkono wa mtu, ninavyosema mimi baada ya kuisikia habari yenyewe.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nilipata bahati ya kukutana na Hakimu wa Wilaya wa kwetu. Nikamuuliza mbona watu wanajaa nje ya Mahakama muda wote? Akasema hawa wote ni TAKUKURU, wamehamishia ofisi zao nje ya Mahakama, wanakaa wanasubiri tu Hakimu katoka nje kamsalimia mtu ambaye labda ana kesi, hapo hapo wanamdaka, mnaongea nini, rushwa?

Mheshimiwa Spika, kule kwangu wamemfuata mfanyakazi wa Mahakama ya Mwanzo mpaka nyumbani kwake wakamkamata na rushwa, wakampeleka ndani, mke wake hayupo, ikabidi watoto wake waende, hali hii inasikitisha. Yale ambayo yanakusudiwa kufanyika hayafanyiki na TAKUKURU imekuwa kama ya kina fulani na fulani na fulani, huku wanatetea maovu makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nashukuru hatua iliyofikiwa, naunga mkono kwamba wawajibishwe lakini sioni kama TAKUKURU inafaa, tubuni chombo kingine cha kusimamia rushwa na sio tena kile ambacho kilikuwepo. Kwa kweli mimi nadhani hiyo ndiyo itakuwa msimamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo niongezee tu, mahabusu wangapi wako kule jela? Wengine tuna ndugu zetu, Watanzania ndio rafiki zetu wako ndani, wako mahabusu miaka na miaka kutokana na kesi za TAKUKURU ambazo hazina uthibitisho na wanashindwa, kila siku unasikia hakuna ushahidi, hakuna usahidi. Kwa hiyo, hivi ni vitu ambavyo vinatia uchungu kweli hasa sisi ambao tunawakilisha Majimbo ambayo yako mbali sana ambapo mnaweza mkashindwa hata kujua ukweli ulivyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu nidhamu ya uwoga kwa watumishi wa umma, mwenzangu mmoja amejaribu kulieleza lakini na mimi naomba nilizungumzie. Tumeona kwenye hii ripoti, nidhamu ya uwoga ni kubwa sana kwa watendaji wa Serikali. Tujiulize ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, nimefanya kazi Serikalini miaka 21, ni kweli kabisa kama usipokuwa mwoga, utawajibishwa. Nimekalia cheo kimoja tangu nimemaliza *Degree*

yangu ya pili, kwa miaka 14 sikupandishwa, kwa sababu gani? Ninasema ukweli na ninakataa. Sasa inafika mahali lazima ukubali kujitoa.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu watumishi wa Serikali mliobaki, mimi ndio maana nilitoka, ilifika mahali nikaona napoteza muda wangu, maisha yanakwenda, nikaja kwenye siasa. Kama hamuwezi basi tafuteni sehemu nyingine lakini jengeni ujasiri na ujasiri utajengwa endapo viongozi hawa watakuwa wanahakikisha kwamba wanafanya yale ambayo ni ya kweli.

Mheshimiwa Spika, niwape moyo watumishi wengine wa Serikali, kama unaona yule *direct* humuwezi basi panda juu mtafute hata Mbunge mmoja mnong'oneze, sisi tupo kwa ajili yenu, tutayafanya hayo. Wengine tume-*risk* makubwa sana, pengine nisingekuwa leo hapa kama mnavyoniona lakini nime-*risk* kwa sababu ya kutaka haki itendeke na ndio maana nipo hapa nilipo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu nidhamu ya woga kwa wananchi. Kwenye ripoti tumeona wananchi wameshindwa kujitokeza kutoa ushahidi wa mambo mbalimbali, wenyewe wananong'ona lakini njoo sema rasmi, wanaogopa. Nadhani kuna haja ya kujenga imani kwa wananchi wetu ili waweze kusema waliyonayo. Mtu anasema kidogo, jamani tabu atakayoipata huyo mtu, anaweza ahame hata eneo.

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi wa watu ambao kwa kusema ukweli walinyanyaswa, walifanyiwa kila aina ya jambo. Sasa hii tabia lazima ifike mahali ikomeshwe ili kuwapa wananchi ujasiri na naomba hili tulianze kuanzia leo na ikibidi basi semina mbalimbali ziendeshwe na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuwapa wananchi ujasiri wa kusema yale ambayo wanayo na yanawakera vinginevyo itaishia tu kwamba labda wananchi hivi na hivi.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba niseme tu hapa, hii taarifa imezua mengi, baadhi tumepata vitisho, sijui ndugu yangu, Dr. Harisson Mwakyembe na Kamati yake hali ikoje na hawana ulinzi wala nini lakini *of course* mimi naamini Mwenyezi Mungu akiamua niondoke, nitaondoka.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni ili mjue kashfa zitakuja, kwenye magazeti tutaandikwa, tutachorwa vikatuni vya ajabu ajabu, hapa mama Shellukindo na wengine lakini hivi ni vitu ambavyo lazima vikemewe maana wengine hapa sasa hivi wanashindwa hata kutoka kwa sababu wanawindwa hapa na pale. Kwa hiyo, nasema kwamba kuna haja kabisa tuangalie tunafanyaje.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu mmoja alinipigia simu, akaniuliza, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu kajiuzulu, je, marupurupu yake yako pale pale? Bahati nzuri nilikuwa Utumishi, najua kuna Kanuni ambayo inaelezea kabisa mafao ya wastaafu katika nafasi kama hiyo ya Waziri Mkuu lakini kwa wanojiuzulu na hususani kwa mazingira ambayo amejiuzulu Waziri Mkuu huyu, mimi najua kabisa hastahili.

Mheshimiwa Spika, labda wapo watakaolisemea lakini wananchi wengi jana walichangia suala hilo kwenye redio kwamba ni vema mzigo wa marupurupu sasa upungue sio tena mambo haya yamefanyika, ameshatengeneza huko bado tena aendelee kutengeneza kama ilivyo kawaida. Naomba niwahakikishie kwamba kitu hicho kama kumbukumbu zangu ziko sahihi, hakuna na kama kipo basi kiletwe hapa kwenye nyumba hii tuweze kukijadili na tuweze kukiwekea mkakati.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, naomba nitoe pongezi sana kwa Waandishi wa Habari ambao wamekuwa mstari wa mbele sana kuelezea mambo haya. Sasa nimeelewa kwa sababu nilikuwa najiuliza hivi kwa nini magazeti mengine yanaitwa ya udaku? Kumbe ndiyo yenye taarifa za ukweli ambazo hatutaki kuzisikia. Mimi kuanzia sasa, magazeti yangu ni hayo mnayoita ya udaku, ndiyo nitakwenda nayo, kumbe yanaeleza ukweli, yanachambua mambo kwa kina na bila uwoga.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nimechunguza baadhi ya Waandishi ni watu wenye akili sana, ma-*genious* mashuleni ambao pengine hawakubahatika kupata ajira kwingine lakini pengine ajira *best* ilikuwa ni hii. Kwa hiyo, naomba tuondoe neno la udaku, hakuna cha udaku, ni taarifa wananchi wanaeleza kwa njia ambazo wanaweza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, nataka kuzungumzia zile *generator* ambazo nimezisoma kwenye hii taarifa kwamba zina uwezo wa kuzalisha *megawatts* 105.6 lakini zenyewe zinazalisha *megawatts* 20 tu, sasa sisi kule Kilindi hatuna umeme, hatuwezi kufikiriwa? Ninaomba majibu kwa atakayejumuisha, hatuwezi kufikiriwa basi ili na sisi tunufaike na hizi *generator* zifanye kazi iliyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema yote hayo, naomba nirudie tena kusema kwamba naomba mapendekezo ya Kamati yatekelezwe. Naomba wachukuliwe taratibu za kisheria ambazo zipo na za Kikatiba na kadhalika lakini ni lazima mapendekezo yale yatekelezwe. Kila aliyeguswa ambaye anaona hausiki basi aende Mahakamani atoe taarifa tofauti. Ninachosema mimi ni kwamba kila mmoja achukuliwe hatua mapema tu tusingoje haya mambo ya kavutana kwa muda mrefu sana, kama kuna watu wanaona hawajatendewa haki, nimeona pale Mheshimiwa *Attorney General*, Mwanyika amesema hajahusika na nini, basi iende kwa utaratibu, atoe maelezo yake lakini vinginevyo hatua zichukuliwe bila uwoga, bila hofu. Tuhurumieni mimi na Mheshimiwa Shellukindo, maana wote tumehusika na imebidi jana nimwambie, Mzee naona sasa tuandike *will* yetu, makabidhiano ya mali zetu, tumpelekee Mwanasheria maana hatujui itaishia wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niko tayari kwa lolote, subirini magazeti yatanichora kwa sababu hata leo asubuhi nimepigiwa simu na watu wa magazeti wanasema kuna habari zako, tuzitoe? Nikawaambia toeni kwa sababu ya mambo haya, tusiogope, twende mbele na kazi ifanyike.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naipongeza tena Kamati, nawapongezeni sana Waheshimiwa Wabunge, Wabunge wenzangu wa *CCM* tuungane

mkono, tusiogope kwa sababu tunalindwa na Katiba, Sheria na Kanuni ambazo zinaongoza nchi hii. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha shughuli za Bunge umefika. Kwa sababu ile orodha yetu imeparaganyika kidogo, niwatamke wale ambao watachangia jioni ili wafanye maandalizi. Jioni saa 11.00 nitaanza na *Dr.* Raphael Chegeni, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, atafuatiwa na *Dr.* Guido Sigonda, halafu Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

Baadaye nitaanza na wale Wanakamati ambao ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Lucas Selelii na atakayehitimisha ni Mheshimiwa Waziri wa Nchi Sera, Uratibu na Bunge, ndio atakuwa msemaji wa mwisho saa 01.30 hivi.

Kesho asubuhi nitamwita Mheshimiwa Stella Manyanya, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa *Dr.* Harrison Mwakyembe. Baada ya hapo, tutakuwa na mjadala wa kuyapitia yale mapendekezo na kuyapitisha kadri itakavyoonekana.

Niwakumbushe wasemaji wa jioni kwamba ni vizuri twende moja kwa moja kwenye mapendekezo, tuone yamekaa vipi ili tuyaboreshe. Anayetaka mabadiliko, anajua Kanuni, tunaweza kuyabadili.

Kesho tukishamaliza majumuisho ambayo ni ya dakika 60 kwa mtoa hoja, dakika 15 kwa Makamu Mwenyekiti kama mchangiaji, tutakuwa tumesogeza muda na ndio nitaweza kumuita Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge, nadhani itakuwa kwenye saa sita na robo hivi.

Ahsanteni sana na sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge*
*lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, mimi napenda niende moja kwa moja katika hoja ambayo iko mezani kwetu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ninapenda sana kuipongeza Kamati Teule ya Dr. Harrison Mwakyembe na wenzake kwa kazi ambayo kwa kweli kama Watanzania tunapaswa kuwapongeza na kuwatia moyo. Kazi waliyoifanya ilitaka ujasiri wa hali ya juu na kiwango kikubwa sana cha uadilifu. Ndiyo maana wamekuja na ripoti ambayo ilikuwa siri mpaka dakika za mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Mwakyembe pamoja na timu yake kwa kuweza kufanya kazi nzuri yenye uchambuzi wa kina. Tufike mahali Watanzania sasa tuanze kubadilika kwa sababu tusipobadilika hii yote itakuwa ni kitendawili. Lazima tuwe na utashi sasa wa kubadilika. Utashi wenyewe huu sasa lazima uende sambamba na mikakati yenye matendo, si kusema tu, kusema ni jambo lingine na kutenda ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia ripoti hii, Watanzania sasa tubadilike, tujitokeza waziwazi kukemea ufisadi, kukemea rushwa na kuangalia maeneo mengine yote ambayo yana utata kwa maslahi ya Taifa hili. Hii nchi ni ya Watanzania wote, kila Mtanzania ana hati miliki katika nchi hii, si nchi ya watu wachache. Inavyoelekea sasa hivi ni kwamba tunaingia katika wingu bovu sana la kuanza kuweka matabaka katika Taifa la Watanzania, matabaka ambayo ni hatari kubwa sana kwa mustakabali wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingi sana katika ripoti hii lakini kutokana na ulivyoshauri kwamba ni vema tujielekeze zaidi katika mapendekezo ya Kamati, nami najielekeza huko. Wenzangu wote wamezungumza kwa mapana, wameainisha mambo mbalimbali, nisingependa kuyarudia lakini napenda tu nisisitize yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, zile zama za kuwa na mikataba ovyo ovyo, sasa iwe mwisho. Huyu mama yao *IPTL* akamzaa Songas, akamzaa na *Richmond*, akaenda kwa kaka yake *Dowans*, biashara iishe. Haiingii akilini kwamba nchi inaingia mkataba na kampuni hewa na tuna watalaam katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wetu. Hiki ni kitendo cha kudhalilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kama ndiyo hivyo, bado mimi nasikitika sana kwamba mikataba kama hii inagharimu Taifa fedha nyingi sana ambazo ni za walipa kodi na wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa haraka mkataba wa *Richmond* peke yake, kwa muda wa mwaka mmoja ile *capacity charge* peke yake ni shilingi bilioni 55, hawa watu wanalipwa tu *whether* wamefanya kazi *or not* na hii ni fedha ya walipa kodi!

Mheshimiwa Spika, leo sisi tunalia umeme vijijini, tunalia gharama ya umeme imepanda, kumbe wenzetu wanakula kuku kwa mrija! Ndio, huku ni kula kuku kwa mrija. Hivi kweli Watanzania tutafika? Sasa naomba hii biashara iishe.

Mheshimiwa Spika, tumeona katika takwimu mbalimbali kwamba *TANESCO* peke yake mapato yake kwa mwezi mmoja ni bilioni 30 lakini zaidi ya bilioni 21 wanalipia hizi gharama kwa makampuni haya. Sasa shilingi bilioni nane au tisa kwa *TANESCO* kuendesha shughuli zao, haiwezekani!. Ninaomba kwa kweli hii nidhamu ya utendaji kazi ndani ya Serikali ibadilike.

Mheshimiwa Spika, nilishangaa sana nilipomsikia Mheshimiwa Waziri anasema kwamba nilipokea amri kutoka juu, kulikuwa na maelekezo kutoka juu, unaelekezwa wewe hujui cha kufanya? Kama unajua cha kufanya basi ungeamua kujiuzulu kwamba sitaki maelezo hayo kwa misingi hii hapa vinginevyo mimi najiuzulu. Hii *spirit* ingejenga

uwajibikaji katika taasisi zetu hizi za Serikali. Sasa kama unaelekezwa na wewe unafanya, ukiambiwa geuka kushoto, unageuka kushoto, lala chali, unalala chali, hii biashara iishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inatia uchungu sana kuona watu ambao wamepewa dhamana ya kuongoza nchi hii wanatumia dhamana hizo kwa maslahi binafsi, inatia uchungu sana kwa Watanzania. Leo hii tunawachangisha watu vijijini fedha kwa ajili ya kujenga madarasa, zahanati na shughuli nyingine za miradi mbalimbali. Hili ni tatizo kubwa sana, hawa watu kipato chao ni cha chini sana lakini bado anakamuliwa kwenye umeme, akifika kwenye bidhaa zinazidi kupanda bei leo hii wengine wanakula kuku kwa mrija, hii biashara iishe.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Kamati hii, nashauri kabisa kwamba ile dhana ya uwajibikaji ndani ya Serikali sasa ichukue mkondo wake. Mapendekezo yangu ambayo napenda niungane moja kwa moja na mapendekezo ya Kamati hii ni kwamba wale wote walioshiriki, kujiuzulu ni jambo moja, kuna kujiuzulu kwa sababu ya *political responsibility*, lakini kama umefeli kutimiza wajibu wako na ukasababisha hasara lazima uchukuliwe hatua za kinidhamu na upelekwe Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitoshi watu kujiuzulu, mimi nasema haitoshi kujiuzulu, lazima hawa watu tuwafikishe kwenye vyombo vya Sheria, ikiwezekana wafilisiwe kabisa. Ninapendekeza kwamba hili liwe ni kosa la uhujumu uchumi wa nchi *(economic sabotage)*, huu ni uhujumu uchumi wa nchi, hatuwezi kuuachia hivi hivi. Naomba kwa kweli wale wote ambao wamehusika, wameachia ngazi, wanaachia ngazi, lazima vyombo vya Sheria vichukue mkondo wake, tuwafilisi ili fedha hiyo iweze kurudi.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati mimi nilikuwa nchini Kenya, nilichangia kwenye mada moja, nikasema, Kenya ninyi kidogo mnatuzidi Watanzania kwa sababu Kenya wao kwenye ile *scandal* ya *Anglo-lease* na *Goldenberg* waliiba fedha za umma lakini Wakenya wakatumia sehemu kubwa ya fedha zile ku-*invest* ndani ya nchi yao. Kwa hiyo, ina maana kwamba *economic* ina-*multiple effect* kwenye uchumi wa nchi ya Kenya. Sasa zetu hapa zinaibiwa, zinatoroshwa nje, kiasi kwamba hata Mtanzania hawezi kunufaika na fedha hii kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, wenzetu wa Kenya wao wanaiba fedha lakini inabaki kutumika kujenga uchumi wao. Sasa naona hawa Mafisadi wa Tanzania ni wa kupindukia kwa sababu watu wanaweka fedha nje, wananeemeka wao na ndugu zao, wanakuwa miungu watu. Sasa nashauri kabisa kwamba hawa watu lazima tuwapeleke kwenye vyombo vya Sheria na tuwafilisi.

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana na Taasisi hii ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Hii taasisi nadhani tuna haja ya kuleta Azimio la Bunge hapa ili tuibadilishe moja kwa moja. Mapendekezo ya Kamati yanasema kwamba tujaribu kuiimarisha na kuipeleka kwenye Ofisi ya Rais, sawa ni mapendekezo mazuri sana lakini lazima tuikarabati upya taasisi hii. Hawa watu siku zote wao wanakula dagaa wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kampeni za uchaguzi, utaona wanafuata baadhi ya watu kwa maelekezo, hivi kweli wewe ni *profession* katika kazi yako unakuta mtu eti anatoa rushwa, amewakimbia, atawakimbiaje, *are you serious*, mnafanya kazi yenu kweli? Unakuta watu wanaotoa fedha kidogo kama Mahakimu, Walimu, Waganga sijui watu gani, hawa ndio wanaokamatwa lakini wale wenye rushwa nene, hawakamatwi, ni lazima hii taasisi tuibadilishe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia napendekeza kwanza Mkurugenzi wa Taasisi hii lazima awajibike moja kwa moja. Nashangaa mpaka leo hii sijamsikia na yeye anaachia ngazi. Nashangaa kwa sababu katika suala hili Taasisi kama hii muhimu, kutuhumiwa kwa jambo hili na ilitumika kuficha uozo wa mambo ya *Richmond*, leo unaiacha, wala hajasema kwamba jamani sasa mimi naachia ngazi halafu Sheria ifuate mkondo wake, yeye bado ameng'ang'ania anafanya nini huko? Hii ni aibu kubwa sana, ninaomba kesho tunapokuwa tunahitimisha, tuipe maelekezo Serikali.

Mheshimiwa Spika, bado Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nayo lazima ifanyiwe ukarabati. Mheshimiwa Rais ameonyesha nia yake njema ya kujaribu kuiboresha ofisi hii lakini ile *degree* ya kukosa *responsibility, high degree of irresponsibility* katika mkataba huu wa *Richmond,* ni kielelezo tosha kwamba hawa watu *they are not serious,* naomba wote waliohusika wawajibishwe kwa sababu tusipofanya hivi, hatuwezi kujenga nidhamu ya uwajibikaji ndani ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, wenzetu wametueleze lakini mimi si Mwanasheria, mimi ni mtaalam wa masuala ya fedha na uchumi, hivi unaposema kwamba *the contract was void abi-initio,* wewe Mheshimiwa Spika ni Mwanasheria, *was void abi-initio* kwa maana ya kwamba mkataba uliofanyika kati ya *Richmond* na Tanzania ulikuwa ni mkataba hewa ambao hau-*stay*. Nchi inaingia mkataba na kampuni ambayo haipo, hivi kweli bado tunachelea kuzidi kuwaangalia watu wa *Dowans*? Ninashauri kwamba ni lazima huu mkataba tuusitishe mara moja na kuwatua mzigo Watanzania, hatuishii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kidogo nimesikitika sana, kuna baadhi ya Watanzania wenzangu katika kutoa mawazo katika vyombo vya habari na hata baadhi ya viongozi wastaafu, wanasema kwamba fulani kaonewa, hivi kweli wewe kiongozi mstaafu ambaye unapambana na rushwa, unajali maslahi ya nchi hii, umeona kabisa kwamba baadhi ya watu wamekiuka maadili ya utumishi wao, wamekiuka maadili ya utendaji kazi wao, leo unasema wameonewa, mimi sielewi kama kweli tunajenga Taifa la uwajibikaji. Sawa ni uhuru wa kila mmoja kutoa mawazo yake, mimi sipingi wala siwezi kusema kwamba napingana nao, lakini tunapotoa mawazo tuangalie sasa hivi Taifa liko katika hali gani, tunapambana na rushwa, tunapambana na mafisadi, leo unasema hawa mafisadi wameonewa, wataonewaje? *We need a joint effort,* hili suala siyo dogo, ni suala tete lazima Watanzania tushikamane na tusioneane aibu. Ikifika kama ni ukweli, sema ukweli, *call a spade a spade,* ukianza kusema unajua hii, inakuwa hii, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumekuwa tukisema kwamba hili Bunge linawakilisha wananchi ikifika kwa suala la mikataba wanasema unajua mikataba ni siri

lakini baada ya muda kwenye mtandao unaikuta, sasa siri iko wapi? Kama kweli mikataba ni kwa maslahi ya Watanzania ambao tunawawakilisha hapa, kuna haja gani ya kusema kwamba hatuwezi kuiona mikataba? Nafikiri *this is the public document*, ni vema Watanzania waweze ku-*challenge*, waweze kuona na waweze kuchangia ufanisi wa mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, tunalipa gharama kubwa sana halafu wenzetu, samahani sana mimi siyo mtu wa kusema kwamba nabagua au nafanyaje, bado kuna *class* ya watu wao wanakuwa na *force* kubwa sana ya kucheza na hii mali ya umma kama wanacheza na karatasi tu, naomba yeyote aliyetajwa kwenye ripoti hii, tumwajibishe bila kujali ni nani.

Mheshimiwa Spika, unajua katika suala la kuthibitisha au la vielelezo, unapokuwa una-*investigate* kesi yoyote unafanya *investigation* unaweza ukataka ushahidi wa mdomo au ukapata vielelezo ambavyo vinakutosheleza wewe kujiridhisha na uchunguzi wako unaofanya. Sielewi kwa nini wenzetu wanakimbia kusema kwamba hapana mtu fulani hakutendewa haki au fulani hakufanyiwa hivi kwa sababu hakupewa nafasi labda ya kujieleza, nafikiri huko tuondoke, tuangalie kwamba misingi mizima ya ripoti hii ilikuwa imelenga kusema mambo gani, imeainisha mambo gani ambayo ni ya msingi kwa ajili ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, namheshimu sana aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, ni mchapa kazi, ana rekodi ya kibinadamu lakini kama kuna upungufu, ni changamoto, sidhani kama yeye moja kwa moja amehusika katika masuala yote haya lakini kama kuna namna yoyote ambayo amehusika, basi ni vema tuangalie taratibu za kumwajibisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tufike mahali tuanze kuogopa, Mwalimu Nyerere alisema: "ukimuona mla rushwa, muogope kama ugonjwa wa ukoma". Sasa ugonjwa ukiulea, utakatika mikono, utakatika na viganja vya miguu. Sasa masuala haya mimi nashauri kwa kweli tuna haja ya kubadilika.

Mheshimiwa Spika, lingine nadhani imefika muda wa Bunge hili kupewa nafasi ya kuwathibitisha baadhi ya watendaji wateule mbalimbali ndani ya taasisi zetu. Kwa sababu inaonekana bado *system* yote iko *float*, anaweza akapewa mtu kumbe ni jambazi, kumbe ni fisadi, linakabidhiwa kwenye bucha, wewe fisi umkabidhi bucha, unategemea nini? Sasa lazima tufike mahali hawa watu waingie hapo, tuwathibitishe hapa kama taasisi muhimu ya wananchi, itasaidia sana kuondoa tatizo hili kwa sababu tunawafahamu na kuna kumbukumbu nyingine nyingi tu ambazo zinatumika kutaka kuwathibitisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako limefanya kazi kubwa sana na wewe mwenyewe umefanya kazi ya kijasiri kwa sababu kama ungekuwa unapiga *mark time*, mimi nilishasema kwamba hii ripoti ungejaribu kuifichaficha kidogo, tungekuwajibisha wewe kwanza, maana wewe ni *size* yetu, kwa hiyo, ungejaribu kucheleachelea kidogo, tungekuwajibisha kwanza wewe. Tufikie mahali huu uwazi wako na kiwango chako cha uwajibikaji iwe ni mfano kwa taasisi zingine. Leo hii Mbunge anatembea anaona

heshima ya Bunge inaanza kurudi kwa sababu tumeweza kuyasema yale ambayo yalikuwa hayasemwi. Nashangaa sana wenzetu kidogo wa upande wa pili, wao walikuwa wanawahi sana kwenda kwenye majukwaa, wakisikia kitu, kwenye majukwaa, sisi hatupiti kwenye majukwaa, lakini huu umaarufu ni wa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sijui na wewe niseme unatafuta umaarufu maana unataka kumwondoa Spika! *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala huu muhimu sana wa Ripoti ya Kamati Teule ya Bunge kuhusiana na mkataba wa kampuni ya umeme ya *Richmond.*

Kabla ya yote, napenda kwanza kutoa shukrani zangu za dhati kabisa na kuipongeza Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji chini ya Uenyekiti wa Mzee Shellukindo kwa sababu ni kutokana na taarifa ya Kamati hii katika Bunge ndiyo ambayo ilipelekea Kamati Teule kuweza kuundwa.

Vilevile kuundwa kwa Kamati Teule na uwasilishwaji wa ripoti na mjadala unaoendelea, ni juhudi za Bunge letu Tukufu kufanya *reform* za ndani. Kwa hali hiyo, basi napenda nikushukuru na kukupongeza kwa kuendesha juhudi hizi za mabadiliko ambayo leo Wabunge tunaweza tukasimama imara kabisa, tunachukua nafasi yetu Kikatiba kama jinsi ambavyo ilivyo katika vipengele vya Katiba.

Mheshimiwa Spika, pili, watu wengine wamevipongeza lakini na mimi ni vizuri pia niweze kuvipongeza vyombo vya habari vyote, Wahariri wa vyombo vya habari kwa sababu suala hili la mkataba wa *Richmond* walilishikia bango sana. Bila vyombo vya habari, ni rahisi sana wananchi kusahau kwa sababu kuna *scandal* nyingi sana ambazo zinapita, vyombo vya habari vikisahau na wananchi wanasahau. Lakini katika hili kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge ya Biashara na Uwekezaji suala hili mpaka limeweza kufikia hapa tulipo, ni heshima kubwa sana kwa vyombo vyetu vya habari. Waziri mpya wa Habari ambaye ni Naibu Katibu Mkuu mwenzangu, huyo ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na mimi ni Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, napenda nimuombe kwamba aangalie uwezekano wa kuviwezesha zaidi vyombo vya habari kupitia programu yetu ile ya *Parliamentary Pros-corps* ili tuweze kuwaimarisha zaidi Waandishi wa Habari wa vyombo vya binafsi na wale wa upande wa Serikali ambao wanaandikia habari za Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati ni sekta nyeti sana katika uchumi wa Taifa na inasikitisha kuona kwamba baadhi ya wenzetu walitumia nafasi ya matatizo katika sekta ya nishati, kujinufaisha wao wenyewe. Ni sekta ambayo ikichezewa, ina madhara makubwa sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kuangalia wakati ule mwaka 2006 kutokana na tatizo la umeme lililokuwepo, uchumi wetu uliathirika namna gani. Utakumbuka mwaka 2006 tumeshindwa kufikia *target* yetu ya ukuaji wa uchumi na

sababu kubwa sana ilikuwa ni *energy crisis*, ni umeme. Sekta ndogo ya umeme peke yake kwa mwaka 2006 ilikua kwa -2.5 na ilisababisha sekta ya maji nayo pia i-*shrink* kwa -1.8. Madhara yake kwenye sekta nyingine za uchumi kwa mfano ilisababisha sekta ya kilimo isikue kwa 1%, ilisababisha sekta ya viwanda isikue kwa 0.4%, ilisababisha sekta yenyewe ya umeme na maji isikue kwa 7.8%. Ukifanya *simulation* ya matatizo hayo yaliyotokea na matatizo yaliyotokea kwenye hizo sekta ambazo nimezitaja miongoni mwa sekta tisa za kiuchumi ambazo tunazo katika uchumi wetu, tulishangaa uchumi ulipoteza jumla ya shilingi bilioni 128 kwa sababu tu ya tatizo la sekta ya nishati. Sekta hii wanaita ni *strategic* sekta kwa hiyo ni lazima tuamue na isitokee tena watu ku-*take advantage* kujaribu kuchukua nafasi ya *crisis* ambazo nchi inapata kujinufaisha kwa sababu madhara ambayo tuliyapata katika uchumi yalikuwa ni makubwa sana. Kwa hiyo, naomba suala hili lisitokee tena na ripoti hii imeonyesha dhahiri kabisa uchambuzi mbovu wa mikataba mbalimbali na kuomba Serikali ihakikishe suala kama hili halitokei tena katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Kamati Teule inapendekeza, katika pendekezo lake namba mbili kwamba Mamlaka ya Manunuzi ipewe meno, iimarishwe na iwekwe chini ya ofisi ya Rais, nakubaliana kabisa kwamba Mamlaka ya Manunuzi ya Umma ipewe meno, nakubaliana kabisa kwamba Sheria iliyotungwa kwa ajili ya Mamlaka ya Manunuzi ya Umma, iimarishwe ili mamlaka hii isiwe inatoa ushauri tu lakini pia iweze kuchukua hatua lakini sikubaliani na maoni ya Kamati kwamba iwekwe chini ya ofisi ya Rais kwa sababu hatuwezi kuweka kila kitu chini ya ofisi Rais. Tukiimarisha mamlaka hii ikawa na nguvu ya Kisheria, hapatakuwa na sababu ya kuiweka chini ya ofisi ya Rais. Ni kiasi cha kuiwekea watendaji wazuri, wazalendo, wenye kujua kazi yao na wataweza kuhakikisha kwamba wanatenda kazi zao vizuri na kuhakikisha kwamba manunuzi yetu yanafuata taratibu ili tuondokane na mtindo wa kutaka kila kitu kiwekwe chini ya ofisi ya Rais. Ofisi ya Rais itakuwa na mambo mengi sana na tutashindwa kusimamia vitu vingine kwa sababu tutasema hii iko chini ya ofisi ya Rais, utamwajibisha vipi Rais!

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi la kuangalia ni kwamba sasa hivi kuna mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya *Controller and Auditor General* ili kumuweka *Controller and Auditor General* chini ya mamlaka ya Bunge na kuripoti moja kwa moja kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Tunaweza tukaamua kwa makusudi kabisa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma iweze kuangaliwa na Kamati Maalum ya Bunge na hapa ninapendekeza Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge kwa sababu sasa hivi mamlaka hii kwa hesabu zake inaripoti kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi. Lakini tunaweza tukaangalia ni jinsi gani ambavyo tutafanya mabadiliko ya Sheria hii ili Mamlaka ya Manunuzi ya Umma iwe inatoa ripoti yake kama anavyotoa *Controller and Auditor General* lakini sio kwenye *PAC* bali kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge ili Bunge liweze kuijadili kama ambavyo tunaweza tukajadili taarifa ya *CAG* na kupendekeza hatua za kuchukuliwa kwa watu ambao wanaenda kinyume na Kanuni za Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo napenda kuchangia ni katika *recommendation* namba tatu ya Kamati ambapo imependekeza kwamba mikataba ya umeme ipitiwe upya, naunga mkono kabisa kwamba mikataba ya umeme ipitiwe lakini tayari mkataba wa

*Richmond* umeshapitiwa na umeonekana kwamba ulikuwa ni mkataba wa kitapeli, ni mkataba ambao kimsingi au kisheria, hakukidhi haja.

Kwa hiyo, katika yale mapendekezo ya Kamati, napendekeza Kamati iseme wazi kabisa bila kumung'unya maneno kwamba mkataba wa *Richmond* uvunjwe na mikataba mingine ambayo haijapitiwa ndiyo ifanyiwe mapitio. Katika hili, tunaomba *commitment* ya Serikali kwa sababu mara zote imekuwa ikiahidi humu Bungeni kuyafanyia kazi mambo kadha wa kadha lakini hayafanyiwi kazi na wala hatuletewi ripoti. Katika hili, tunaomba wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge atakapokuja kuzungumza atoe *commitment* ya Serikali kwamba Serikali itafanya mapitio ya mikataba yote ya umeme ambayo Taifa letu limeingia ili tuweze kuona ni jinsi gani ambavyo tutaondokana na gharama ambazo zinatupata sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, la nne, ni kuhusiana na TAKUKURU, wenzangu wengi wamezungumzia TAKUKURU na nisingependa kurudia yale ambayo wameyazungumzia lakini nilikuwa naomba tufikirie uwezekano wa kuanzisha *serious fraud office*. Hivi sasa TAKUKURU inashughulikia kila aina ya rushwa katika nchi, kwa hiyo, unakuta hawana uwezo, hawana maarifa ya kushughulikia zile rushwa kubwa ambazo wakati mwingine zinakuwa ni ngumu sana kuweza kuzifuatilia na wakati mwingine wanakuwa hawana utaalamu wa kutosha wa kuweza kuzifuatilia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza tuangalie uwezekano wa kuwa na *unit* maalum kabisa ya kushughulikia rushwa kubwa. Nchi zingine wanayo *serious fraud office* na inakuwa inashughulikia rushwa kubwa kubwa tu na kutoa taarifa pale ambapo inahitajika kwa haraka badala ya kutegemea TAKUKURU hiyo hiyo iende kumkamata Mkurugenzi wa Halmashauri, hiyo hiyo imkamate Diwani, hiyo hiyo imkamate sijui *DO* wa kwenye Halmashauri ya wapi, tuwe na *serious fraud office* i-*deal* na rushwa kubwa kubwa na kutoa taarifa yake katika Kamati zinazohusika ama za Bunge au kwa Rais na hatua ziweze kuchukuliwa kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tano ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la maadili ya viongozi. Kamati imetoa mapendekezo yake kuhusiana na suala la maadili ya viongozi kuhusiana na suala la kutenganisha biashara na siasa na Mheshimiwa Rais amelizungumzia hili pia ni sisi tu ndiyo ambao tumechelewa ambapo viongozi wenye ofisi za umma hawawezi kujitofautisha na biashara zao. Kauli hii aliyoitoa Rais kwenye hotuba yake ya mwisho wa mwezi na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa inabidi iwe *clear*, haina maana kwamba inazuiliwa wanasiasa kufanya biashara lakini inaweka utaratibu maalum ya kwamba unapokuwa unafanya biashara uweke biashara hizo kwenye *blind chart*, ziendeshwe na watu wengine, utakapomaliza shughuli zako za umma unaweza ukarudi kwenye hiyo. Kwa hiyo, nadhani pendekezo hili la Kamati lifanyiwe kazi na Serikali kwa haraka sana kwa kuleta Muswada wa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Uongozi wa Umma ili tuweze kuona ni jinsi gani tutaweza kwenda mbele katika kutenganisha *interest* za kibiashara na *interest* za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, la sita, ni kuhusu usiri wa mikataba. Leo asubuhi Waziri wa Nishati na Madini, amezungumzia kuhusu taratibu za kufuata ili kupata mikataba. Ukweli

ni kwamba mikataba kuwa siri *is just a miss*. Mikataba sio siri, hakuna kipengele chochote cha mikataba hiyo kinachofanya mikataba kuwa siri. Kwa mfano sisi kwenye Kamati ya Madini tumepewa mikataba yote na Kamati hii haiendani na *Commission of Enquiry Act*, Kamati hii ni Kamati tu ya Rais, tumepewa mikataba yote bila kiapo, bila kitu chochote, iweje leo Bunge linapotaka mikataba linyimwe? Hiyo *is simply a miss*! Nataka kuwaambia Wabunge hakuna mkataba ulio siri, ni jukumu letu sisi kama Wabunge kupitia Kamati zetu za Bunge kufanya kama wenzetu Kamati ya Uwekezaji walivyofanya, kuhakikisha kwamba mikataba hii wanaipata kwa kutumia Sheria Na.3 ambayo inatoa mamlaka na *powers* kwa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, leo asubuhi amesema, hakuna suala la utaratibu wa kupata mikataba, hakuna *clause* hata moja ya usiri kwenye mikataba hii, tumekuwa tukiambiwa na Mawaziri kwamba ni siri, si siri, si kweli na Bunge na Wabunge wana uwezo wa kupata hii mikataba, tuache uwoga tu wa kuipata hiyo mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, amelizungumzia kidogo Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, ni suala ambalo pia Waziri Mkuu aliyemaliza muda wake, amelizungumzia na Kamati pia ilitoa majibu yake. Ningependa Kamati na Mwenyekiti wa Kamati kwa sababu ni Mwanasheria, atufafanulie vizuri zaidi suala zima lililozungumzwa la *Natural Justice*, haki ya mtu kusikilizwa. Kwa sababu nilikuwa naelezwa na Mwanasheria mmoja ambaye ni Mbunge ya kwamba suala la haki ya kusikilizwa linafikia pale ambapo sasa Bunge linataka kufanya maamuzi siyo kwenye Kamati ambayo yenyewe imetumwa kwenda kuchunguza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda Mwenyekiti wa Kamati aje atufafanulie vizuri zaidi vinginevyo tutaingia kwenye matatizo. Tunaweza tukatoa *loophole* ya mtu kuweza kujitetea kwa sababu tu hakusikilizwa. Kwa hiyo, ni vizuri kama kuna nafasi ambayo Bunge itapata kwa ajili ya mtu chini ya kiapo kuweza kuelezea *involvement* yake, aweze kuelezea.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, tumesikia suala la *Richmond* na yaliyotokea yanaanza kuchukua *angle* za kisiasa. Nadhani hatutaifanyia *justice* nchi hii kwamba Wapinzani tunataka kusema kwamba hili ni suala letu, CCM watake kusema kwamba hili suala lao, *this is wrong!* Hili ni suala la Kitaifa, wote hapa tume-*play role* moja tu ya kuhakikisha kwamba tunalitetea Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tumeshtushwa kidogo na maneno ya Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi aliposema kwamba kutakuwa na maandamo kuipongeza nchi, sioni sababu yoyote ya kupongeza chochote, sioni sababu yoyote ya kufanya maandamano, suala hili liishie Bungeni, Bunge limefanya kazi yake bila kujali itikadi za kisiasa, liishie hapa. Kama kuna Viongozi wa Vyama vya Siasa ambao kwa njia moja au nyingine wanaonekana wameliingizia hasara Taifa, tunaomba vyama vyao viwachukulie hatua. Kuna watu wana mamlaka kwenye vyama vyao, vyama vyao viwachukulie hatua lakini tusiligeuze suala hili kuwa ni suala la kisiasa, suala hili ni la Kitaifa, hakuna sababu ya Chama chochote cha siasa ku-*take credit*, hakuna sababu ya Wabunge kuanza

kurushiana vijembe vya kisiasa kutafuta mambo ya umaarufu na kadhalika, hakuna mtu atakayekuwa maarufu hapa, umaarufu ni wa Tanzania peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mapendekezo ya Kamati pamoja na hayo marekebisho ambayo nimeyatoa ambayo ninaamini Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wataweza kuyaelezea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, atafuatiwa na Mheshimiwa John Paul Lwanji wakati huo Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe ajiandae.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kidogo suala ambalo liko mbele yetu lakini mimi nitazungumza katika mfumo wa maswali, ndiko nitakakojikita zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono Taarifa hii ya Kamati Teule lakini mfumo wangu wa maswali ambao nitauzungumzia, unaanza na swali lifuatalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala ambalo tunalizungumzia hapa ni suala la hujuma. Taarifa imetolewa kwamba ni hujuma ambayo imefanyiwa Serikali. Sasa tuchukue mfano, hivi kosa likitokea, Polisi wamepelekewa malalamiko kwamba kuna kosa fulani limefanyika na mtu aliyefanya lile kosa ni fulani, nafikiri hatua ambayo wanaichukua ni kumchukua yule mtu na kumweka mahali halafu anakuwa anasaidia Polisi, kusaidia Polisi maana yake ni kwamba anasaidia wakati uchunguzi unaendelea. Sasa hili ambalo tunalisema hapa ambalo nafikiri imeshathibitishwa kwamba kuna hujuma imefanywa, wako wapi hawa watu? Hivi hivyo vyombo vya ulinzi na usalama, bado havijathibitisha kweli ili waweke wale watu mahali, wapumzike wakati uchunguzi unafanyika ili waisaidie Polisi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kwa kweli hiyo hujuma imenihusu sana mimi, imenibana sana katika Jimbo langu. Nimekuwa nikiomba hapa umeme, miundombinu yote imetengenezwa lakini kila nikiomba naambiwa bado tunatafuta fedha, kumbe fedha zilikuwa zinaenda sehemu nyingine kwenye *Richmond*. Ndugu zangu wamehangaika mpaka kununua transifoma tumeshindwa! Sasa leo hii hujuma hiyo ambayo imewafanya Watanzania waendelee kuhangaika, tunasema kwamba hapana waende halafu uchunguzi uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, katika taarifa iliyotolewa na Kamati Teule, imeelezea habari ya *Richmond*, sasa kitu ambacho mimi ninawauliza Wanakamati, hivi *Richmond* huyu ambaye makao yake ni huko *Texas* hapa Tanzania hakuwa na wawakilishi? Kwa sababu kwenye taarifa ile wamewaandika watu wawili Naeem pamoja na Mheshimiwa Wakili maarufu sana Ringo Tenga. Bwana Ringo ametajwa kwamba

ndio Katibu wa *Richmond*, hivi alikuwa peke yake, hakukuwa na watu wengine? Mimi nina imani kabisa kwamba Kamati bila shaka iliwaona maana ilikuwa ni moja kwa moja kwenda kumuuliza huyu Ringo, huyu Ringo ni Mtanzania, kulikuwa na ugumu gani wa kumuuliza mlikuwa wangapi katika hiyo *Richmond*? Hilo ni swali mojawapo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kuna *Dowans*, tumeelezwa hawa *Dowans Holdings* ndio ambao walikabidhiwa kwa mara ya pili, ni watu gani hawa, tusije tukawa na *Richmond* nyingine ya pili? Kamati kweli imeshindwa angalau kututajia tu kwamba hawa kina *Dowans* hawa ni fulani, fulani na fulani? Nafikiri kuna nafasi nzuri tu ya Kamati kutuelezea hawa kina *Dowans* ni watu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala lingine limeshazungumzwa linahusu Watanzania wenzetu na wengine ni Waheshimiwa Daniel Yona na Mheshimiwa Rostam Azizi kukaidi ile amri ya Bunge. Sasa hawa ni Watanzania, tumeshindwa kweli kuwaleta kwenye meza kuwauliza kwa nini mmekaidi, kitu gani ambacho kimezuia? Naomba Kamati ituelezee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la mwisho, maana kama nilivyosema mazungumzo yangu yatakuwa katika mfumo wa maswali, najaribu kujiuliza yale maadili ya kuwapata viongozi kama kweli bado tunayazingatia. Nafahamu kabisa kwamba kuna ile hatua ya *vetting,* sasa *vetting* iko katika hatua tatu. Mtu Serikali imekwishamu-*earmark* kwamba huyu tungependa awe kiongozi katika sehemu fulani, kutokana na maadili yenyewe, hawawezi wakamchukua huyo mtu mpaka wamfanyie *vetting.* Akishathibitishwa kwamba huyu mtu hana matatizo basi taarifa inapelekwa kule halafu anachukuliwa akishakuwa *cleared*, hiyo ni moja.

Mheshimiwa Spika, lakini ya pili, ni ile *partial vetting. Partial vetting* ndio ile ya haraka haraka ya kusema hapana hapa panatakiwa kiongozi, lazima tumpate, basi inafanywa ya haraka haraka, anachukuliwa yule mtu lakini bado kuna ya mwisho au ya tatu ambayo ni *extended vetting,* yumo mle ndani, anafanya kazi, ni kiongozi lakini bado kumbukumbu zinaendelea kutafutwa je, huyu mtu kweli ni msafi?

Mheshimiwa Spika, sasa vitu gani vinavyotafutwa? Vinatafutwa vitu vichache kabisa lakini vyenye maana kubwa sana katika uongozi. Kwa mfano kuna wengine wanaamini kwamba ukiwa Mbunge basi unakuwa na nafasi nzuri sana ya kuweza kujipanua zaidi katika shughuli zako za binafsi. Sasa hizo dalili zinaweza zikaonekana maana nia hiyo inaweza ikaonekana katika ile *vetting* siyo hivi hivi na akishajulikana kwa sababu sisi imani yetu ni kwamba tuwe na mtu *clean* basi ripoti zitakuja, zitaeleza huyu mtu pamoja na kwamba anataka Ubunge lakini matatizo yake ni moja, mbili, tatu, huyu nia yake ni kwenda pale ili kusudi awe na nafasi ya kujipanua zaidi, akishaonekana hivyo, hawezi kuchukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri yale maadili ya kumpata kiongozi yakizingatiwa, tunaweza tukawapata viongozi wazuri sana kama kweli tutazingatia ule utaratibu wa kumpata kiongozi ambaye ni sahihi katika uongozi wa kisiasa, katika uongozi wa Serikali au wa Mashirika na hii ilikuwa inafanyika na tunavyo vyombo vya

kufanya shughuli hiyo kwa nini tusivitumie? Tuvipe uwezo vyombo hivyo ili vikatufanyia kazi hii, tunaweza tukaondokana na matatizo ya kuwa na viongozi ambao ndio hawa ambao tunawasemasema sijui nini, sijui nini na vitu kama hivyo. Nafikiri tukumbushane tu kwa kuzingatia huo utaratibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, wananchi wangu wa Jimbo la Songwe, kwa kweli wamefadhaishwa sana na tukio hili, hawakujua, wao walikuwa wana imani tu kwamba kweli Serikali haina fedha za kuweza kuwahudumia, walipojua kwamba fedha zilikuwepo zilikuwa zinaingia mifukoni mwa watu, kweli kabisa wamefadhaika sana. Kwa hiyo, kwa niaba yao pamoja na pongezi zote za Kamati lakini wangependa sana hatua kali zichukuliwe dhidi ya hawa wenzetu ambao wanatuhujumu kwa kuwekwa kwanza sehemu fulani ili waisaidie Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda. Ni zamu sasa ya Mheshimiwa John Paul Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe na ajiandae Mheshimiwa Castor Ligallama.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote, niipongeze kwa dhati kabisa Kamati hii kwa ripoti yake nzuri na yenye ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze na wewe pia kwa ujasiri wako wa kuteua Kamati hii. Si suala dogo, ni suala nyeti na kwa kweli ulihitaji ujasiri wa aina ya pekee kuweza kutoa uamuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nikipongeze Chama changu kwa kutupa nafasi ya kuweza kuchangia juu ya suala hili. Najua tunapita wakati mgumu lakini Chama chetu nacho kikaona ni vema Wabunge wake waweze kutoa maoni kuhusu tatizo hili. Mimi nadhani ... *(Makofi)*

**SPIKA:** Umeruhusiwa na Spika siyo na Chama hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo lakini nadhani ni vizuri pia niweze kutoa pongezi hizo ambazo zimetufungulia njia maana watu wengine walikuwa wanashindwa kupumua vizuri. Sasa kama hilo limetokea, nadhani njia imekuwa wazi. Nilikuwa nina hofu *role* ya mtu kama Waziri Mkuu ambaye ni kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni halafu kwa wakati huo huo tukitoka hapa anakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wa Chama. Sasa bahati nzuri, tumepata Waziri Mkuu mwadilifu, kwa upande wangu ninavyoona, tumepata Waziri Mkuu mwadilifu na *role* hii akiitumia vizuri, basi tutaenda vizuri lakini kama mtu atapenda kuitumia vibaya ndio maana unasikia kuna watu wanalalamika kwamba bwana tunafungwa midomo au

tunafanywa hivi. Sasa hili tatizo si dogo ni tatizo kubwa na ambalo linahitaji kuangaliwa kwa uangalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kusema kwamba katika ripoti hiyo tuliona maamuzi yaliyotolewa katika Baraza la Mawaziri yalikiukwa na watu wachache wawili au watatu. Juzi wakati Mawaziri wanaapa, kuna kipengele kinachosema hivi:-

*"Ninaapa, nitakuwa mwadilifu kwa Rais na kwa vyovyote sitatoa siri za Baraza la Mawaziri".*

Mheshimiwa Spika, mimi ninaona hapo kuna upungufu mkubwa kwa sababu unaposema kwamba hutatoa siri na kweli hawakutoa siri lakini walikiuka na sisi umma huku hatujui siri za Baraza la Mawaziri, kwa hiyo, yale yaliyokuwa yanatakelezwa, inawezekana kabisa watu walikuwa wanaona ndio maamuzi ya Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwamba hati ya kiapo irekebishwe na tuseme kwamba:-

*"Nitakuwa mwadilifu na kwa vyovyote vile sitakiuka wala kwenda kinyume cha maamuzi ya Baraza la Mawaziri"*

Mheshimiwa Spika, maana kwenye kiapo wanachoapa wanaweza kupata *loophole* ya kwamba bwana ni kweli siri sikutoa, sasa iweje? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naona hii hati ya kiapo ina mapungufu mengi. Tuainishe bayana kabisa kwamba bwana kwa vyovyote vile sitakiuka wala sitakwenda kinyume, nadhani itakuwa *binding*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshtuka sana kwa sababu mimi kwa *professional* ni *Administrator* kwamba Baraza la Mawaziri likae sijui *implication* yake ni nini, Baraza la Mawaziri zima limekaa halafu watu wawili, watatu wanaondoka kwenda kufanya kinyume cha maamuzi yale! Maana yake ni kwamba Rais alikuwa hana tatizo, mwadilifu kwa nchi na ndiyo tuliyemchagua, sasa inapotokea tena kuna Baraza lingine la Mawaziri ndani ya Baraza la Mawaziri tulichagua ma-Rais wangapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hiyo ni *very serious implication*, si suala la mchezo. Mkiiangalia kwa ndani hata Kikatiba na nini, ni mbaya sana. Kumbe tumegundua Rais alikuwa mwadilifu, sehemu kubwa ya Baraza la Mawaziri lilikuwa waadilifu lakini kasoro kuna watu waliingia wakapinga maamuzi ya Baraza la Mawaziri. Sasa *consequences* zake ndiyo hiyo, kikatokea kizaazaa hapa, watu wengi wamesumbuliwa. Nadhani Serikali ingeangalia suala hili kwa mapana na marefu, kwa nini watu wachache wakiuke maamuzi ya Baraza la Mawaziri? Hii ni hatari sana kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani tulipoenda kupiga kura mwaka 2005 tulienda kwa wingi wetu kuchagua Rais mmoja wa nchi na ndiye aliyeunda Baraza la Mawaziri. Sasa kama maamuzi yametolewa kwenye Baraza la Mawaziri, kwa nini watokee watu wengine wakiuke? Hiki kitu siyo chepesi chepesi nadhani ni cha kuangalia kwa undani, *constitutionally*, nadhani kuna tatizo kubwa hapa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wangu wa Jimbo la Manyoni Magharibi, kwa kweli wamefadhaishwa sana, labda nitumie maneno ya mwenzangu hapa wamefadhaishwa sana. Nimetoka jana kule tuna maombi mengi ya masuala ya umeme kwamba usambazwe kutoka Itigi kwenda Kitopeni ambapo gharama yake ni Sh.26mil, kwenda Mgandu ni Sh.1.2bil lakini yale malipo yanayolipwa *Dowans* au *whichever Richmond* ya Sh.152mil kwa siku, sasa *can you imagine*, maana yake nini? Maana yake ni kwamba gharama ya kutoa umeme kutoka Itigi kwenda Kitopeni, ni ya robo siku. Mapato yao na uhitaji wa umeme kutoka Itigi kwenda Mgandu ambako kule unaweza kuhudumia vijiji zaidi ya 12 ambavyo viko barabarani vinasubiri umeme na ahadi hiyo ipo, ni malipo ya siku tano, ni wiki moja, ni Sh.1.2bil lakini umeme kutoka Itigi kwenda Gurundu pale ni Sh.300mil malipo ya siku mbili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nadhani wakati huu ni muafaka kabisa kuvunja huo mkataba ili tupate umeme. Kwa kweli mimi ni mmojawapo ambaye nimesimama mara nyingi kulaumu sana *TANESCO*. Naomba sana kama niliwakosea basi wanisamehe, kweli walikuwa na mzigo mkubwa sana na hasa watumishi wa Mashirika ya Umma au Serikali au watumishi wa aina yeyote wanapowaona ninyi ni wanasiasa halafu miongoni mwenu kuna wawili, watatu, wanaowachezea yaani wote wanaona sisi hapa ni zumbukuku kwamba wao walikuwa wanafahamu nini kinajiri sisi hatufahamu! Sasa unapopiga kelele, unapofanya nini, watu wanasema hivi hawa watu kwa nini wanatusumbua sisi?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tuwapongeze watu wa *TANESCO* walikuwa na mzigo mkubwa sana, nisingependa kutaja majina lakini wote wamekuwa waadilifu. Ukisoma ile ripoti kutoka mwanzo mpaka mwisho na sidhani kama tuna sababu yoyote ya kuwa na *accused finger against TANESCO*, walijitahidi na kama mnavyosema wote walikuwa watumishi wanaishi katika kivuli cha uoga katika kuwa jasiri, sasa tutawalau vipi kwa sababu utaratibu ndio huo na waliohusika ndio hao wenyewe ni watu wazito.

Mheshimiwa Spika, nadhani tuwapongeze *TANESCO* kwa msimamo wao waliofanya na ninaomba mkataba huo mara moja ikiwezekana uweze kusitishwa ili tuweze kupata umeme, nishati ambayo ni muhimu kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, nimeamini kwamba tunashindwa kuendelea kwa sababu ya watu wachache. Hii nchi tunashindwa kuendelea kwa sababu ya matendo ya watu wachache sana, tungekuwa mbali. Kuna watu wachache walim-*betray* Mwalimu kwenye suala la Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, basi kwa sababu ndio walikuwa wameshika madaraka makubwa basi imebidi iwe hivyo lakini ukweli ni kwamba ndio maamuzi ya kila mara kwamba tunapofikia maamuzi fulani hutokea watu wachache wakapinda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasisitiza kwamba mapendekezo haya ya Kamati yazingatiwe na kutekelezwa na ikiwezekana mapema sana na hili suala la kuvunja huu mkataba huu liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchezo huu inanikumbusha kwamba wakati watu wana dhiki wengine hufurahi, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa. Unajua inapofikia mtu anaamua kufanya biashara ya majeneza, kuna yule ambaye yuko *genuine* kutoa huduma kwa wenzake lakini nimeona filamu moja ya Nigeria, kuna bwana mmoja alikuwa anatengeneza majeneza mpaka anafika mochwari kwenda kujua leo wamekufa wangapi na mpaka kufikia hatua ya kuwahonga hata Wauguzi wawapige sindano au wawape dawa ile ya usingizi ya moja kwa moja yaani alikuwa anafurahia matatizo ya wenzake ili aweze kuuza majeneza kwa wingi. Kuna watu wa aina hiyo na ndivyo inavyoonekana kwa sababu wakati wa matatizo makubwa kama hayo nyinyi mnaleta mradi wa kufyonza, kwa kweli imetusikitisha sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba ripoti hii ifanyiwe kazi kwa kina ili tujikomboe. Nisingependa kutumia maneno ya mwanasiasa mmoja anayesema: “saa ya ukombozi ni sasa” lakini ukweli ni kwamba hii imekuwa dira, *it’s a very serious issue* inayoligusa Taifa na mtikisiko wake tumeuona.

Mheshimiwa Spika, ningeshangaa sana kama wenzetu walio katika *front page* wengi wangeondolewa kwa sababu kumbe wengine walikuwa waadilifu, sasa imeonekana kwamba ni watu wachache wanaoyumbisha nchi hii. Wengine wametajwa ni akina nani na akina nani, sasa bila kujali ni akina hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa ili tuweze kujikomboa na hakuna mtu atakayekuja kutuondolea matatizo yetu, ni sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa John Paul Lwanji, namwita sasa Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Magalle Shibuda, simuoni humu ilikuwa ndio afuatie.

Kabla Mheshimiwa Chacha Wangwe hujaongea, naomba kukupongeza tangu mkutano uliopita, umechaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha *CHADEMA*, hongera sana. Nikisema hivyo siyo kwamba ninamdharau jirani yangu, Mheshimiwa Said Arfi, wa Mpanda Kati lakini ni kutambua tu kwamba kura za Mheshimiwa Wangwe zilitosha, hongera sana na tunakutakia mema. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa pongezi hizo na pia ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumza machache katika hoja hii ambayo imekuwa ya kusisimua sana kwa wananchi wote wa Tanzania.

Pia napenda kukushukuru kwa kuwa Mheshimiwa Spika ambaye kweli unaongoza mabadiliko maana unapenda mabadiliko hata Kanuni zetu humu umezibadilisha ili ziweze kwenda na *standard and speed*. Kwa hiyo, nakuaminia sana na ninaamini kwa namna hii, Bunge hili linaweza likawa ni Bunge la kihistoria katika Tanzania ikiwa Waheshimiwa Wabunge kwa azma ambayo nimeiona wataamua kufanya kazi ya Kibunge badala ya kufanya kazi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha msingi ambacho kimetuweka hapa Bungeni, ni kiapo tulichokula, naona hata Waheshimiwa Mawaziri wapya walikula kiapo jana. Hiki kiapo ni kitu muhimu sana na tulipofika hapa Bungeni tulikula kiapo na kiapo tulichokula ni cha kulinda Katiba na kusimama katika ukweli na haki daima. Sikuona kiapo kingine pamoja na kwamba tumetokana na vyama lakini sikuona tunakula viapo vya vyama hapa, sisi tulikula viapo mbele ya Spika vya kulinda Katiba ya nchi. Sasa ni lini Katiba ya nchi itaanza kufanya kazi kwa sababu inaonekana kama Katiba ya nchi, ni kitu cha mchezo tu. Ni kweli hata sisi wa upande wa Upinzani tunasema mara kwa mara hata katika magazeti kwamba tunataka Katiba ibadilishwe, ni kweli kwa sababu tunaona kama ina mapungufu fulani lakini ile Katiba yenyewe iliyopo ina haki nyingi za msingi na maelekezo na wajibu wa msingi ambao hatuutekelezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapenda kujikita katika mapendekezo kama ulivyosema kwa sababu mengi yameshazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Ninapenda kusema kwamba hili suala la *Richmond* limejitokeza kwa sababu ya msimamo wa Mbunge wetu mmoja, Mheshimiwa William Shellukindo, ninapenda kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa William Shellukindo, ni Mbunge wa siku nyingi na ninakumbuka tulipokuwa katika semina kule Dar es Salaam alituelekeza jambo ambalo sijalisahau mpaka sasa. Alisema kuna Wabunge wa aina mbili. Kuna Mbunge ambaye ni *MP (Member of Parliament)* ikiwa na maana ya Mjumbe wa Bunge na kuna Mbunge ambaye ni *Parliamentarian* kwa Kiswahili nadhani ni Mwanabunge ambaye anawakilisha maslahi ya Taifa, Mheshimiwa William Shellukindo alituambia kwamba kuna hiyo tofauti. Kwa sababu *Member of Parliament*, yeye hawezi kuvuka kiwango cha Chama, daima yeye anajikita katika Chama lakini *Parliamentarian* anawakilisha wananchi na maslahi ya Taifa. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa William Shellukindo kwa kutoa hoja na baada ya kuangalia nikasema mmh, hapa, hapana hili suala lazima lichunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru sana Kamati ya Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kwa kuamua kuwa Wanabunge *(Parliamentarian)* wanaowakilisha wananchi. Kama wangezingatia maslahi ya Chama kwamba, je, katika kura za maoni nitachaguliwa tena kuwa Mbunge au hapana, pengine wasingeweza kutoa yale waliyoyatoa. Kwa hiyo, naamini huu ni mwanzo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, ninapenda kulaani ufisadi. Ufisadi ni kitu kibaya sana na siyo hapa tu lakini hata katika nchi nyingine, kitu ufisadi kimeleta madhara makubwa sana. Ninaamini sisi katika Tanzania ni sehemu ya Afrika Mashariki, tuna

Waziri anayewakilisha masuala ya Afrika Mashariki, pengine sitakosea sana kama nikitoa rambirambi zangu kwa watu ambao wamekufa kule Kenya kutokana na uchaguzi ulioharibiwa na mafisadi. Yale yaliyotokea kule ni mambo ya mafisadi kwa sababu mafisadi ndiyo wanaotoa rushwa kwenye uchaguzi halafu ndiyo wanaoiba kura halafu wakiona watu wanalalamik, wanachukua silaha wanawaua. Sasa huo mtindo tusingependa uwepo katika nchi yetu kwa sababu hali iliyopo kule Kenya ni ya kusikitisha. Mimi nikiwa Mbunge ambaye natoka Tarime, Jimbo ambalo linapakana na Kenya, kuna mambo ambayo ninayafahamu pengine Serikali isingependa tuseme lakini mimi ni mwakilishi wa wananchi nitayasema kama yataonekana hayana maana basi nitakosolewa.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu limejaa watu lakini Serikali haitaki kukiri kwamba kuna watu Tarime, kila mji una watu kumi au ishirini kwa sababu ni ndugu zetu. Kama Serikali haitaki basi tungependa tusaidiwe na Umoja wa Mataifa chakula, mavazi na madawa lakini Serikali haitaki tuseme kwamba wale Wakenya wapo pale, hiyo ni kazi ya mafisadi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kule Kenya kwenyewe kuna Watanzania kutoka hasa katika Jimbo langu la Tarime ambao walikuwa wanafanya kazi katika mashamba ya miwa na chai, wamekuwa *stranded* huko, wengine wamekufa, wengine wameuawa na wengine wamenyang'anywa mali zao lakini hatuwezi kusema kwa sababu tunatakiwa tuwe *neutral*. Lakini sisi kwa sababu tunafuata ukweli na haki, tunatetea demokrasia na haki, tunasema jamani muangalie sana hili suala la ufisadi litakuja kutufikisha mahali pabaya sana msione wananchi wa Tanzania wamenyamaza siyo kwamba ni wajinga, wanaistahi Serikali, kwa hiyo, Serikali bado ina nafasi ya kuweza kurekebisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, sassa nitazungumzia ufisadi katika mapana yake tusiangalie *Richmond* peke yake kwa sababu mtu anapokuwa na ugonjwa ndani ya damu, majipu yanatokea mengi tu mwilini, kuna jipu lingine linaitwa *Richmond*, lingine *BOT*, lingine *EPA* na lingine linaitwa Ndege ya Rais. Sasa ukipenda unaweza kwenda kwa *Chemistrian* akakupa dawa, ukapakapaka, yakapona siku hiyo na baada ya siku tatu yanatoka tena. Kumbe unatakiwa kwenda kwa Daktari, afanye *diagnosis,* apime ili aone ni *bacteria* gani wanaokusumbua halafu uvumilie apige sindamo halafu unapona.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tusifanye zile zinazoitwa *cosmetic changes* kwa sababu suala la Mheshimiwa Edward Lowassa kujiuzulu, ni kweli ni suala zuri lakini pia sidhani kila mtu atakayekuwa amepatikana hapa kwamba alishiriki katika ufisadi basi anaambiwa ajiuzulu halafu tunampongeza kwamba yeye ni shujaa. Sasa hivi bado hata *BOT* haijaja, kwa hiyo, ina maana Baraza la Mawaziri litabadilishwa kila mara inapobainika kwamba kuna ufisadi! Sasa suala la ufisadi ndiyo ambalo linatakiwa Bunge letu lilishughulikie na ili tulishughulikie suala hili inabidi tuangalie historia ya ufisadi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi hii wakati wa kipindi cha kwanza cha Mwalimu ndiyo tunaweza kulaumu wafanyabiashara kwa sababu kuna wafanyabiashara ambao si waadilifu, mabepari na wanyonyaji. Mwalimu alikuwa anapambana nao lakini siamini

kwamba wafanyabishara wote ni mafisadi kwa sababu historia yetu inaonyesha kabisa kwamba wafanyabiashara ndiyo waliomsaidia Mwalimu katika ukombozi wan chi hii! Kuna wafanyabiashara Wazee wetu akina Mzee Sykes, Mzee Rupia, Mzee Mbowe, Mzee Jamal na wengine wengi ambao walikuwa ni wafanyabiashara waadilifu hata ukikagua hesabu zao Mkoloni alikuwa anaona wako safi na waliweza kusimama kidete na wakasimamia ukweli. Kwa hiyo, wafanyabiashara vilevile wana *role* au wana sehemu ya kuchangia katika kupambana na ufisadi ili waendelee kufanya biashara vizuri na kwa amani au wanataka iwe kama Kenya?  Kwa hiyo, mfanyabiashara ambaye ana akili timamu lazima atasaidia kupambana na mafisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba tuangalie uadilifu wa mtu kwa sababu katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, wafanyabiashara hawakuwemo lakini ufisadi ulianzia pale, walipambana sana na Mwalimu mpaka akaja hata Sokoine mnafahmu vizuri hiyo historia. Walikuwa ni hawahawa akina sisi ambao hatuna biashara lakini tukipata mwanya huo wa kufanya ufisadi, tunaufanya. Kwa hiyo, naomba sana tuchukie ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili suala la ufisadi, ndugu zangu mimi naona hatujawa *serious* kwa sababu tumekuwa *Members of Parliament* ambao tunafikiri masuala ya vyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia kwamba Chama hakiwezi kukuleta Bungeni kama wananchi hawataki. Naamini kwamba wanaotuleta hapa ni wananchi ndiyo maana tunapoanza kuangalia suala la ufisad, tutaangalia kuanzia Serikalini, mpaka ndani ya vyama vyetu vilevile, viwe Tawala au Upinzani, tuangalie ufisadi ni nini. Katika hali hiyo, ninaomba Wabunge waache ile hali ya kuleta ushabiki hapa Bungeni na hili suala tusiliangalie kwamba ni umashuhuri wa Chama.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyoletwa hapa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, sisi tuliikataa, tukamfukuza hapa lakini Rais akaona alikuwa na hoja ya msingi, akaamua kuunda Kamati pembeni ya Bunge badala ya Kamati Teule ambayo sisi tulikuwa tunaitaka ambayo Zitto alikuwa anaitaka. Sasa unaona hii Kamati ya Dr. Harrison Mwakyembe, ambayo imetokea upande wa CCM, naona kidogo imeruhusiwa, umeona vile Kamati Teule inavyofanya kazi? Kumbe hata hili suala la madini lingekuja hapa kama Kamati Teule, tungeshafunga kazi tayari hapa lakini kwa sababu ya mambo ya Chama ikabidi hata Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, aende Mwembeyanga kuzungumza. Haya ndio mambo yanayokwamisha maendeleo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninamshauri Mheshimiwa Rais ikiwa Wabunge watakataa hoja zake, maana yeye aliona hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe ni ya msingi ndiyo maana akaamua kumuweka katika Tume nyingine aliyoiunda pembeni, kwa hiyo, inawezekana Rais ni muadilifu kabisa lakini tunamtatiza sisi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kipengele katika Ibara ya 90(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambacho kinasema:-

*"Kama Bunge limekataa kupitisha hoja ambayo ni ya msingi katika Sera za Serikali na Rais anaona kwamba njia ya kuendelea kutoka hapo ni, si kumteua Waziri Mkuu mwingine bali ni kuitisha uchaguzi mkuu"*

Mheshimiwa Spika, mimi niko tayari kwa sababu najua mimi ni msafi na kweli kama sisi ni wanaume na wanawake ambao tuko humu, tumruhusu Rais avunje hili Bunge, turudi kwa wananchi, wachague watu *fresh* ili waje kumaliza tatizo la ufisadi lakini vinginevyo sasa tufanye kazi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba hii Kamati ya Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe i-*extend* badala ya kuwa Kamati ya kuchunguza tu ipewe mamlaka ya kuwa kama Kamati ile iliyoundwa Afrika Kusini ya *Truth and Reconciliation* kwamba kuwe na mambo ya ukweli, haki na uwazi na maridhiano. Wewe kama ni fisadi, wewe njoo ukiri pale, uturudishie mali yetu, tunaweza kukusamehe lakini vinginevyo kama unabisha basi Mahakamani kisha Segerea, ndivyo Sheria zinavyosema.

Mheshimiwa Spika, ufisadi uko kila kona na ni nchi nzima na wanaowajua mafisadi ni wananchi kwa sababu mimi siamini kwamba Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alikuwa anajua kwamba Balali ana mashamba sehemu fulani! Wananchi wanajua na ndiyo wanaojua mafisadi! Kwa hiyo, tuwashirikishe wananchi kama *operation* moja kali kama ile iliyofanyika wakati wa Mwalimu Nyerere na Mheshimiwa Marehemu Sokoine. Watafutwe hao mafisadi mpaka vijijini, wapo, Mheshimiwa Mizengo Pinda ni shahidi yangu, ndani ya Halmashauri kuna mafisadi kibao ambao hawataki kutoka kule, kila siku wanaandikiwa hati chafu lakini tunataka sasa nguvu za kuwatoa mle na wawajibike kwa wizi wanaowafanyia wananchi kwa kuwakosesha barabara, shule, hospitali na hata maji. Sasa tumeona kumbe ilikuwa ni mchezo unachezwa watu wanasema jenga shule kwa nguvu, watu wananyang'anywa mali zao vijijini kumbe huku mabilioni yanachotwa, hiyo ndiyo Tanzania na wananchi wameng'amua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninaomba hili suala Bunge lilishughulikie kwa sababu hata juzi Bunge la Senate kule Marekani liliita watu pale waliokuwa wamekula madawa ya kulevya wakaja na wakakiri na sisi tuna uwezo kabisa wa kufanya kazi hiyo ya kuwaita hapa na kuwahoji badala ya kukaa hapa tukilalamika. Sisi tumepewa mamlaka na Katiba, hii Katiba itafanya kazi lini? Kwa sababu kama kweli sisi Wabunge ndiyo ambao tumekuwa hapa miaka miwili mizima tukizuia hoja za msingi, akisimama tu mtu hapa anataka kusema hoja ya msingi kama ni wa Upinzani, anapigiwa kelele anakaa chini, kama ni wa CCM, anaitishwa kwenye kikao pale, anakwenda kuhojiwa. Siku moja hapa amesema Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba unaitwa unakwenda unatishwa, sasa miaka miwili mizima tumeipoteza. Sasa siamini kama hii miaka mitatu kweli kuna mabadiliko ambayo tutayafanya kama siyo ni unafiki tulionao wa kutaka kutetea vyama vyetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mimi nilishangaa sana ile hotuba ya Mheshimiwa Anne Malecela, alisema mambo mazuri sana ya kusisimua wananchi lakini akaishia kusema haya ni kwa sababu ya kutaka kukisafisha Chama chetu na kukinusuru, sitaacha haya mambo yasemwe na Mheshimiwa Zitto Kabwe, ina maana gani hiyo

sentensi kwamba mtaendelea kutubagua hapa eeeh? Kwamba haya mambo mnayafanya kwa sababu mnaona CCM huko wananchi wameishtukia? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ninachosema ni kwamba wananchi wako macho kama tuna hiari ya kuwafanyia kazi tuwafanyie kazi lakini vinginevyo tusipoteze fedha za wananchi hapa na muda wao, turudi kule nyumbani, kijijini basi kama wanakuja wengine, waje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Castor R. Ligallama, atafuatiwa na Mheshimiwa Magalle John Shibuda na wakati huohuo Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary ajiandae.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mengi tumeongea kuhusu *Richmond* na wananchi wametusikia na kama tungekuwa vitani, tunafikia hatua sasa vita ya *Richmond*, itaisha kesho. Sasa kama ni vita na kipindi kile wanaita wenyewe wanajeshi ya ku-*reorganise* yaani pale mnaangalia Maaskari waliokufa, mnaangalia zana za kupigania na wapiganaji wenyewe ni Wabunge, tumepoteza makamanda watatu katika vita hii ya *Richmond*.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa zaidi kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri Mkuu jana katika mkutano pale CCM wa kujitathmini kutokana na hayo yaliyotokea. Sasa hivi wananchi wetu ni tofauti kidogo na miaka ya nyuma uelewa wao ni mkubwa sana. Siku ile kabla ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hajajiuzulu yaani siku moja kabla, sisi tulikuwa tunakutana kwenye Chama chetu usiku, baada ya mkutano nilikwenda kutafuta chakula, nikakuta wananchi wa Dodoma kutokana na hisia tu kwamba jambo hili wamelisikia, wao kwa uamuzi wao wakawa tayari wameshaweka hukumu, wanabandika makaratasi. Nikamwambia Mbunge mwenzangu baada ya muda tuje tuangalie wameandika nini.

Mheshimiwa Spika, yale maandishi yanafanana na hisia za watu wa Dar es Salaam waliokwenda kwenye shamba la Balali baada ya kusikia kwamba Sh.135bil ni huyu fisadi twende tukachukue shamba lake. Sasa na hapa Dodoma wakaamua kuandika na katika ile karatasi niliyosoma walisema hawa watu wa CCM wanakwenda kuongea ili watetee mafisadi na manyang'au, hela zetu wanaiba kila siku Sh.152mil. Kama tungeamua tofauti lakini Wabunge wako makini wote tukawa na msimamo mmoja, ingekuwa shida. Kwa hiyo, yale makaratasi yalienezwa mji huu kama ingekuwa ni suala tofauti na lile tuliloamua, kwa kweli katika mji huu wa Dodoma tungepigwa mawe. Nakala ya maandishi yale niliyaleta kwa Mheshimiwa Naibu Spika nafikiri Mheshimiwa Spika utakuwa umeyaona.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inajenga nini? Inajenga chuki, wananchi wanatafsiri maisha yao magumu lakini jawabu lao ni wizi unaofanyika, sasa tukienda hivi, siku moja tutaingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana nimeuliza maswali ya umeme hata siku moja Spika ulinitania nje ukasema, aaah, yaani wanakunyima umeme na wakati wewe ndiye unayezalisha umeme? Nina migodi miwili ya umeme Jimboni kwangu wa Kidatu na Kihansi, nimepigiwa simu na wananchi wangu wakiuliza hivi sisi tumekosa nini? Tukae gizani, hela ziliwe na umeme tukose?

Mheshimiwa Spik, mwaka jana tulimshika mtu anataka kuangusha ile nguzo kubwa ya kusafirisha umeme, anachimba ili kuiangusha tukaagiza Mtendaji wa Kata amtafute na wamemshtaki kwamba ni mhujumu uchumi. Lakini tafsiri ni kwamba kuna faida gani, nimetoka kwenye eneo ambalo ndiyo umeme unazalishwa lakini sisi tupo gizani, wenzetu waende wakaangaziwe huko? Nimeshazungumza hapa hata *on humanitarian grounds justification*, ni vema sisi tukose umeme kweli? Hilo moja.

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwenye gazeti la *This Day* la tarehe 11/2 mwezi huu, *topic* ilikuwa: **"***Now the Contravention Richmond Company resurfaces"* nikasoma aaah, ndani nikakuta ametajwa mtu mmoja ambaye ametajwa kwenye Kamati ya Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, ndugu Gire. Gire anasema kwamba mkataba tuliouweka sisi na *TANESCO* ni wa dola 83 milioni ambayo ni sawa na shilingi bilioni 98 siyo dola 172 milioni mnaotaja ninyi. Nikasoma tena mbele wametuma *fax* iliyokuja huku wanajitetea wanasema wao hawajawahi hata kumuona huyu Waziri Mkuu ambaye amejiuzulu, sasa nikajiuliza hizi fedha milioni 152 kama hawa wanasema hawajapokea hata senti tano kutoka Serikali ya Tanzania katika hilo gazeti sasa hizo hela milioni 152 analipwa nani? Jamani tunaweza kuwa na *Richmond* mbili, moja *genuine* na nyingine ndiyo inapokea hela. Sasa huyu ambaye anasema ameweka mkataba na *TANESCO* wa 83 milioni *US dollars* anakataa hajalipwa hata senti tano, sasa hizi milioni 152 zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapo tunaomba Kamati ifanye kazi ya ziada hapo, watu wanaochukua hizi hela ni watu gani? Wanajitambulisha kwamba wao wapo Houston Texas, hapa katika *continent* nne wameshafanya kazi kubwa sana na wanaamika lakini hawataji *continent* hizo walizofanya kazi ni zipi? *Fax* yenyewe hawakuisaini lakini hata mwandishi naye pamoja na kwamba alikuwa anaandika alikuwa anahoji uhalali wa hili. Lakini huyu mtu Gire anatajwa na mwingine anaitwa Haque. Sasa kama tunakuja ili tuweze kujisahihisha tuanze upya humu ndani kama alivyosema msemaji mmoja, vita hizi zitakuwa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulisema unaongea na Serikali ili *report ya Ernest & Young* ije, sasa hiyo ni vita nyingine. *EPA* tumepata *summary*, *it is another war*. Sasa kila wakati tutakuwa tunapoteza makamanda? Sasa kama ni hivi na umesema kabla ya Bunge hili halijaisha utakuwa umetuarifu kama Serikali inasemaje kuhusu suala la *report* ya *Ernest & Young* kuja kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la *BRELA*. Nimesoma katika vielelezo vya Tume Teule, hivi hii Wizara ya Viwanda, mimi ningeiomba kitu kimoja kwamba pamoja na kwamba *BRELA* ni *independent authority* yaani ni *authority* ambayo inajitegemea, sasa hivi haiko chini ya Wizara ya Viwanda *direct*, Wizara ya Viwanda ingekuwa na

*control* na yule bwana angekuwa analeta *returns* za makampuni yaliyosajiliwa *on weekly basis* ili kujua wale wenye makampuni ni akina nani. Kwa sababu hainiingii akilini mtu mmoja eti ananyofoa wale walioandikishwa kwanza kama kampuni ya *Richmond*, huyo ni Mwananchi huyo amesema, naomba kwa usalama jina langu lisiandikwe hapa mwanzoni, walifungua *Richmond* viongozi watano, anasema akiwemo Waziri Mkuu baadaye zikanyofolewa zile, wakawekwa watu wengine. Sasa huyu mtu anapewa nyumba Chang'ombe, Serikali ina *furnish* ile nyumba na kuifanyia ukarabati, si ajabu mpaka leo yule mtu yupo Chang'ombe, kweli ana *enjoy*. Mimi ninafikiri baada ya *report* hii yule mtu angeshachukuliwa na nyumba ile ikarudi kwetu Serikalini lakini si ajabu mpaka kesho yule mtu yupo. Naiomba Serikali ichunguze hilo, huyu mtu wa *BRELA* anakuwa na nguvu gani ya kunyofoa vitu hivi? Lakini tungekwenda ku-*control* kwenye Wizara na kupeleka *returns* za kampuni zilizofunguliwa na Ma–*director* wao, hata akinyofoa kule kwenye *BRELA* huku tunayo. Kwa hiyo, kuanzia sasa labda ingeanzishwa utaratibu huu wa kuweka *bank* au mahali fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nije baada ya maamuzi haya, unajua kwenye *science* unaweza kufanya *experiment* halafu mwishowe ndiyo ukasema by *inference* uka *conclude* kitu fulani, kwa hiyo, una *conclude by inference*. Mimi katika Jimbo langu nina shamba. Shamba hili nilikuwa nalima mpunga. Shamba la mpunga Serikali imeamua kwa makusudi tena imepitia kwa Baraza la Mawaziri kwamba lilime michikichi, inaniuma sana na wananchi wangu wote tumeumia lakini baada ya hii kesi ya Richmond, nimefanya *by inference* yanaweza kuwa maamuzi hayo ni ya ki-*Richmond Richmond*. Haiwezekani, mwekezaji anakuja anataka kulima michikichi, kwa nini usimpeleke Kigoma? Shamba la mpunga una-*return to* michikichi, uharibu ardhi ya mpunga kwa michikichi? Sera kwanza ya *biofuel* hatuna, hatuna sera ya *biofuel so far*, wewe unakwenda kuanzisha mambo ya *biofuel* wakati sera hatujapisha?

Mheshimiwa Spika, wananchi kwa kweli wa Tarafa yangu ya Mgeta wamesikitika sana na maamuzi ya Serikali na kwa bahati nzuri tumepata Katibu Mkuu mpya, naomba maamuzi haya yarejewe tupate mwekezaji wa mpunga ambaye tulishampata na akatuahidi vitu vingi na wananchi wanavijua. Ametuahidi umeme ambao Serikali imeshindwa kutupatia, ametuahidi miundombinu ya umwagiliaji, ametuahidi kutujengea Sekondari mpaka *High School*, ametuahidi kutujengea hospitali siyo kituo cha afya ni hospitali, ametuahidi kutuwekea na sisi watu tunaolizunguka lile shamba miundombinu ya umwagiliaji na Rais anasema Mkoa wa Morogoro uwe ghala la Taifa, mnapingana naye, unaweza kuweka michikichi *biofuel by the time* mnaanza kuvuna mnatengeneza mafuta ya *diesel* bei ya *diesel* duniani ikishuka, utafanya nini? Basi tupeleke kwenye fursa kule Kigoma tuwasaidie Kigoma kwanza wenzetu wanalima na wana uzoefu nalo tukiwaongezea sawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwamba tunataka shamba letu lilimwe mpunga, yule ametuahidi vitu vingi na mimi kweli baada ya kuangalia kwamba kwa nini Serikali ilishindwa kuona mpaka nikamuuliza ndugu yangu Ngasongwa, alikuwepo kwenye lile Baraza hajui lile shamba ameliona? *By*

*inference* nikasema *Richmond* hiyo! Sasa tunaomba tulime mpunga, tumuheshimu Rais wetu amesema Mkoa wa Morogoro uwe ghala la chakula lakini sasa kauli hii inapingwa kwa kuweka tena michikichi jamani! Wale wawekezaji walisema kwamba Mr. *MP you will forget about importing rice in this country, it is a big statement, forget about importing rice in this country* kwa sababu leo hii Dar es Salaam kula wali ni anasa kilo shilingi 800/= …

**SPIKA:** Mheshimiwa Ligallama rudi kwenye hoja tafadhali.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Aaaah! *Sorry* ni *Richmond* eeh! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nasisitiza hapa ni Taasisi hizi ambazo zinahusika na usajili wa makampuni ziwe makini.

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU, sitaki kuongelea mengi kwani wenzangu wamesema mengi, zijipange vizuri labda kama kuna tatizo katika Sheria yetu hii ya TAKUKURU basi tuirekebishe hapa. Kwa mfano, kama hii ya *BRELA* hakuna haja ya kuleta Sheria ni kuweka Kanuni tu, Waziri ana uwezo huo wa kuweka Kanuni kwamba lazima kampuni yoyote inayosajiliwa *returns* zake nizipate kila wiki na kujua ma-*Director* wako wangapi kwenye zile kampuni na TAKUKURU vilevile.

Mheshimiwa Spika, kuhusu yaliyotokea, kesho tutayajua mwisho wake na ningeomba Kamati ya Mheshimiwa Dr. Mwakyembe, tuishukuru kwani wamefanya kazi nzuri ambayo kwa kweli kama kuna makosa ni madogo ya kawaida ambayo hata fursa zipo kama kuhojiwa wanaweza kuitwa na wakahojiwa. Nafasi ipo tu ikawa *annexed* pale au kwenye Chama chetu wanaweza kufanya hivyo siyo lazima hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Ni zamu sasa ya Mheshimiwa Magalle John Shibuda na ajiandae Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia *agenda* hii ya Kamati Teule kuhusu Kampuni ya *Richmond.*

Mheshimiwa Spika, unapochangia hoja ambayo tayari imeshaanza kupata tiba, kwa kweli mchangiaji unakuwa na mtihani kuhusu maneno yapi uyatumie ya busara na hekima, kwa sababu unahitajika sasa uchangie jinsi gani Serikali mpya iliyopo madarakani, iweze kupokea hoja za kwenda kuboresha utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ninaomba kutambua kwamba, Chama cha Mapinduzi na Serikali zake, toka enzi za Uhuru na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, tumekuwa na utaratibu kama wa nyoka wa kuvua gamba la ngozi, ambayo unataka ujing'arishe upya. Ninaipongeza Serikali na Uongozi wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais wetu kuhakikisha kwamba, umechukua hatua za kuing'arisha upya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitapenda vilevile nitambue jambo moja kwamba, kuendelea na mjadala huu, imekuwa ni kheri kabisa na ni kwa maslahi ya nchi yetu. Ninakupongeza wewe kwa kuamuru kwamba, tuendelee na mjadala huu. Tusingeendelea na mjadala huu, pangeweza kuzuka mambo ya hisia ya kwamba, labda taarifa ya Tume hii ilikuwa inamlenga mtu kutokana na hali halisi ya uchangiaji jinsi ulivyoanza. Lakini hivi sasa minong'ono na mivumo haviwezi kuwepo, kwa sababu tumeendelea na uchangiaji kwa maslahi ya kuhakikisha kwamba, michango yetu inaboresha utekelezaji wa Serikali mpya, ambayo *birthday* yake tumeipata juzi baada ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kuapishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nijielekeze kwenye *agenda* iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, ninapenda kupongeza kwamba, Serikali yetu na Uongozi wa Taifa, umeweza kuonyesha dhahiri katika Tanzania, Kitaifa na Kimataifa kwamba, uongozi uliopo madarakani unaheshimu Katiba ya nchi. Hivyo, hili ni funzo kubwa kwamba, viongozi wote wawe wanaheshimu mamlaka ya Katiba ambazo zinaongoza nchi. Ninapongeza vilevile kwamba, haya yaliyotokea ni kisomo kwa maslahi ya maendeleo ya nchi yetu. Ninayapongeza mabadiliko yaliyotokea kwa amani na utulivu, chini ya busara za Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Vilevile ninapongeza sana kwamba, tumeweza kufaulu haya. Mwenyezi Mungu, amjalie Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania tuna deni la kuhakikisha kuwa, tunang'arisha Serikali yetu baada ya machafuko yaliyokuwa yamejitokeza na utaratibu ni ule ule wa kuhakikisha kwamba, Bunge tunawajibika kwa maslahi ya Taifa. Mimi siamini kama Bunge hili lina vita na mtu yeyote, bali tunatekeleza wajibu wetu kwa maslahi ya nchi, kwa mujibu wa Kanuni na Katiba ya nchi yetu, ambayo inatuwajibisha sisi Wabunge kuisaidia Serikali kung'ara. Kwa hiyo, hatuna vita na mtu yeyote; anapoguswa na mapungufu, basi aelewe ni katika utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kupongeza na kutambua uteuzi wa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda; ni mtu mstaarabu, muungwana, uwezo anao, nia anayo na yupo katika wito wa kulitumikia Taifa hili. Wahenga husema, huwezi kuwa Sheikh kama hukupitia Madrasa. Ninampongeza Mheshimiwa Pinda kwamba, yeye ni mwanachuoni aliyepitia mafunzo ya Hayati Baba wa Taifa katika ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, rudi kwenye hoja tafadhali. *(Kicheko)*

**MHE. MAGALLE J. SHIBUDA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa katika utangulizi wa kuboresha mchango, nitakapomimina. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwamba, nipo katika mrejeo wa hiyo hoja. Sasa ninaomba kujielekeza katika uchambuzi wa Kamati Teule ya Bunge. Ninaunga mkono, mapendekezo yote ya Kamati Teule ya Bunge. Dhamira ya mapendekezo ya Kamati Teule ni kwa maslahi ya kujenga nchi yetu, kwa hiyo, ninaiomba Serikali iyapokee kwa mantiki ya kwamba ni mchango wa kuboresha Utawala Bora na si kwa dhamira nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, uongozi wako wa Bunge una dhamira ya sisi Wabunge tuhakikishe tunatekeleza kwa viwango, wajibu wetu wa kuchangia na kuirekebisha Serikali kwa maslahi ya umma. Kama Bunge hili litakaa kimya, maana yake ni kwamba, watajitokeza watu wengine wa kuzungumza kwa niaba yetu. Viongozi wa madhehebu watajitokeza, Viongozi wa Dini wataanza kupiga kelele, wananchi watauliza Wabunge tunafanya nini? Kwa hiyo, ninaomba yote haya yaliyotokea, yapokelewe kwa dhamira njema.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, imejenga heshima ya Bunge, kwa hiyo, ninaipongeza sana na ninaomba matatizo yaliyozaliwa kutokana na upatikanaji wa kampuni ya *Richmond*, yashughulikiwe kikamilifu, utimilifu, ushujaa na kwa uhodari wa Serikali. Pamoja na mambo yote yaliyobainika katika ripoti yetu, hoja moja iliyobainika ni uvivu wa kufuatilia juhudi za viongozi walio chini.

Mheshimiwa Spika, kama kweli pangekuwa na juhudi za kufuatilia ninadhani leo hii tusingekuwa katika hii *Richmond.* Ninashauri Serikali iunde kanuni za kulinda wafanyakazi waliopo chini kwa sababu moja kubwa; boi hawezi kumchunguza bwana na mtwana, hewala ndiyo shukrani ya uhai wake. Kama hatuna kanuni za kuwalinda Watendaji, kwa mfano, Kamishna wa Madini aliyekuwa anayumba, akienda kwenye Bodi ya *TANESCO* anakubali, akija kwa Waziri anakubali. Hiyo imetuonyesha wazi kwamba, Serikali iwe na kanuni za kuwalinda watendaji ambao wana maarifa na taaluma mbalimbali ili wanapomshauri kiongozi ambaye ana kiburi cha madaraka cha kutaka kuitwa ndiyo mzee, athibitike na inapotokea awajibike yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati umefika, tuwalinde wataalam na ninashauri viongozi wote sasa tubadilike, tusitumie sifa ya mwenzetu au ya kuzoeana kuwa nayo ni viwango katika maamuzi yetu, hii ndiyo imetuweka mahali hapa. Ninaishauri Serikali kutokana na taarifa ya *Richmond* sasa tujisahihishe na tukubali kwamba, tuwaheshimu wanataaluma na sisi viongozi tubadilishe *mind sets* zetu kwamba, ukipewa madaraka siyo umemilikishwa mawazo, busara na hekima za watu unaowaongoza na usibinafsishe maarifa, juhudi na ujuzi wa mtu unayemwongoza. Tukubali uongozi wa pamoja, shirikishi na wa kuvuna mawazo hasa kutoka kwa watu walio chini yetu. Wahenga husema, huwezi kumchunga bwana kwa sababu wewe ni mtwana. Sasa kanuni zetu mpaka sasa ziliwekwa *in the clause of subordination,* baada ya mkoloni kuona kwamba, yeye ni mtu wa kutoa amri. Sasa ni vyema tupitie mambo yote ambayo hayaendani na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, dhamana zina raha na ulevi wake, kwa hiyo, ninaomba tukubali kwamba, mivumo iliyokuwa imetokea ilikuwa ni ya kuhatarisha umoja na mshikamano. Ninawapongeza Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, kwa kushirikiana na

Wabunge wa Vyama vya Upinzani na ninaona Wapinzani wanajifunza mengi ambayo Chama cha Mapinduzi, kinadhihirisha ustaarabu wake katika hadhara. *(Kicheko/ Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, kwa ujasiri na uongozi mahususi aliouonyesha baada ya Serikali kuwajibika. Waliowajibika, ninaomba kusema, kuvunjika kwa koleo siyo mwisho wa uhunzi. Kwa hiyo, ninapenda kusema kila jambo lina wakati wake, ninawaombeni ndugu zangu wote mliowajibika, mkubali kwamba, kufa ni kufaana na hivyo tushirikiane kwa dhati kabisa na Serikali mpya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, duniani hakuna mtu anayejua mambo yote. Ninaomba kusema kwamba, iwapo taarifa ya Kamati Teule itakuwa na mapungufu, basi ichukuliwe mantiki na dhamira ya ripoti hiyo ilikuwa ni kupiga vita unyonyaji. Kwa hiyo, ninaomba Serikali kwa kutumia vyombo vyake, itakapobaini palikuwa na mapungufu, isisutwe taarifa hiyo, bali ipokelewe kwamba, ilikuwa ni changamoto kwa maslahi ya ustawi wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ijadili mantiki ya taarifa si mabishano yaliyoweza kuwa katika mijadala iliyotokea Bungeni. Ninaomba tukumbuke kwamba, Bunge na Serikali ndiyo kiungo cha amani na utulivu, wananchi wanatazama tunakwenda vipi. Hivi sasa tumeshaibua mgutuko kwa wananchi kwamba, maisha yanapanda kwa sababu ya watu wachache, wanaotumia madaraka kwa maslahi binafsi, kunyonya Taifa letu. Kwa hiyo, mgutuko huo ni lazima sasa upate majibu kwa upungufu wote uliobainishwa katika ripoti na Serikali ije na hotuba ya kuweza kuwatoa hofu wananchi kwamba, zinachukuliwa hatua na hatua hizo zidhihirike.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu anayeweza kusukuma gari akiwa amekaa ndani ya gari, sisi Wabunge tumetimiza wajibu wetu, kwa hiyo, ninaomba Serikali nayo itimize wajibu wake kwa wananchi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, gari likipata pancha, lazima uondoe tairi. Uongozi wa Chama cha Mapinduzi, umeshaondoa matairi yaliyopata pancha, tumeweka mapya *aluta continua*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali izibe vitobo vidogo vidogo, ambavyo vitakuwa vinaibua masuala ambayo yatawachanganya wananchi. Tumezungumza mengi na magazeti na vyombo vya habari vinahabarisha, kwa hiyo, ninaiomba Serikali mpya sasa sherehe ya *birthday* imekwisha, waanze kazi ya kuhakikisha kwamba, vitobo vidogo vidogo wanaviziba, kwa sababu paa la nyumba linalovuja dawa yake si kuhamisha kitanda, dawa yake ni kuziba vitobo. Kwa hiyo, ninamwomba Mkuu wa Serikali, asimamie hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninapenda kusema kwamba, kujua mambo mengi sio kosa, kosa ni kutokujua usahihi wa mambo. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ihakikishe itakapokuwa inaadabisha, izingatie uwazi na ukweli. Isije ikatokea samaki mkubwa kumeza samaki mdogo, wasije wakatolewa watu kafara. Ninakumbuka Mheshimiwa

Rais wetu, amewahi kulitangazia Taifa hili kwamba, anajutia kumfukuza Katibu Mkuu kwa kuhabarishwa vibaya. Ninaomba sisi Bunge letu pamoja na ibuko la Kamati yetu hii, tuhakikishe kwamba, watakaokuwa na upungufu waadabishwe kwa uwazi na ukweli ili kila mtu apate haki ya kusikilizwa. Inawezekana tukaadabisha mtu kwa jambo dogo kumbe mzizi upo, lakini jipu lile bila kuondoa mzizi hatuwezi kulitoa. Tusiwajibishe watu kwa sababu tumeamua kuwaajibisha, kumbe ule mzizi upo chini. Kwa hiyo, ninaomba tung'oe mizizi na ufanywe utafiti wa kuhoji kila mtu ambaye ana makosa kwamba, kwa nini hakutekeleza, je, ilikuwa ni kwa sababu ya "hewala bwana." Kwa hiyo, ninaomba tuendelee.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kusema kwamba, biashara zina vishawishi na ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahakikishe anazingatia kwa haraka sana, masuala ya maadili. Meme ya taarifa hii ya suluba kwa vitendo vya ufisadi na sio suluba kwa mtu, ninaomba ipokelewe hivyo. Kiu ya taarifa hii imekidhi matarajio ya wananchi kwamba, Bunge letu na Serikali tunakwenda. Ninaipongeza Kamati hii na maamuzi yake. Sasa wananchi wanasubiri watachukua hatua gani na Serikali idhibiti uwongo wa kuthibitishwa na uwongo. Ninaomba Serikali idhibiti uwongo wa kuthibitishwa na uhodari wa uwongo na isije ikatumia mwenzetu na si mwenzetu katika maamuzi yake. Ninaomba sana tulinde mafanikio tuliyoyapata kwa imani ya wananchi kwa kuhakikisha kwamba, Serikali inakuja ni kheri kuombewa msamaha lakini akajulikana mtu alikuwa ni mkosefu. Hoja iliyo mbele yetu ni unyonyaji wa Taifa, hoja iliyo mbele yetu si mtu kwa mtu. Kwa hiyo, hoja iliyopo ni unyonyaji.

Mheshimiwa Spika, wadogo wanasema, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kwa hiyo, ninaomba tukubali kwamba, Serikali itathmini tulipotoka. Kuna mivumo mingi kama ilivyosemwa ya Benki Kuu, Rada, Helikopta na kuna mambo mengi, lakini ninaipongeza Awamu ya Nne kwa dhati kabisa, kuhakikisha kwamba, inatekeleza maelekezo ya CCM asilia. Mungu amjalie Mwenyekiti wetu na wewe Mheshimiwa Spika kwa ujasiri, kwa sababu ungeyumba leo tungekuwa hatupo katika mstari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutakulinda, tupo pamoja na wewe na Mungu akujaalie, akuvushe na mitihani ambayo itakuwa labda ya nguvu za giza. Ninaiomba Serikali kwamba, lugha iliyotumika ya taarifa hii isichukuliwe vibaya, ilikuwa ya kuibua msisimko wa kugusa hisia na kukonga mioyo ya kukemea uhalifu wa dhuluma. Kwa hiyo, ninaomba isichukuliwe kwamba, labda Mheshimiwa Mwenyekiti aliyewakilisha, alikuwa na ubinafsi. Bunge ninaamini tutaendelea kufanya kazi ya dobi. Kazi ya dobi ni kung'arisha nguo na kutoa uchafu, kwa hiyo, Serikali ijiandae kwa usanifu wa kuhakikisha kwamba, upungufu unadhibitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, mtu anayekusikiliza, hawezi kudhani unatoka Maswa, atadhani unatoka Mji Mkongwe. Tunaendelea Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. ABOUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie kidogo kuhusu suala hili ambalo liko mbele yetu. Mimi nitazungumza mambo mawili tu. La kwanza ni kuishauri Serikali na la pili ni kujaribu kuboresha haya maazimio ambayo yalitolewa na Kamati Teule. Katika kufanya hivyo, nitazungumzia katika nyanja nne. Ya kwanza ni TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa).

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi kama hili jina kweli ndilo hasa la chombo hiki, kwa sababu mambo ambayo yamefanywa na chombo hiki ambacho kiliundwa na Mheshimiwa Rais, kwa ajili ya kumsaidia katika shughuli za utendaji mzuri na Utawala Bora wa Serikali, lakini badala yake utaona kwamba, chombo hiki kimemwangusha sana. Kutokana na hayo, lile lengo hasa ambalo Mheshimiwa Rais alikiundia chombo hiki halikupatikana, kilichofanya chombo hiki ni kubatiza na kubariki rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa chombo kikubwa kama hiki kimefanya kama hayo, kwa kweli ni kosa kubwa ambalo ninahisi Serikali lazima ichukue hatua katika hayo. Kwa hiyo, ushauri wangu katika suala hili kwa Serikali ni kwamba, watendaji wakuu wa chombo hiki akiwemo Mkurugenzi Mkuu, pamoja na maofisa wengine ambao wamehusika ni lazima wawajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kupanua lile azimio lililotolewa katika Kamati Teule la kusema kwamba, chombo hiki kimeshindwa kufanya kazi, chombo hiki kimetia aibu kwa Serikali na nchi na hivyo wanaohusika wote wawajibishwe na kwamba, chombo hiki kina haja ya kuundwa upya. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu Utawala Bora. Ninashukuru kwamba, katika suala hili, Serikali imeonyesha lile jukumu la *individual responsibility* na *collective responsibility* na ndiyo maana Mawaziri wawili wale wakajiuzulu na Waziri Mkuu kwa kuchukua *collective responsibility* naye akajiuzulu. Katika Utawala Bora haya hayatoshi, hii ni sehemu moja tu, sehemu nyingine bado zipo ili kuonyesha kweli kwamba, Serikali imeazimia hasa kutekeleza Utawala Bora na sehemu hizo ni zipi. Ya kwanza, kuna njia za watu hawa na wengine kama hawa kutaifishwa mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninaomba nitofautiane kidogo na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri aliposema kwamba, zile fedha ambazo *TANESCO* wanalipa zipelekwe Serikalini, yaani Serikali ndiyo walipe. Mimi sifikirii kwamba hayo ni sawasawa, kwa sababu ikipelekwa Serikalini au *TANESCO* ikiwa inalipa, suala ni kwamba, wananchi ndiyo wanaobeba gharama hizi. Sasa nini la kufanya? Kwa sababu fedha hizi zipo katika mifuko ya hawa wachache, basi ndiyo tunasema kwamba, wataifishwe fedha hizi zipatikane na zifidie katika hiyo hasara ambayo imepatikana. La pili, ambalo ningeomba liingizwe katika maazimio ni kwamba, hatua za kisheria baada ya hapa zichukuliwe ikiwa ni kwa mmoja au wote kwa pamoja, ili sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, suala langu la tatu katika hoja hii ni Mkataba wa *Richmond*. Bahati nzuri nimeupitia Mkataba huu na ninasikitika sana, unapousoma kwa kweli unatokwa na machozi kwa masuala mawili muhimu. Je, hawa watu ambao wameutazama walikuwa hawaoni au ni kwa sababu gani walikubali utiwe sahihi? Lakini la pili, pengine nikataka kuji-*console* kwa kusema kwamba, pengine labda sheria zangu nilizosoma ni za zamani. Mwaka 1972 ndipo niliposoma Chuo Kikuu. Sasa pengine sheria zile za mwaka 1972, zimeshapitwa na wakati na kwa maana hiyo, sheria za wakati huu pengine zina maudhui mengine, kitu ambacho sifikirii.

Mheshimiwa Spika, ukitazama vifungu vya Mkataba ule kwa mfano, vifungu vya 12(1)(g), 12(3), 4(4), 3(4) na kifungu cha 15, hivi vyote vinaonyesha dhahiri kwamba, hawa watu waliokuwa wanashughulika na Mkataba huu walikuwa ni wazembe, hawana imani na nchi, walikuwa ni watu ambao pengine walikuwa wakifanya kwa maslahi yao, kwa sababu gani? Kwa sababu kifungu cha 12 kwa mfano, imeelezwa wazi pale kuna hatua za kuvunja Mkataba na Mkataba unasema au Sheria za Mikataba zinajulikana kwamba, kuna *elements* ambazo ikiwa ama mmoja wao amezivunja, basi Mkataba unaweza kuvunjwa kwa mfano, kunapokuwa na *misrepresentation, incorrect statement*, mtu mmoja aliyeingia kwenye Mkataba hana *legal status*, hayo ni mambo ambayo unaweza kuvunja Mkataba. Sasa haya yote yapo katika Mkataba wa *Richmond*, sioni sababu kwa nini Mkataba huu hauvunjwi.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 4(4) kimeeleza wazi kwamba, haki ya *TANESCO* inaweza kuvunja Mkataba na kudai fidia. Sasa *TANESCO* na Serikali, kwa nini hawakuweza kuvunja Mkataba na kudai fidia, badala yake wakajitia katika gharama ambazo zimewabebesha wananchi gharama kubwa sana. Hii ni kasoro kubwa sana ya watendaji wetu na ndiyo maana nikasema kwamba, watu wa aina hii ni lazima wachukuliwe hatua. Sasa ushauri ninaotoa kwa Serikali ni kwamba, Mkataba huu una vifungu ambavyo tunaweza kuvunja Mkataba kama Serikali, kwa hiyo, ninaishauri Serikali iweze kuuvunja Mkataba huu mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna watu kama akina Ndugu Chidowu wa *Attorney General's Chamber* na Ndugu Godson Makia, Mwanasheria wa *TANESCO*, hawa ni wanasheria wa zamani ni wanasheria ambao mimi ninahisi wangeweza kuwa na imani na Serikali. Haya majina yao ni mazuri tu, Godson mtoto wa Mungu huyu. Ajabu mtoto wa Mungu huyu anafanya mambo ambayo ni kinyume kabisa. Sasa ushauri wangu kwa hili ni kwamba, hawa lazima wachukuliwe hatua ya haraka iwezekanavyo na wasiwekwe tena katika vyombo hivi kwa sababu wataendelea kututia hasara na kuwabebesha mzigo mkubwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama suala lingine la Mkataba, tujiulize Serikali au sisi Tanzania tulikuwa tunahitaji *megawatts* 105 na *megawatts* hizi Marekani kule walikokwenda Tume, walisema kwamba, kulikuwa na mashine ambazo zinauzwa ambazo kila jenereta moja ni *megawatts* 17.5 na kila jenereta moja ni dola 7.5 milioni. Sasa hawa watu ambao wamepewa dhamana hii, wangekuwa kweli wana uchungu na Tanzania na Watanzania, wangeweza kununua majenereta haya sita kwa dola 45 milioni na wakishayanunua yakawa ni ya kwetu. Gharama zote hizi zisingeweza kutokea, lakini

sasa hapa ndiyo ninajiuliza; kwa sababu gani waliingia katika kukodisha na halafu kukodisha kwenyewe utaona kuna kifungu cha 15 nilichokitaja mwanzo, ukikisoma utatokwa na machozi, kwa sababu kifungu hicho kinasema kila kitu ambacho kinapaswa kufanywa na huyo *Richmond*, basi watakifanya *TANESCO*, maana yake mpaka kipuri ambacho kimeharibika hilo ni tatizo la *TANESCO*?

Mheshimiwa Spika, ninajiuliza Mkataba huu wenye vifungu namna hiyo ni mahali gani duniani ambapo upo kama si Tanzania na *TANESCO*? Kwa kweli ni kitu cha kusikitisha sana. Kitu ambacho ninakisema katika mjadala huu ni kwamba, ninaiomba Serikali kwanza, ifute Mkataba huu. La pili, ifute au iunde upya hii TAKUKURU na wale maofisa wake kuanzia Mkurugenzi, awajibishwe pamoja na wasaidizi wake. Halafu wale wote ambao wamehusika, mali zao zifilisiwe na pia wapelekwe katika vyombo vya Sheria ili Sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, pamoja na mapendekezo ya ziada niliyoyatoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijajikita katika hoja ambayo ipo mbele yetu, ninapenda nitangulize maneno yafuatayo: Sina uhakika lakini nilipata kusikia ndiyo maana ninaogopa kusema kwamba ninamnukuu, lakini sijapata kuona kiongozi katika Afrika kama Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Wakati fulani, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, katika moja ya hotuba zake ambazo nilipata kuzisikia, anasema kwamba, kulikuwa na Mgiriki mmoja aliwahi kujitapa tu kusema kwamba, ameiweka Serikali mfukoni. Hayati Baba wa Taifa, akamtia ndani, hakumtoa mpaka Baba Askofu Macharious wa Cyprus alipokuja kumwomba na kwa heshima tu akamtoa.

Mheshimiwa Spika, si huyo tu, katika hotuba zake pia amewahi kusema kuhusu mmoja katika Viongozi wake wa Serikali ambaye alipatikana na hatia, akampeleka gerezani akapigwa viboko kumi na mbili wakati anaingia gerezani na akapigwa viboko kumi na mbili wakati anatoka akamwonyeshe mke wake. Huyo alikuwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Leo tunacheka Sh. 152m kila siku tunawalipa *Richmond*; ndiyo aina ya Viongozi tulionao sasa, ambao wanaingia katika mikataba mibovu inayoliangamiza Taifa na kuwapa mzigo maskini wa nchi hii. Sasa maadam Kamati hii Teule ya Bunge imeanza na *Richmond* ni sawasawa na kuinua zulia na sasa tusafishe nyumba yetu. Uchafu ni mwingi na wala sitaki kwenda huko katika aina ya mikataba inayofanana na huu wa *Richmond*, tumeanza tuendelee na mikataba yote.

Mheshimiwa Spika, siku ile baada ya Mwenyekiti wa Kamati Teule kuiwasilisha taarifa yake na wewe Mheshimiwa Spika kuliahirisha Bunge, nilipokuwa ninapita pale nilinunua gazeti miongoni mwa magazeti makini tu ya kila wiki, nilipokuwa ninasoma lile gazeti katika makala moja, Mwandishi wa makala ile ameandika: "Rais Kikwete mfikishie Bush kilio cha wakulima wetu." Hapo ndipo tulipofikishwa Watanzania. Mwandishi wa makala ile aliendelea kusema: "Nasi pia tunahitaji kujengewa uwezo wa kutoa ruzuku kwa wakulima wetu." Hii ina maana kwamba, hatuwezi kuendesha mambo

ya Serikali yetu mpaka tumwombe Bush, ndipo Watanzania wamefikishwa hapo. Tunaomba hata ruzuku ya kuwapa wakulima, mabilioni ya fedha yanapotea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti, tulipata matatizo sana, Kamati ya Bunge ya Miundombinu kulikuwa hakuna fedha kabisa ya miradi ya barabara, tukalazimika kwenda kumwona aliyekuwa Waziri Mkuu, tukamwambia hali hii sijui tutaielezaje kwa Watanzania, ikafikia mahali wakafanya marekebisho fedha zikapatikana na ikasifiwa bajeti ile kwamba ni bajeti ya aina yake, ambayo ilikuwa imetenga shilingi bilioni 774.2 kwa ajili ya Wizara ya Miundombinu, sawasawa na asilimia 12.8 ya Bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha wanazolipwa *Richmond*, shilingi bilioni 200 ni sawasawa na asilimia 25.8 ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Kwa maana hiyo ni kwamba, fedha anayolipwa *Richmond* ni sawasawa na fedha yote iliyotengwa katika bajeti ya mwaka huu, kwa ajili ya barabara kwa fedha za ndani ambazo ni shilingi bilioni 202. Hii ni hatari! Fedha anayolipwa *Richmond* leo ni sawasawa na matumizi ya fedha za maendeleo zinazotolewa kwa Mkoa wa Rukwa, shilingi bilioni 11, sawasawa na matumizi ya miaka 18 au 20, tunampa *Richmond* na bado fedha hiyo iliyopelekwa Rukwa shilingi bilioni 11, wakatumwa Mawaziri kwenda kusifia. Fedha anayopewa *Richmond* ni sawasawa kama itapelekwa kila mwaka kwa Mkoa wa Rukwa kwa miaka 18 mpaka miaka 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo barabara za lazima kabisa zimekosa fedha. Barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora, haikutengewa fedha, tunategemea wahisani watusaidie. Fedha anayolipwa *Richmond*, ingeweza kutengeneza kilomita 400 za barabara ya lami kutoka Tunduma mpaka Mpanda, tunangojea *MCC* na hawatupi shilingi bilioni 200 ambazo sisi tunampa *Richmond.* Reli imetengewa shilingi bilioni kumi na fedha yenye siyo ya ndani, tunangojea wahisani na wafadhili watupe fedha hiyo, sisi tunapeleka kwa *Richmond!*

Mheshimiwa Spika, inatia uchungu sana, lazima sasa tujitazame kama kweli tuna dhamira na nia ya kuwapelekea watu wetu maendeleo, matumizi kama haya ni lazima tuyasimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajisikia vibaya sana, lakini ninalazimika tu, ninaona sasa nijikite katika mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii ambayo nimeisoma katika ukurasa 130 na 131, kwa ruhusa yako ninaomba ninukuu: "Hivyo basi, *Richmond Development Company LLC* ni Kampuni ya kimakusudi, ya kimkakati ambayo haikamatiki, haishtakiki, haipigiki faini na haiadhibiki kwa lolote lile litakalofanyika kwani haina uhai wa kikampuni." Mwisho wa kunuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazugumza na hewa haipo, haikamatiki, haishtakiki na tunaendelea kulipa fedha, analipwa nani? Katika mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kifungu cha tano kinazungumzia Mkataba, jinsi ambavyo umesheni makosa kadhaa ya kisheria. Sasa nilikuwa ninafikiri pamoja na udhaifu wa watendaji katika Ofisi ya

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni lazima Mkataba huu usitishwe. Kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali haiwezi, basi tuwaombe *Law Society* waingilie kati, Mawakili katika nchi hii wenye uchungu na nchi hii na wenye uzalendo, walisimamie hili la kusitisha Mkataba na *Richmond*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Kamati, kifungu cha pili kinazungumzia kuhusu kuchunguzwa upya mikataba na taarifa itolewe. Nilikuwa ninapenda kuongezea kwamba, baada ya uchunguzi huo kukamilika, taarifa iletwe Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni kuhusu mapendekezo yaliyopo katika kifungu namba saba, kinachozungumzia Wajumbe wa *GNT,* wenzangu wengi wamekwisha kulizungumzia hilo. Nilichokuwa ninataka kuongezea ni kwamba, nchi hii tumekuwa na tabia tu kuwajibishana, ukimfukuza kazi inatosha, akijiuzulu inatosha. Wameleta dawa hapa wamezirudisha wamewajibishwa. Nilikuwa ninataka twende mbali zaidi; hawa wote ambao wamekuwepo katika hii *GNT* kwanza, wafukuzwe kazi. Pili, wasilipwe mafao yao. Tatu, wanyang'anywe nyumba za Serikali kama walikopeshwa na mwisho wapelekwe Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie tu kwa neno moja, kwa ruhusa yako, ninampongeza sana Waziri Mkuu, ndugu yangu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Ninamwomba kabla hajaanza ziara zake za kikazi arudi nyumbani, njoo Mpanda tufanye matambiko na tukupe zana za kufanyia kazi. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika sehemu ya Taarifa hii ambayo nimeshiriki katika kuiandaa.

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi ya kwanza kabisa, kuwashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati Teule, kwa jinsi tulivyoshikamana tukawa kitu kimoja, tukatunza siri na tukaweza kuandika taarifa hii usiku na mchana na leo ipo inajadiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nichukue nafasi hii, kuishukuru Sekretarieti, kwa kujitahidi kuweka siri. Ninajua Mwenyekiti atachukua hiyo nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, shukrani nyingine zimekwishatolewa na pongezi kwa wale ambao wamepata nyadhifa mbalimbali, sitarudia huko. Nimesimama ili nichukue fursa hii, kumsaidia Mwenyekiti wangu wa Kamati, mambo ambayo tutahitaji kuyazungumza ni mengi. Kwa hiyo, tumeamua kugawana, nitazungumza machache na wajumbe wenzangu nao watafanya hivyo na hatimaye Mwenyekiti wetu atahitimisha.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo tumesikia Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Ninaomba niwashukuru sana, wote ambao wamesimama wengi wametuunga mkono, ukiondoa wachache waliozungumza mwanzoni kabisa, ambao mimi

ninaamini walizungumza kwa jazba, vilevile ninaamini kwamba, hawakuisoma taarifa yetu kwa umakini, bila shaka hawakupata muda wa kutosha na Mwenyezi Mungu awasamehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge waliozungumza mwanzoni kabisa na sitaogopa kumsema ni Mhesimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, alisema kwamba, ana wasiwasi na jambo hili. Nimeona linarudiwa mara kwa mara, alisema ana wasiwasi kwamba, yeye alikuwa anaamini kwamba, *Richmond* hawakulipwa hata senti tano. Nimeona katika taarifa yetu tumesema kwamba, *Richmond dollar* milioni kumi. Ninataka niyaweke mambo sawa hapa. Hakuna mahali popote ndani ya taarifa ile, ambapo sisi tumesema kwamba, *Richmond* amelipwa *dollar* milioni kumi. Hivyo, ni dhahiri mwenzetu huyo pia haikusoma vizuri taarifa yetu.

Mahali ambapo ameshindwa kupaelewa ni pale tuliposema kwamba, kulikuwa na dhamira ya makusudi ya kutaka kumsaidia *Richmond* alipwe fedha za awali *advance payment* ya *dollar* kumi ili kumwezesha *Richmond* kununua mitambo kama alivyoeleza yeye mwenyewe, kununua mitambo na kuisafirisha kuileta Tanzania. Kwa utaratibu wa biashara za nje, huduma au kupata bidhaa kutoka nje ya nchi kuja nchini kupitia mabenki, chombo kinachotumika ni kufungua kitu kinachoitwa Barua ya Dhamana ya Benki *(Letter of Credit),* kwa kifupi nitakuwa nikisema *LC.*

Mheshimiwa Spika, ili kumwezesha *TANESCO* kumlipa *Richmond* kama angetimiza masharti yake, ilifunguliwa *LC* ya *dollar* milioni 30,696,598. Hii ni dhahiri inaonyesha kwamba kwanza, Tanzania tulikuwa nazo *dollar* hizo. Cha kujiuliza hapa ni kwamba; kwa nini Benki, maana yake unapofungua hiyo *Letter of Credit* lazima iwe *confirmed* na Benki ya kule ambako unatarajia mteja wako apokee fedha hizo; Benki ambayo hapa Tanzania walifungua hiyo *Letter of Credit, City Bank* ya hapa Tanzania kwenda kwa *City Bank* New York Marekani, ambako ndiko alipo mteja wetu *City Bank* ya Marekani, ikakataa kufungua *Letter of Credit on behalf of Richmond;* kwa nini walikataa, hilo ndilo swali la msingi la kujiuliza, kwa nini walikataa?

Walisema walikataa kwa sababu walikuwa hawamtambui vizuri wala hawawajui uwezo wao. Benki iliyopo Marekani huko huko aliko *Richmond;* hivi kweli *Richmond* ipo Marekani! Huyo aliyetajwa kwa jina hilo aliyeko kule ni yule anayetengeneza mambo ya *Printing*. *(Makofi)*

Sasa ninaomba sote tuelewe, hatukusema *Richmond* amelipwa *dollar* milioni kumi, kwa sababu jitihada zote zilizofanywa na wataalam wetu wote za kumtaka *Richmond* apewe *advance payment* ziligonga ukuta. Wizara ya Nishati na Madini walifanya hilo kumsaidia, Wizara ya Fedha ikasema hapana, haturidhiki, Wizara ya Nishati na Madini ikaendelea kusema eti Wizara ya Fedha imekubali kumbe si kweli na vielelezo vipo, kwenye lile *book* kubwa, mtaona karatasi zote zipo. Kwa hiyo, ni kweli *Richmond* hakulipwa hata senti tano, kwa sababu alishindwa kutimiza masharti ya *Letter of Credit*. Alichokuwa anataka ni *advance payment;* utalipwaje *advance payment* bila kutoa huduma? Toa huduma na uthibitisho wa utekelezaji wa huduma halafu ndiyo

uchukue fedha, mwenzetu alitaka achukue fedha atie mfukoni kabla hajatoa huduma. *Letter of Credit* haikutoa nafasi ya namna hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, alishindwa *Letter of Credit* ile ikakaa benki ikiwa imeshafunguliwa kwa miezi akashindwa kutimiza masharti mpaka ikafikia muda wa ku-*expire.* Sasa hapo ndipoWanasheria watusaidie; huyu akashindwa kutekeleza wajibu wake, mkataba kweli bado upo? Hapa ndipo mahali pa kujiuliza. Nilitaka nifafanue hilo. Aliyekuja kurithi Mkataba huyu Dowans, naye sasa alipokuja akafunguliwa *Letter of Credit* mpya kwa sababu ile iliyokuwa imefunguliwa kwa *Richmond* ilikwishakufa. Akafunguliwa *Letter of Credit* nyingine mpya huyo Dowans ya kiwango kile kile cha 30,696,598 ili atekeleza Mkataba ule. *(Makofi)*

Sasa *Richmond* tatizo linakuja hapo, wakati *Richmond* anaomba hizo *dollar* milioni 30, alileta vielelezo vya kuonyesha kwamba, anahitaji hizo fedha ili naye aweze kununua mashine na kuzisafirisha. Kwa hiyo, akaleta kitu kinaitwa *Pro-forma Invoice* ya *Air-flight* ya kuonyesha kwamba, atasafirisha mashine ile kutoka huko atakakoitoa kuileta Tanzania kwa *dollar* 4,865,000. Sasa cha kujiuliza; hivi kweli kiwango hiki ni sahihi? Hilo ndilo la kwanza. *Flight* ya kutoa mtambo wa megawati 22.5 kutoka huko uliko kwa gharama hii, lakini wataalam wetu walisema hicho kiwango ni sahihi.

Sasa Dowans aliporithi mkataba akaanza utekelezaji kwa kutumia *Letter of Credit* yake ile ya kiwango cha *dollar* milioni 30. Tunachosema hapa kwa Dowans sasa ni kwamba, aliye-*draw* kutoka kwenye *Letter of Credit* ile zaidi ya *dollar* milioni 30 zilizopo pale; idhini ya kutoa fedha zaidi ya hizo ilitoka wapi wakati *LC* yake ni ya *dollar* 30,696,598? Ukitazama kwa umakini, utaona kiwango ambacho kimevuka kiasi kile ndiyo kile kiwango ambacho walikuwa wamesema *Richmond* wangekitumia kusafirishia mashine ile kuileta Tanzania. Hapakuwa na *Letter of Credit* mpya iliyofunguliwa. Kwa hiyo, tunashangaa kwa nini Dowans alichukua *dollar* milioni 35 badala ya milioni 30! Tunasema hapa na katika maelezo yetu tutasema kwamba, Benki Kuu lazima iwajibishwe kwa hilo kwa sababu walichukua zaidi ya kiwango kilichokuwa kimewekwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhuisha mkataba kumetuletea madhara gani? Kwanza, *Richmond* alishindwa kutekeleza mkataba wake, lakini katika Mkataba wake alikuwa na tarehe maalum inaitwa *Commercial Operation Date*, siku ambayo mitambo itakuwepo hapa na ataanza kuzalisha umeme; ilikuwa ni tarehe 4 Februari, 2007, ilipofika *Richmond* alishindwa na akahuisha mkataba wake.

Sasa tatizo linakuja; Dowans anakuja, watu wanaingia mkataba na Dowans aliyerithi Mkataba wa *Richmond*, lakini ile *Commercial Operating Date* inabadilishwa, kwa manufaa ya nani? Kwa mfano, kama tungeendelea na mkataba wa mwaka mmoja kwa *Richmond*, mkataba huo wa mwaka mmoja ungekuwa umekwisha tarehe 4 Februari, 2007, leo tungekuwa hatuna *Richmond* tena kimkataba. Kwa kuipa *Richmond* mkataba wa miaka miwili badala ya mwaka mmoja, ndiyo imetupelekea sasa kwenda mbele zaidi na *Richmond* mkataba wake wa miaka miwili badala ya kwisha, Februari, 2007 ni mpaka mwezi Februari, 2009.

Mheshimiwa Spika, suala hili limetuongezea mzigo mkubwa. Tumechukua *Commercial Operating Date* ya Dowans kuwa ni tarehe 3 Oktoba, 2007, yaani yule kashindwa, halafu tunatengeneza *Commercial Operating Date* mpya kwa mtu mwingine, wakati ambapo tungeweza ku-*negotiate* naye, kwa sababu huyo anairithi ya *Richmond*, ilikuwa inakwisha mwezi Februari, 2007. Wewe unachukua dhamana ya mikataba yote, kwa nini tunampa tena miaka miwili, tena inaanza mwezi Oktoba, maana yake tumempa *extension* nyingine ya miezi mine; muda wa mkataba wake ni miaka miwili na miezi minne. Haya ni matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema katika Halmashauri zetu, kuna matatizo makubwa sana, fedha zinaliwa kweli kweli, hata Mheshimiwa Rais amesema kuna mchwa wanamaliza Halmashauri zetu. Madiwani hawashiriki katika kusimamia *tender*, siyo Wajumbe katika *Tender Committee*. Sasa tunasema tutoke ngazi hii ya Bunge, hebu tufikirie uwezekano wa namna ya kuzisaidia Halmashauri. Halmashauri zitawezaje kuwa na fursa ya kuweza kuunda Kamati Teule kama hizi, zisimamie matumizi ya fedha katika Halmashauri zetu, ziweze kuingia ndani kuchunguza mikataba na kusimamia matumizi ya fedha za umma?. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba hili liwe mojawapo ya pendekezo la ziada katika Kamati yetu na Waheshimiwa Wabunge wote, tunatoka katika Halmashauri zetu, tunaelewa kinachoendelea. Pendekezo hili jipya, tuliunge mkono ili watengeneze uwezekano wowote kurekebisha sheria ili nao waweze kupata fursa ya kuunda Kamati Teule, ambazo zitafanya kazi sawasawa kama Kamati Teule hizi za Bunge zinavyofanya kazi. Kwa njia hiyo, tutakuwa tumelisaidia Taifa, kulinda fedha za umma na kuhakikisha matumizi bora ya fedha za Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokuwa tumejipanga, ninaishia hapa ili wenzangu wapate fursa ya kuendelea. Ninaomba kusema kuwa, ninaunga mkono hoja ya Kamati Teule. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Herbert J. Mntangi ahsante sana na hususan kwa pendekezo lako hilo, ambalo ni moja ya mafunzo tunayopata kutoka kwenye sakata hilo. Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo. Kwanza, nami ninawashukuru Wajumbe wa Kamati Teule na kwamba, mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati hiyo na ninawashukuru kwa namna tulivyoshirikiana kufanya kazi ile. Kumbe inawezekana kabisa, watu kukaa pamoja wakaacha maslahi ya vyama, wakawa katika maslahi ya nchi. Ninashukuru kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwa wenzangu hao, ambapo mimi kutoka Kambi ya Upinzani nilikuwa peke yangu. Hakukuwa na tofauti yoyote, tulifanya mijadala tukaelekezana na tukafanya kazi ile kwa ufanisi mliouona. Kwa hiyo, hilo ninashukuru, kumbe inawezekana na wengine waige mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, kwa vile mwenzangu amekwisha fafanua baadhi ya vipengele na amelazimika kuitaja Kampuni ya Dowans na kuna Mheshimiwa

Castor R. Ligallama na Mheshimiwa Said A. Arfi, walikuwa wanahoji kwamba, hiyo *Richmond* ni kampuni hewa; kwa hiyo, hizo milioni 152 zinalipwa wapi?

Mheshimiwa Spika, ni vyema nichukue nafasi pia nilifafanue; ni kweli *Richmond Development Company LLC* ni kampuni hewa, lakini fedha zinalipwa kwa Dowans. Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke kwamba, baada ya Kampuni hiyo hewa kudanganya ilivyodanganya na wakashindwa vipengele vya kupata hiyo fedha, waliweza kuhuisha mkataba mnamo mwezi Desemba, tena wakati huo mgao haukuwepo tena. Waliweza kuhuisha mkataba, ukachukuliwa na Dowans na Dowans kwa vile walirithi ule mkataba ndiyo wanaopata hizo fedha. Kwa hiyo, hilo nilipenda niliweke wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, alikuwa anasema haina raha kuzungumzia hoja ambayo tiba yake imekwisha kupatikana. Tiba imepatikana nusu, lakini bado nusu nzima au nusu na robo ya tiba, kwa hiyo, bado utamu ungalipo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ningeomba sasa na mimi nitoe mchango wangu katika ripoti hii, sehemu ambazo labda nikizizungumza hapa hadharani, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wanaweza wakafaidika.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa nizungumzie hii taarifa ya ukame; imedhihirika kwamba, kitengo chetu cha Hali ya Hewa, kinatoa takwimu na *data* sahihi kwa miaka yote na taarifa hizo zinawasilisha kunakohusika mpaka kufikia Baraza la Mawaziri. *TANESCO* kuna kitengo maalum cha *Hydrology* cha kutazama mwenendo wa maji kwenye mabwawa na wao wanafanya kazi hiyo hiyo na taarifa zinapelekwa kunakohusika. Kwa hiyo, hali ya ukame iliyolikabili Taifa, ishara zinaonyesha katika *drawings* tulizozipata na kila kitu na Serikali ina taarifa zilianza mwaka 2002, 2003, 2004, 2005 na 2006, ndiyo yakatokea yaliyotokea. Kwa maana hiyo, ishara zilikuwepo kwa muda mrefu na tungeweza kujiokoa na tatizo hili kama Serikali ingekuwa makini, kuzipitia takwimu hizo na kujiweka tayari kama wanavyofanya nchi majirani zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la *emergency* inaonekana hapa nchini kwetu ni kitega uchumi maalum, kinachotegemewa kitekelezwe kwa kutumia kisingizio cha *emergency*. *Emergency* hizo zimetupelekea leo kuwa na makampuni; kabla ya hiyo *Richmond*, tumekuwa na *IPTL, AGGREKO, SONGAS* na *ALSTOM*, yote hayo yamekuwa kwa mfumo wa *emergency*. *IPTL* na *SONGAS* muda wao miaka ishirini ishirini; sijui *emergency* hiyo ilikuwa ya namna gani? Hatuwezi kama Serikali kwenda kwa mfumo wa *emergency* kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala lilikuwa lina taarifa mapema. Hatuwezi kwenda kwa *emergency* na ndiyo maana hata katika Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kukawa kuna pendekezo lile la kuwa na *Power System Master Plan*, ambayo inaombwa kila siku katika Bunge hili lako Tukufu. Kwa maana hiyo, kilichotokea hakikuwa kitu cha *emergency*. Ukame ulitokea tunakiri, lakini taarifa zilikuwepo na tungeweza kujipanga mapema. Hilo lilikuwa la kwanza ambalo nilitaka lifahamike kwa uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni udanganyifu unaofanywa na nianzie kwa walewaliozungumzia kwamba, huyo Mohamed Gire anasema hakulipwa fedha. Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, amekwisha kulijibu la udanganyifu, *attempt* alikuwa nayo, lakini kusema kwamba, mradi huu ulikuwa na thamani ya *dollar* milioni 83 nayo ni udanganyifu na pia amedanganya bado.

Mheshimiwa Spika, udanganyifu huu umeanzia mbali. Nichukue nafasi hii niseme kwamba, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilidanganywa na Bunge lako lilidanganywa. Nifafanue kusema kwamba, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilipohoji gharama za mradi huu na ikajibiwa ni bilioni 172.9, wastani wa *dollar* za Kimarekani milioni 134, wakati huo tunaelezwa mambo hayo, Wizara na *TANESCO* walikuwepo, walitudanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya 2007/2008, mimi mwenyewe katika taarifa yangu ya Kambi ya Upinzani, nilihoji mradi huu kutumia *dollar* hizo za Kimerikani milioni 134 na mnakumbuka tarehe 16 Julai, 2007, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati huo, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, alilijibu Bunge lako Tukufu kwamba, gharama za mradi ule siyo *dollar* milioni 134 bali ni *dollar* milioni 102.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lilidanganywa kwa jibu hilo la tarehe 16 Julai, 2007. Kamati Teule, ilipoangalia mkataba la ajabu ni kwamba, hakuna sehemu inayozungumza waziwazi *Contract Sum*, lakini kutokana na *minute* na baadaye kutokana na hizo *LC* alizozizungumza Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, tukagundua malipo wanayotaka kulipwa ya kutamka asilimia 35, ikapigwa hesabu hiyo 30,696,598, ndipo tuka-*drive back* kutafuta *Contract Sum* ni ngapi ndipo tukagundua ni *dollar* milioni 87. Kwa hiyo, tulidanganywa kutoka *dollar* milioni 134 katika *level* ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara na likadanganywa pia Bunge *dollar* milioni 102 mpaka kuona mkataba wenyewe *dollar* milioni 87. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitendo ambacho si kizuri kwa Serikali na inabidi sijui tufanye, namna gani, bahati nzuri Serikali hiyo haipo tena, ipo Serikali mpya, lakini tulidanganywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, nieleze kidogo ambalo litahusiana na takwimu za huko huko kudanganywa. Kudanganywa huko kumetugharimu vibaya sana. Tukiweka uzoefu wa tulipotembelea kule Marekani, kama alivyogusia kidogo Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary; tulikuta kwamba mitambo ya aina ya *PBG 180*, ambayo inazalisha megawati 17.5, tungeweza kuinunua sita kwa thamani ya *dollar* milioni 45, kuisafirisha kutoka Marekani mpaka Tanzania, kwa njia ya kawaida ni asilimia 12 ya gharama pamoja na usafirishaji ingefikia *dollar* milioni 50.4.

Kwa kuokoa, ina maana tungeweza kuokoa zaidi ya *dollar* milioni 34 na mitambo ile ingekuwa ni mali ya Tanzania; haina *capacity charge* na ingekaa hapa tukazalisha umeme aidha wa dharura au wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo dhamira ya hao watu inafahamika. Nchi kama Nigeria wananunua mitambo hapo, tumekuta kwamba, huo wakati ambapo tunaambiwa kuna *emergency*, mitambo hiyo haipatikani, kuna KAWASAKI walikuwa na mitambo minane ya aina hiyo, ambayo walikuwa tayari kuuza au kukodisha, ambapo wao ni *manufacturer*.

Aina ya mitambo yote waliyonayo, bei na kila kitu; tumekuta nchi kama Nigeria wamenunua mitambo kama hiyo kwa bei ya chini. Tumekuta nchi kama Venezuela, wana *order* zaidi ya *generators* 20 pale kwa bei nafuu.

Hiki kitu cha *capacity charge* huko duniani hakuna, wenzetu wanakwenda wanafanya hivi vitu, ila hao tunaowaweka, wanapandia juu kwa kutafuta kujitajirisha haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama itakumbukwa tena mradi wa ALSTOM wa Mwanza, tuliupigia kelele hapa Bungeni, ingawa ni wa mwaka mmoja, tukasema hivi itakuwaje tuna uzoefu wa *IPTL*, leo tunakwenda kukodi mtambo tena unaotumia dizeli, ambao gharama yake ni *dollar* milioni 130.1?

Tumegundua kwamba kuna *track* ambazo zinasafirisha *tubines* ambazo unaweza ukasafirisha hii *gas* yetu asilia, kuna matanki ambayo zile *gas ways* tulizozizungumzia, ambazo ni *upper track* na *gas ways* unaweza ukachimba ukazika matanki ardhini, ukanunua *track* zako 12.

Kwa hesabu tulizofanya mtambo ule ule tungeweza kuzalisha megawati 52 badala ya ile 40 yao na bado tungeweza kunusuru fedha ya Taifa zaidi ya *dollar* milioni 68. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni taarifa na *data* zote za uhakika zipo hapa na hii ni kampuni moja tu tuliyopata taarifa ya haraka haraka. Yapo makampuni mengi kama hayo, leo nchi inaingia katika hasara kwa kutumia mkono wa tatu na bila kuwapa uzoefu na bila kuwatumia wataalam wetu ipasavyo, ambao wanaweza wakatufafanulia vitu hivyo.

Mheshimiwa Spika, mitambo hiyo tuliyoikuta kule ina faida nyingine kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimebakiza wachangiaji wanne na muda uliopo, hata huyo mmoja hauwezi kumtosha. Kwa hiyo, kesho asubuhi tutakwenda kwa utaratibu huu; ataanza Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mjumbe mwingine wa Kamati Teule, halafu nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Mambo ya Bunge, halafu atakuja Makamu Mwenyekiti wa Kamati Teule, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, hawa wote kwa dakika 15, 15 kila mmoja.

Hiyo itatufikisha kwenye saa 5.30 asubuhi, ambapo nitamwita Mwenyekiti, atatufikisha saa 6.30 mchana, kwa sababu ana dakika zisizozidi 60, lakini bado itabidi niwahoji ili tuyapitishe mapendekezo kwa njia ya kawaida na itabidi baadaye nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kuliahirisha Bunge.

Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge ajiandae, kesho ninadhani itabidi tuombe nusu saa ili tusiwe katikati ya shughuli hizi iwe muda ule wa 7.00 umefika tujikute tuna matatizo.

Kwa hiyo, tukienda kwa utaratibu huo, ninaamini kabisa kwamba, yote haya niliyoyatamka saa 7.30 yatakuwa yameisha na basi tutaweza kurudi Majimboni na wenzetu Mawaziri watakwenda katika kazi zao.

Kwa hiyo, kesho wakati muafaka, nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi Waziri Mkuu, ili aweze kutoa hoja ya kuongeza muda kidogo tuiamue. Ninajua katika Kanuni inaruhusiwa kuendelea kuongeza nusu saa tu, lakini sijui kama inapendeza kufanya hivyo wakati ambapo ninataka kumwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitaangalia kesho.

Waheshimiwa Wabunge, leo ni Siku ya Wapendanao *(Valentine Day)*. Kwa kuwa saa mbili kasoro robo inakaribia, ninachoweza kuwatakia ni kuwatakia jioni ya wapendanao, maana yake siku imekwisha.

Ninapenda kutangaza kwamba, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na familia yake, wameandaa hafla maalum ya wapendanao katika Ukumbi wa *Loyal Village Hotel, Area D,* Dodoma ambapo kutakuwa pamoja na mambo mengine; mapochopocho, soda na burudani itakayotumbuizwa na mwanamuziki anayeitwa Zahir Zollo, pamoja na wanawe; Banana Zollo na Ismail Zollo.

Waheshimiwa Wabunge wote, mnakabirishwa kuanzia saa 2.30. Itapendeza wale ambao wanao wenzao, basi kwenda wawili wawili maana yake ndiyo utaratibu wa Siku ya Wapendanao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatakuwepo huko siyo kwa sababu yoyote nyingine, ila sababu kwa utamaduni wa nyumba yetu, siku hiyo huwa tunaisherehekea tukiwa wawili tu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba kuliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.38 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 15 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*